

**UJITAMBUZI NA UTAMBULISHO WA KIJINSIA KATIKA RIWAYA YA *MAISHA*
*KITENDAWILI***

NA

PETER KITANGI KILONZO

C50/83913/2012

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI**

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2015

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Peter Kitangi Kilonzo

(Mtahiniwa)

Sahihi..... Tarehe.....

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Prof. Mwenda Mbatiah

(Msimamizi)

Sahihi..... Tarehe.....

Dkt. Evans M. Mbutia

(Msimamizi)

Sahihi..... Tarehe.....

KUTABARUKU

Tabaruku yangu imwende bibi yangu, Gladys Mbula na mtoto wetu, Amos Mumo kwa kuniulewa, kuniombea, kunihimiza na kunihudumia kwa njia anuwai nilipokuwa ninasomea Uzamili. Pia, walionyesha mapenzi kwangu nilipokuwa ninaendelea na utafiti wa kuandika tasnifu hii. Uvumilivu wao umenitia shime kuandika tasnifu hii.

SHUKRANI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii kuwa hai na kuniwezesha kusoma hadi kiwango hiki. Ingawa elimu ina changamoto zake, ameniwezesha kukabiliana nazo tangu nilipokuwa chekechea hadi hivi sasa. Kama si karama na neema yake singeweza kufikia kiwango cha kuandika tasnifu hii.

Ninatoa shukrani maalum kwa wasimamizi wangu Profesa Mwenda Mbatiah na Daktari Evans Mbuthia. Kando na kuwa wahadhiri wangu nilipokuwa ninaendelea na masomo yangu, mwongozo wao wa dhati wa mara kwa mara ulinifaa sana katika kuandika tasnifu hii. Ninawashukuru sana kwa kutumia wakati wao mwingi katika kunielekeza na kunipa mawaidha katika utafiti na uandishi wa tasnifu hii. Nilipoenda kombo walikuwa tayari kunirekebisha. Kwa hakika, msaada wao kwangu hauelezeki kwa maneno. Mungu awabariki kwa wema wao.

Shukrani ziwaendee wahadhiri wote walionifunza na wasionifunza wa Chuo Kikuu cha Nairobi. Wao wanifaa kwa hali na mali nilipohitaji msaada wao. Ninawashukuru sana Profesa Kineene wa Mutiso, Profesa John Habwe na Daktari Amiri Swaleh kwa mwongozo walionipa wakati nilipokuwa nikiteua mada yangu ya utafiti. Siwezi nikamsahau Daktari Iribe Mwangi kwa kunielekeza kuhusu mada ya utafiti na usomaji wa yaliyoandikwa kuhusu mada maktabani. Pia ninatambua mchango mkubwa wa Daktari Zaja Omboga aliyetufunza kozi ya Tafsiri Pevu kwa ukakamavu na kujitolea kwingi.

Pia ninawashukuru mke wangu, Gladys Mbula na mtoto wetu Amos Mumo Nilipokaribia kwa kunishauri na kunihimiza nitie bidii zaidi nikiwa na matumaini kuwa siku moja ningekamilisha masomo yangu. Ingawa familia ina changamoto zake alizivumilia wakati nilipokuwa mbali na nyumbani kwa shughuli za utafiti na uandishi wa tasnifu hii. Shukrani zangu pia ziwaendee wazazi wa pande zote mbili. Ninawashukuru marehemu baba, Kilonzo Mulwa na mana, Lydia Kilonzo kwa kunizaa na kunilea. Kama si kwao nisingekuwa katika dunia wala nisingesomea uzamili. Babamkwe, Joseph Masaku na mamamkwe, Lydia Masaku ninawashukuru kwa ushahuri na mahimizo yao wakati wa kusomea uzamili. Pia ninawashukuru ndugu zangu Anna Wathome, Tabitha Jacob, Dorcus Kimeu, James Kilonzo, John Kilonzo na Ruth Kilonzo kwa kuniombea na kufuatilia elimu yangu kwa makini.

Sina budi kuwashukuru wanafunzi niliosomea nao, na ambao walikuwa kama ndugu tulipokuwa tunasoma. Baadhi yao ni Paul Sito, Rose Nyamemba, Everlyn Kanyange, Judithi Kemunto, Mutahi Miricho, Dina Osango, Queen Ndoni, Edward Zani, Nyandiwa Hudson, Lydiah Shaviya, Flora Omosa, Rose Mutunga, Damaris Otwoma, Julita Wanjala, Magdaline Yegon, Gladys Kinyua, Lawrence Orenge miongoni mwa wengine. Ninawashukuru wote kwa kunipenda kwao na kunihimiza nitie bidii masomoni. Nilipobisha walinifungulia. Nilikoenda kombo walinielegeza. Msaada wao kwangu haukuwa na kipimo. Mungu awajalie wote maishani.

Ninawashukuru walimu wa Shule ya Upili ya Yeemulwa kwa kunipa motisha na matumaini nilipokaribia kukata tamaa katika elimu na utafiti wangu. Walimu hao walijumuisha Mwalimu Mkuu Bw. Mutwii, Naibu wa Mwalimu Mkuu Bw. Kitema, mabwana Muthoka, Maliomo, Mutuku na Ngovi; mabibi Muia na Kyalo. Mungu awabariki

Kadhalika, siwezi kamwe nikasahau msaada wa kupigiwa mfano nilioupata kutoka kwa wakutubi wa Chuo Kikuu cha Nairobi, hususan wa Bewa Kuu na wa Bewa la Kikuyu. Hawa walijitolea kufa kupona kuhakikisha nimepata tasnifu, vitabu na makala mengine ya kufanyia utafiti. Shukrani za pekee zimwendee Bwana Peter Matanji mkutubi mkuu wa Bewa la Kikuyu ambaye yeye binafsi alichukua fursa ya kunipeleka katika maabara ya kompyuta na kunielekeza jinsi ningepata matini za kiusomi kutoka katika mtandao. Kadhalika, wakutubi wengine walionisaidia kwa pakubwa katika utafiti wangu ni wale wa kutoka katika Maktaba ya Kitaifa ya Kinyambu. Wakiongozwa na Bwana Mutiso walinisaidia kupata vitabu na makala mengine ya utafiti huu. Kwa jumla wakutubi wote ninawavulia kilemba kwa msaada wenu usio na kipimo.

IKISIRI

Dhamira ya utafiti huu ilikuwa ni kuchanganua ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* ya John Habwe. Mada ilichaguliwa kwa misingi kwamba kazi za kifasihi huibua ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia tofauti. Dira iliyotuongoza kuifanyia utafiti riwaya hii ni nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Vuguvugu la ufeministi huwa na nadharia nyingi kama vile Ufeministi wa Uingereza, Ufeministi wa Ufaransa, Ufeministi wa Marekani, Ufeministi wa kibidhaa, Ufeministi wa kitamaduni miongoni mwa aina nyingine. Tuliuteua Ufeministi wa Kiafrika kama msingi wa kuifanyia riwaya hii utafiti kutokana na ukweli kuwa imeandikwa kwa misingi ya Kiafrika. Nadharia hii huonyesha jinsi asasi tofauti katika jamii zinavyopelekea kuwako kwa udhalimu wa kijinsia. Pia, nadharia hii hupendekeza mbinu za kupigania ukombozi wa kijinsia katika jamii. Malengo ambayo tuliyaangalia ni jinsi ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia unaathiriwa na asasi za kijamii, jinsi umri tofauti tofauti unavyoathiri ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii inayomkandamiza mwanamke na ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika kupigania ukombozi. Mbinu tuliyoitumia katika utafiti huu ni ile ya kukusanya matini za data ya utafiti kutoka vitabuni maktabani. Matokeo ya utafiti wetu ni kuwa, asasi za kijamii kama vile utamaduni, siasa, uchumi, dini na jamii hupelekea kuwako wa udhalimu wa kijinsia. Aidha, tuliona kuwa kuna njia mbalimbali zinazotumiwa ili kuleta ukombozi wa kijinsia.

YALIYOMO

UKURASA

Mada	i
Ungamo.....	ii
Kutabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Ikisiri.....	vi
Yaliyomo.....	vii
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti.....	3
1.3 Sababu za Kuchagua mada.....	3
1.4 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	4
1.5 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	4
1.6 Misingi ya Nadharia.....	12
1.7 Malengo.....	21
1.8 Nadharia Tete.....	21
1.9 Njia za Utafiti	21
1.10 Hitimisho.....	22

SURA YA PILI

UJITAMBUZI NA UTAMBULISHO WA KIJINSIA KWA MUJIBU WA ASASI

TOFAUTI ZA JAMII.....	23
2.0 Utangulizi.....	23
2.1 Utamaduni.....	23
2.1.1 Tohara kama Kipengele cha Utamaduni Kinachotambulisha Jinsia.....	23
2.1.2 Ndoa kama Kipengele cha Utamaduni Kinachotambulisha Jinsia.....	27
2.1.3 Utamaduni Unavyotambulisha Utumishi wa Nyumbani wa Kijinsia.....	33
2.1.4 Haki ya Urithi kama Kipengele cha Utamaduni Kinachotambulisha Jinsia.....	34
2.2 Uchumi na Utambulisho wa Kijinsia.....	37
2.3 Siasa, Uongozi na Jinsia.....	39
2.4 Dini na Utambulisho wa Kijinsia.....	41
2.5 Jamii na Utambulisho wa Kijinsia.....	45
2.6 Asasi ya Elimu na Utambulisho wa Kijinsia.....	52

2.7 Hitimisho.....	53
--------------------	----

SURA YA TATU

UJITAMBUZI NA UTAMBULISHO WA KIJINSIA KIUMRI.....	55
--	-----------

3.0 Utangulizi.....	55
---------------------	----

3.1 Ujitambuzi na Utambulisho wa Watoto.....	55
--	----

3.2 Ujitambuzi na Utambulisho wa Vijana.....	58
--	----

3.3 Ujitambuzi na Utambulisho wa Wazee.....	72
---	----

3.4 Hitimisho.....	79
--------------------	----

SURA YA NNE

UJITAMBUZI NA UTAMBULISHO WA KIJINSIA KATIKA KUPIGANIA

UKOMBOZI.....	81
----------------------	-----------

4.0 Utangulizi.....	81
---------------------	----

4.1 Ukombozi wa Kijinsia Katika Siasa.....	82
--	----

4.2 Ukombozi wa Kijinsia Katika Dini.....	83
---	----

4.3 Ukombozi wa Kijinsia Katika Utamaduni.....	83
--	----

4.4 Ukombozi wa Kijinsia Kiuchumi.....	84
--	----

4.5 Ukombozi Kupitia Ushirikiano wa Kijinsia.....	85
---	----

4.6 Ukombozi wa Kutoa Maamuzi na Ushauri Katika Jamii.....	86
--	----

4.7 Ukombozi Kupitia Upangaji Uzazi.....	88
--	----

4.8 Ukombozi wa Kijinsia Katika Sekta ya Elimu.....	90
---	----

4.9 Ukombozi Kupitia Kutoshiriki Ngono na Jinsia Inayoidhulumu Nyingine.....	91
--	----

5.10 Hitimisho.....	92
---------------------	----

SURA YA TANO

MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	94
--	-----------

5.0 Utangulizi.....	94
---------------------	----

5.1 Mukhtasari wa Sura Zote.....	94
----------------------------------	----

5.2 Mapendekezo.....	96
----------------------	----

Marejeleo.....	97
----------------	----

SURA YA KWANZA

1.1 UTANGULIZI

Utangulizi huu unanua kutoa maelezo kuhusu mada ya utafiti, baadhi ya dhana za mada hiyo, nadharia ya utafiti na pengo tunalolifanyia utafiti. Utafiti huu unachunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya John Habwe: *Maisha Kitendawili*. Dhana za ujitambuzi na utambulisho zina asili moja. Zinatokana na kitenzi tambua. Kitenzi hiki kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* kina maana ya kung'amua, kubainisha au kuelewa. Katika utafiti wetu dhana ujitambuzi itatumiwa kumaanisha jinsi jinsia ya kike na kiume zinavyojibainisha kupitia mazungumzo yazo, vitendo vyazo zenyewe; huku dhana utambulisho ikitumiwa kumaanisha jinsi jinsia hizi zinavyotambulishwa na mwandishi wa kazi ya fasihi husika, wahusika wengine na jamii kwa jumla. Kwa kuwa ujitambuzi wa kijinsia unahusiana na kuonyesha jinsi wahusika wanavyojibainisha kupitia usemi wao au vitendo vyao, tutatua maelezo kuhusu jinsi wahusika tofauti tofauti wanavyojipa vitambulisho mbalimbali riwayani. Katika utambulisho wa kijinsia tutakuwa tukichunguza jinsi wahusika wa jinsia zote mbili wanavyotambulishwa kupitia maelezo ya wahusika wengine, usimulizi wa mwandishi au jamii kwa jumla.

Jinsia kwa upande wake ni dhana inayomaanisha hali ya kuwa mwanamke au mwanamume. Iribemwangi na Mukhwana (2011:134) wanasema kwamba, jinsia ni kigezo cha maumbile ambapo inakuwa ni dhana ya kibiolojia idhihirishayo kama mtu anayezungumziwa alizaliwa mke au mume na hali hii huwa haibadiliki. Wanaungwa mkono na Timammy na Swaleh (2013:153) ambao wanafafanua kuwa, jinsia ni dhana ya maumbile na ya kibiolojia na haiwezi ikabadilishwa (Tafsiri Yetu). Gordon (1999) anaeleza kuwa jinsia hujengwa na jamii. Jinsia humfanya mvulana na msichana, mwanaume na mwanamke na makundi yote ya kijamii kuwa na mienendo na tabia fulani zinazodhibitiwa na jinsia yao.

Dhana ya jinsia huwa ni tofauti kutoka jamii moja hadi nyingine. Jamii huwa inatoa maelekezo kuhusu majukumu, wajibu na kadhalika ambayo ni mwafaka kwa wanaume na wanawake kwa mjibu wa umri tofauti tofauti na jinsi wanavyofaa kuhusiana katika jamii. Jinsia huwa inatambua ni nani aliye na uwezo mwingi kumshinda mwingine katika jamii.

Ni muhimu tueleze hapa kwamba, jinsia ni tofauti na uana. Dhana ya uana ni ya kisosholojia na imezalika kutokana na nadharia ya ufeministi inayodai kuwa kijamii mwanamke na mwanamume wanayo majukumu tofauti. Habwe, Matei na Nyonje (2010:87) wanasema kuwa, yapo majukumu mbalimbali ya kijamii ambayo huhusishwa na jinsia mahususi. Wanasema kwamba, katika jamii za Kiafrika, mwanamume anatarajiwa kuwa shujaa, kuwa kama jogoo, simba n.k., huku mwanamke akitarajiwa kudumisha heshima, kuwa mwadilifu n.k. Uana ni dhana tata kwa misingi kuwa ni dhana ya kijamii na kisosholojia (Iribemwangi na Mukhwana, 2011:134).

Jinsia ni dhana jumuishi ya mahusiano yaliyomo baina ya wanawake na wanaume ambayo yanategemea mwingiliano wa kijamii. Hii ina maana kwamba, dhana hii inajihusisha na mahusiano na maingiliano ya wanawake na wanaume katika jamii. Itakumbukwa kuwa, majukumu ya wanawake na wanaume huwa yanaidhinishwa na jamii kupitia kwa michakato ya maingiliano ya kijamii.

Wafula (1998:116) anaeleza kuwa, swala la jinsia limewashughulisha waandishi kwa muda kufikia sasa. Anaeleza kwamba, swala hili limeanza kuzungumziwa kwa utaratibu kuanzia miaka ya sitini na sabini. Baadhi ya watunzi wanafikiria kwamba, mfumo wa kuumeni wa kuendeleza kizazi cha mtu ndio kadhia muhimu inayosababisha dhuluma zinazofanywa na wanaume dhidi ya wanawake.

Sisi tumepata msukumo wa kufanyia mada yetu utafiti kutokana na kuwapo kwa pengo katika kulichunguza swala la kijinsia kwa ujumla. Watafiti wengi wa hapo awali katika Kiswahili hawakulifanyia utafiti swala hili kwa jumla, bali wamekuwa wakiifanyia jinsia ya kike utafiti na kupuuza kuwa kuna jinsia ya kiume ambayo pia ni muhimu kuifanyia uchunguzi. Ni kutokana na tatizo hili ambapo tumeona kuna umuhimu wa kulichunguza swala la kijinsia kwa ujumla pasipo kujikita katika jinsia maalum. Hii ina maana kwamba, tutajadili ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili (2000)*. Hii ni riwaya ambayo haijafanyiwa utafiti mwingi. Katika utafiti huu tutajikita katika riwaya hii kama kielelezo hata ingawa tutarejelea matini zingine ambazo zina maudhui ya ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii. Katika kuchanganua matini zetu tutaegemea katika nadharia ya ufeministi wa Kiafrika.

1.2 TATIZO LA UTAFITI

Swala la mwanamke limetafitiwa na watafiti wengi. Katika harakati zao za kufanya utafitii wamechunguza maswala mbalimbali yanayokumba jinsia ya kike. Uchunguzi wao umejikita katika nafasi ya mwanamke, utambulisho wa mwanamke, ukombozi wa mwanamke, taswira ya mwanamke miongoni mwa maswala mengine.

Tafiti zao zina pengo, kwani zimeshughulikia jinsia ya kike kwa kiasi kikubwa na kuipuuza ile ya kiume. Ni kutokana na pengo hili ambapo tumepata msukumo wa kuzifanyia jinsia zote mbili utafiti, hususan kutokana na uhusiano na mwingiliano wazo. Tumetumia riwaya ya *Maisha Kitendawili* kwa kuwa migogoro inayopatikana katika riwaya hii ni kielelezo cha yale yanayopatikana katika jamii ya mwandishi. Mada hii ina uzito wa kufanyiwa utafiti kwa kuwa katika kupigania haki na utambulisho wa kijinsia kuna haja ya kuhusishwa kwa jinsia zote mbili. Kuipuuza moja huenda kukadidimiza mikakati ya kuleta mabadiliko mwafaka ya kijinsia katika jamii. Zote zinafaa kushirikishwa katika kupigania haki na usawa wa kijinsia.

1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Tafiti nyingi za hapo awali zimeegemea zaidi kwenye aina za dhuluma wanazokumbana nazo wanawake katika jamii za Kiafrika. Aidha, tafiti hizo zinaonyesha kuwa mwanamke anaendelea kudhulumiwa na mwanamume, lakini nyingi hazionyeshi ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii za Kiafrika. Kwa hivyo, eneo hili linaonekana kupuuzwa na watafiti wengi wa fasihi ya Kiswahili. Watafiti wengi wamejishughulisha na jinsia ya kike na kupuuza kuishughulikia ile ya kiume ambayo inaingiliana kwa njia moja au nyingine na ya kike. Jinsia hizi pia zinahusiana kwa namna moja au nyingine. Kwa hivyo, sababu moja ya kuchagua mada hii ni kushughulikia jinsia zote kwa pamoja pasipo kujikita katika moja.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kwamba, riwaya ya *Maisha Kitendawili* ina wahusika wengi wa kiume na kike wa umri, matabaka, viwango vya elimu tofauti na kadhalika ambao wanajitambuza na kutambulishwa na jamii kwa njia tofauti tofauti. Ni kutokana na msukumo huu ambapo tumeona mada hii ikiwa mwafaka kuifanyia utafiti.

Pia tunafanyia mada hii utafiti kwa sababu tofauti na kazi nyingi za fasihi za hapo awali; ambazo zilionyesha kwamba, baadhi ya wanaume wanajitambulisha kama madhalimu kwa jinsia ya kike, utafiti wetu utakuwa katika nafasi ya kuonyesha kuwa baadhi ya wanaume wa kisasa wameanza kupevuka kimawazo, kubadilika na kupigania ukombozi wa jinsia ya kike katika jamii. Tafiti nyingi za awali hazikuonyesha hili. Hata hivyo, ukombozi kamili huenda ukachukua muda mrefu kuafikiwa, kwani ubabedume umekita mizizi na kukithiri sana katika jamii nyingi za Kiafrika. Kupigana na tatizo hili kunahitaji ukakamavu na ujasiri wa kiwango cha juu kutoka kwa jinsia zote.

1.4 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Katika utafiti huu tutajishughulisha na riwaya ya *Maisha Kitendawili* ya John Habwe. Hata hivyo, ikibidi tutakuwa tunatoa mifano ya kuunga mkono kauli zetu kutoka katika vitabu vingine. Katika utafiti huu tutakuwa tukishughulikia kipengele cha ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kutoka katika riwaya tuliyoitaja hapo juu. Tutakuwa tukitumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika kama msingi wa kuchanganulia kazi hii.

1.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Lugano (1989) katika tasnifu yake “Usawiri wa Wanawake katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi” ameangalia mada ya nafasi ya mwanamke katika riwaya hizi jambo ambalo sisi hatutalifanya. Mada ya utafiti wetu ni ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* wala si nafasi ya mwanamke katika riwaya za Kezilahabi. Maswala ya kutetea haki za jinsia ya kike hayakuwa yakitiliwa mkazo wakati huo kama hivi sasa.

Katola (2006) katika kazi yake “Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili” anasema kuwa, maswala ya kimsingi yaliyopata kushughulikiwa kuhusiana na maudhui ya kijinsia katika fasihi ya Kiswahili ni swala la sura, picha na taswira ya mwanamke kama inavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili.

Utafiti wa Katola unahusu udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Utafiti wake ni tofauti na wetu, kwani sisi tutakuwa tukishughulikia ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* ya John Habwe. Pili, utafiti wake ni tofauti na

wetu tukizingatia misingi ya kazi za fasihi. Yeye alijikita katika tamthilia za Kiswahili, lakini sisi tutakuwa tukichambua na kuchanganua maswala ya kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*.

Utafiti wake ni muhimu kwa mada yetu, hasa katika kuchunguza jinsi jinsia ya kiume inaidhulumu ile ya kike kwa misingi ya utamaduni na ubabedume. Hii ina maana kuwa, utafiti wake utakuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu kwani baadhi ya hoja tutakazozitolea maelezo ni utamaduni na taasubi ya kiume.

Magoma (1997) katika utafiti wake “Mwamko wa Mwanamke, Katika Tamthilia Nne za Peninah Muhando” ambazo ni *Hatia, Heshima Yangu, Nguzo Mama* na *Lina Ubani* amejadili kuhusu utamaduni, itikadi, mila, mapenzi na ndoa, mwanamke na elimu, taasubi ya kiume, kisiasa, mwanamke n.k.

Utafiti wa Magoma ni tofauti na wetu kwa kuwa sisi tutachunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia riwayani, bali si katika tamthilia kama alivyofanya mtafiti huyu.

Utafiti wake ni muhimu kwetu kwa kuwa utamulika mwamko katika kuleta ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia, hasa jinsia ya kike inapopigania ukombozi wake. Pia, utafiti huu una manufaa kwetu, hususan tutakapokuwa tukishughulikia ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika maswala ya kitamaduni, kisiasa, kiuchumi, kimapenzi, kindoa n.k. yanayopelekea kukandamizwa kwa jinsia ya kike katika jamii.

Mirikau (2011) katika “Taswira ya Mwanamke Katika Tamthilia za Wamitila K.W.: *Seserumbe, Pango* na *Wingu la Kupita*”, amezungumzia kuhusu dhuluma zinazomkumba mwanamke katika tamthilia hizi. Dhuluma alizozitolea maelezo ni kama vile kupigwa na wanaume, kuteswa katika ndoa, kuzalishwa watoto wengi, kuchukuliwa na wanaume kama vyombo vya mapenzi, kutishwa, kupashwa tohara, kutusiwa miongoni mwa dhuluma nyingine. Aidha, Mirikau amezungumzia pia kuhusu kutukuzwa kwa jinsia ya kike katika jamii. Anasema kuwa, mwanamke ni mtetezi wa haki, ni mkombozi, ni mwanasiasa, ni mwenye bidii, ni mkarimu, ni jasiri, ni msomi miongoni mwa sifa nyingine za kumwinua mwanamke.

Utafiti wake unahitilafiana na wetu kwa njia kadha. Kwanza, mada yake inatofautiana na yetu. Mada yake inahusu taswira ya mwanamke, huku yetu ikiwa inahusu ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia.

Utafiti wa mtafiti huyu utakuwa na umuhimu kwetu tutakapokuwa tukichunguza jinsi jinsia ya kiume inavyoidhulumu ile ya kike. Pia, utatusaidia katika kuchunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia ya kike katika maswala yanayopelekea kutukuzwa kwake, hasa katika kupigania ukombozi wa kisiasa, kiuchumi, kitamaduni miongoni mwa mambo mengine.

Maingi (2011) amefanya utafiti wenye mada “Upepembezwaji wa Mwanamke kama Udokezi wa Nafasi ya Mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma*”. Katika utenzi huu Maingi ameonyesha jinsi jamii imeshindwa kumshirikisha mwanamke katika kutoa maamuzi ya kijamii. Ameonyesha pia maisha ya Fatuma kabla ya kuolewa kwake, kuposwa, ndoa yake mbinguni na ndoa yake duniani. Kadhalika amehughulikia matumizi ya lugha katika utenzi huu.

Tofauti baina ya utafiti wa Maingi na wetu ni kwamba, yeye ameshughulikia utanzu wa ushairi, ilhali sisi tutashughulikia riwaya.

Utafiti wa Maingi utakuwa na manufaa katika utafiti wetu, hasa tutakapokuwa tukishughulikia ubabedume utatoa mchango mkubwa kwa utafiti huu, hususan tutakapokuwa tukichanganua namna ubabedume unavyomzuia mwanamke kutoa maamuzi katika ndoa.

Kipyegon (2013) katika tasnifu yake “Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke katika tamthilia za *Natala na Kifo Kisimani*” ameonyesha nafasi anayopewa mwanamke katika jamii pamoja na utambulisho wake katika jamii kama vile kuwa mtegemezi, mlezi wa watoto, chombo cha kumfurahisha mwanamume miongoni mwa maswala mengine. Isitoshe, amejadili kuhusu changamoto zinazomkabili mwanamke katika tamthilia hizi mbili.

Utafiti wake ni tofauti na wetu, kwani mtafiti huyu ametafitia kuhusu mada ya nafasi na utambulisho wa mwanamke katika tamthilia mbili tulizotaja hapo juu, ilhali sisi tutakuwa tukishughulikia mada ya ujitambuzi na utambulisho katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* katika

kuchunguza changamoto zinazomkumba mwanamke katika kusaka ukombozi wake. Sisi hatutajishughulisha na changamoto hizi, bali tutatoa maelezo kuhusu ujitambuzi na utambulisho wa jinsia inayojikomboa kutokana na udhalimu wa kijinsia.

Utafiti wake una mchango mkubwa katika utafiti wetu. Ni kutokana na utafiti wa Kipyegon ambapo tutakuwa katika nafasi ya kufahamu jinsia ya kike inavyojitambuza na inavyotambulishwa na jamii za Kiafrika. Pia, tutapata kujua jinsi asasi za kitamaduni, kindoa na kiuchumi zinavyomdhalilisha mwanamke katika jamii.

Onyoni (2012) amefanya utafiti kuhusu “Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za *Natala* na *Mama Ee*”. Katika utafiti wake ameonyesha jinsi ubabedume unavyoitawala na kuidhulumu jinsia ya kike. Ameonyesha vile wanawake wanavyoachiwa majukumu ya nyumbani na wanaume. Kando na haya, ameangalia jinsi vipengele vya fani kama vile wahusika, mandhari na matumizi ya lugha vinavyomsawiri mhusika wa kike katika tamthilia za *Natala* na *Mama Ee*.

Utafiti huo ni tofauti na wetu kwa misingi kuwa Onyoni amejikita katika usawiri wa wahusika wa kike, ilhali utafiti wetu utachunguza uhusiano na mwingiliano katika jinsia zote mbili pasipo kujikita katika jinsia moja maalum kama alivyofanya Onyoni. Kadhalika, mtafiti huyu ametafitia kuhusu baadhi ya vipengele vya fani kama vile mandhari na matumizi ya lugha, swala ambalo hatutalishughulikia katika utafiti wetu.

Utafiti wa Onyoni ni muhimu kwa utafiti wetu. Utachangia katika kuchunguza namna ubabedume unavyopelekea ukandamizaji wa jinsia ya kike katika jamii. Utatuwezesha pia kufahamu jinsi jinsia ya kike inavyokandamizwa na utamaduni wa Kiafrika.

Muhanda (2011) katika kazi yake “Nafasi ya Dini katika Ndoa: Tathmini ya *Utengano* na *Paradiso*”, ameshughulikia nafasi ya dini ya Kikristo na Kiislamu katika riwaya hizi mbili. Kwa kurejelea *Utengano* ameonyesha nafasi ya dini ya Kiislamu katika ndoa na pia akaonyesha nafasi ya dini ya Kikiristo kwa kurejelea riwaya ya *Paradiso*.

Utafiti wa Muhanda ni tofauti na wetu, kwani utafiti wake unahusu nafasi ya dini katika ndoa; ilhali sisi tutachunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia wala hatutajikita katika mada ya mtafiti huyu. Kadhalika, yeye amelipa swala la ndoa kipaumbele katika utafiti wake, jambo ambalo ni tofauti katika utafiti wetu.

Utafiti wake utakuwa na dhima katika utafiti wetu kwa sababu utatupa mwangaza kuhusu maswala ya ndoa na dini katika jamii za Kiafrika. Hata hivyo, dini tutakayoizungumzia kwa kina ni ile ya Kikiristo, kwani ndiyo inayotawala sehemu kubwa katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Tutatoa maelezo kuhusu unafiki na ulaghai unaopatikana katika dini hii riwayani.

Chacha (2013) amefanya utafiti wenye mada ‘Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za *Nguzo Mama na Mama Ee*’. Mtafiti huyu ameshughulikia matatizo ya unyumba, ubaguzi wa kijana wa jinsia ya kike, nafasi ya mila na desturi katika ndoa, nafasi ya dini katika mahusiano ya kinyumba, umoja wa wanawake miongoni mwa maswala mengine. Aidha, katika tamthilia ya *Nguzo Mama*, Chacha amezungumzia kuhusu utabaka na wanawake, majukumu ya mwanamke, nafasi ya mwanamke katika jamii miongoni mwa mambo mengine. Pia, mtafiti huyu ameshughulikia wahusika na mandhari vipengele ambavyo ni vya kifani.

Utafiti wa Chacha unahitilafiana na wetu kwa kuwa sisi tutajikita katika ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia riwayani wala si taswira ya mwanamke kama alivyofanya mtafiti huyu. Isitoshe, mtafiti huyu ameshughulikia tamthilia mbili; lakini sisi tutakuwa tukifanya uchunguzi wetu katika riwaya.

Utafiti huu utatusaidia kufahamu umuhimu wa muungano wa wanawake katika kupigania ukombozi wa jinsia ya kike katika jamii. Utatusaidia pia katika kutoa maelezo kuhusu nafasi ya mila na desturi katika ndoa za Kiafrika. Halikadhalika, utafiti huu utachangia katika kutoa ufafanuzi kuhusu ujitambuzi na utambulisho wa vijana katika jamii.

Karinge (2013) ameshughulikia ‘‘Usawiri wa Ndoa katika Riwaya ya *Unaitwa Nani?*’’. Ameangalia ndoa za wahusika mbalimbali katika riwaya hii. Pia amechunguza changamoto tofauti tofauti zinazokabili asasi ya ndoa kama vile kukosa uaminifu katika ndoa, mila na desturi

zilizopitwa na wakati, hila na udanganyifu n.k. Kadhalika, ameshughulikia mikakati ya kuokoa taasisi ya ndoa.

Utafiti wa Karinge ni tofauti na wetu kwa sababu kadhaa. Kwanza, mada inayoshughulikiwa na utafiti huu ni tofauti na yetu. Mtafiti huyu amejihusisha na usawiri wa ndoa, lakini sisi tutajishughulisha na ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Pili, nadharia inayotumiwa katika utafiti huu ni tofauti na yetu. Yeye ametumia nadharia ya sosholojia katika utafiti wake. Sisi tutatumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika.

Utafiti wa Karinge una manufaa kwa utafiti wetu. Utatusaidia katika kushughulikia swala la ndoa katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* na makala mengine yanayohusiana na ndoa ambayo tutayatumia katika utafiti wetu. Tutakuwa pia katika nafasi ya kushughulikia matatizo yanayokumba ndoa kutokana na utafiti wa mtafiti huyu.

Dorothy (2007) katika “A Critical Analysis of Patriarchy and Masculinity in Kezilahabi’s *Rosa Mistika* na *Kichwa Maji*” ameshughulikia swala la ubabedume. Anasema kuwa, ubabedume umepelekea kudhulumiwa kwa jinsia ya kike. Kadhalika, ameonyesha jinsi utamaduni wa Kiafrika unavyomkandamiza mwanamke. Utafiti wake pia umeshughulikia wajibu wa wavulana katika jamii inayotawaliwa na mifumo ya ubabedume. Kadhalika, ametoa maelezo kuhusu swala la ubakaji katika utafiti wake.

Utafiti wa Dorothy ni tofauti na wetu. Hata hivyo, utatusaidia katika kuchunguza jinsi jinsia ya kiume inavyojitambuzi kwa kutumia kipengee cha ubabedume. Pia, itatufaa kwa kuchunguza namna utamaduni unavyoifanya jinsia ya kike kukosa utambulisho mwafaka.

Maina (2005) katika “Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi Mbili za Shaaban Robert: *Utenzi wa Haki* na *Utenzi wa Adili*” amezungumzia kuhusu maswala ya wanawake na utamaduni, wanawake na elimu, wanawake na uchumi, wanawake na ndoa, wanawake wanaoelekea kujikomboa n.k. Pia, amemwona mwanamke kama pambo la kumfurahisha mwamume. Katika utafiti wake, Maina ametumia nadharia ya ufeministi.

Utafiti wake ni tofauti na wetu lakini utatufaa, kwani tutautumia katika kutambua jinsi jinsia inavyojitambuliza na kutambulishwa katika asasi za kitamaduni, kiuchumi, kisiasa n.k. katika jamii za Kiafrika. Pia, nadharia aliyoitumia katika utafiti wake ambayo ni ya ufeministi itatusaidia katika kutoa ufafanuzi wa nadharia hii katika kazi yetu.

Maobe (2011) katika tasnifu yake ya “Ukombozi wa Mwanamke katika riwaya za Habwe” ambazo ni *Maumbile si Huja* (1995) na *Fumbo la Mwana* (2008) anasema kwamba, mwanamke hukumbana na dhuluma mbalimbali katika maisha yake. Baadhi ya dhuluma alizozitolea maelezo ni k.v. ndoa za lazima, kufanyizwa kazi ngumu, kubaguliwa katika uongozi, kudhulumiwa katika taasisi za kielimu na kadhalika. Ingawa wanakumbana na dhuluma hizi, Maobe anaeleza kuwa mwanamke anaweza kujikomboa kwa kupitia harakati tofauti za ukombozi. Baadhi yazo ni kama vile kuwakabili wanaume wakandamizaji, kuchukua uamuzi, wanawake kuwa na umoja na ushirikiano, kuanzishwa kwa vyama vya ushirika, kujiunga na taasisi za elimu miongoni mwa harakati nyingine.

Utafiti huu unahitilafiana na wetu kwa kiasi fulani. Unachunguza ukombozi wa mwanamke, ilhali wetu utachunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii kwa kurejelea riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Ukombozi wa mwanamke kama sehemu tu ya ukombozi wa kijinsia utajitokeza tu tutakapokuwa tukishughulikia ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia inavyojikomboa; wala hatutauangalia kama mada kuu jinsi Maobe alivyofanya. Tofauti nyingine ni kwamba, yeye ameshughulikia riwaya mbili za John Habwe, ilhali sisi tutashughulikia riwaya moja ya mwandishi huyu.

Utafiti wa Maobe utatusaidia kwa sababu baadhi ya maudhui yanayopatikana katika riwaya za *Maumbile si Huja* na *Fumbo la Maisha* yanapatikana pia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Baadhi ya maudhui hayo na ambayo yatakuwa na mchango mkubwa katika mada yetu ni malezi, biashara, ndoa, ukuzaji wa vipawa, ushirikiano wa wanawake na kadhalika. Kadhalika, utafiti wake utakuwa na umuhimu kwetu kwa sababu utatufaa kuitolea nadharia ya ufeministi maelezo zaidi.

Obure (2012) katika utafiti wake “Dhuluma Dhidi ya Vijana wa Kike katika Riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini*” amebainisha kwamba, vijana wa kike wamedhulumiwa na kudunishwa katika jamii. Anaonyesha kuwa, wanapigwa, wanabakwa na kupachikwa mimba, wanatolewa vitisho, wananyanyaswa kimapenzi na kadhalika. Vijana hawa pia hukumbana na tohara, ukosefu wa elimu miongoni mwa dhuluma nyingine katika jamii.

Utafiti wake ni tofauti na wetu, lakini utakuwa na manufaa kwa utafiti wetu, kwani utatusaidia katika kuelewa jinsi vijana wa kike wanavyojitambulisha katika kamii kwa kuegemea riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Pia utakuwa na dhima ya kutuwezesha kutambua baadhi ya dhuluma anazokumbana nazo mwanamke katika jamii, hasa anapojaribu kupigania ukombozi wake katika jamii isiyomjali.

Kinyua (2011) katika tasnifu yake ya “Riwaya ya *Unaitwa Nani?* Inavyoshughulikia Swala la Ukombozi wa Mwanamke” ametafitia jinsi ubabedume unavyomnyima mwanamke utambulisho wake kama mwanajamii kamili. Anaeleza kuwa, mfumo wa ubabedume humnyima mwanamke nafasi ya elimu katika jamii. Mtafiti huyu anafafanua jinsi vikwazo vya kitamaduni vinavyopelekea mwanamke kunyanyaswa na kudhulumiwa katika jamii. Pia ameonyesha namna mwanamke anavyoweza kupigania ukombozi wake katika jamii dhalimu. Isitoshe, ameangazia kuhusu uhusiano wa jamii ya kike na ya kiume.

Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa kuwa, anafanya uchunguzi na uchanganuzi wa ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* ya Wamitila K.W., ilhali riwaya tunayoifanyia utafiti ni ya *Maisha Kitendawili* ya John Habwe.

Kazi yake Kinyua itakuwa na manufaa makubwa kwa utafiti wetu. Hii ni kwa sababu itatuwezesha kufahamu ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia inayotaka kujikomboa, hasa ile ya kike ambayo inataka kujikomboa kutoka kwa utamaduni na ubabedume unaomdunisha mwanamke katika jamii. Pia, itatusaidia katika kueleza baadhi ya majumu yanayopewa jinsia ya kike na jamii za Kiafrika. Kadhalika, utafiti huu utatujalia katika kuonyesha uhusiano wa kijinsia katika jamii za Kiafrika.

Yego (2013) katika utafiti wake “Nafasi ya Mwanamke katika Nyimbo za Taarab”, ameeleza jinsi utamaduni na ubabedume unavyochangia katika kudhalilishwa kwa jinsia ya kike. Ili kuepuka ukandamizaji huu mwanamke hana budi kupigania haki zake katika jamii anamoishi. Yego anafafanua pia jinsi ndoa inavyopelekea kudhulumiwa kwa wanawake katika jamii za Kiafrika. Ndoa inapelekea kudhulumiwa kwa mwanamke kimwili na kimawazo. Mwanamke huwa hana usemi katika maswala ya ndoa kama vile uchumba na mapenzi. Kadhalika, katika utafiti wake; Yego amezungumzia kuhusu sababu zinazopelekea kuwako kwa usaliti katika jamii. Anasema kuwa, tabaka la juu lililo na mali ya kutosha huitumia kuwadanganya wasichana na mabibi za watu na kushiriki ngono nao. Ili kuepuka dhuluma zinazomkumba mwanamke katika jamii inapasa kusimama kidete na kupigania haki zake za kiuchumi, kijamii na kadhalika.

Utafiti wa Yego ni tofauti na wetu, lakini utachangia pakubwa katika kazi yetu. Aidha, nadharia yake ya ufeministi itatufaa katika utafiti wetu. Tutapata maelezo ya ufeministi wa Kiafrika kutoka katika kazi ya mtafiti huyu. Isitoshe, tutafahamu baadhi ya dhuluma zinazoikumba jinsia ya kike inapoingiliana na ile ya kiume, hususan inaposaka utambulisho mwafaka katika jamii. Utafiti huu pia utatusaidia katika kumaizi jinsi utamaduni, ndoa na kadhalika zinavyochangia katika kuhakikisha kuwa, mwanamke hapati utambulisho wa kupigiwa mfano katika jamii yake. Kadhalika, kwa kuwa utafiti wake ni wa hivi majuzi, utatusaidia kuangalia maswala yanayokumba ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii za Kiafrika za hivi sasa.

1.6 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti wetu utaongozwa na nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ambayo iliasisiwa na Steady (1981). Katika tovuti ya [www.edu/8281460/celebrating African Feminism](http://www.edu/8281460/celebrating_African_Feminism) Roda Asikia akimrejelea Filomena Steady anaeleza ufeministi wa Kiafrika kama vuguvugu linalojumuisha vipengele vya udhalimu wa kirangi, kijinsia, kitabaka na kitamaduni ambavyo vinafaa kubadilishwa ili kuzalisha mtazamo ambao utawaona wanawake kama binadamu wala si vyombo vya kuwafurahisha wanaume. Kadhalika, Asikia katika tovuti hiyo hiyo akimnukuu Mac Fadden anaeleza ufeministi huu kama muundo wa kisiasa ambao unatokana na hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika utafiti wetu tutachukulia ufeministi wa Kiafrika kama ufeministi unaojijhusisha na utambuzi wa vikwazo vinavyoinyima jinsia haki, usawa na ukombozi na namna ya

kukabiliana na vikwazo hivyo ili kuuondoa udhalimu wa kijinsia unaopatikana miongoni mwa Waafrika wawe barani Afrika au mahali kwingineko ulimwenguni.

Filomena Steady (1981) anasema kuwa, nadharia hii inachunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazochangia unyanyasaji wa wanawake wa Kiafrika. Anasema kuwa, mwanamke wa Kiafrika ni mtetezi wa haki na usawa kuliko mwanamke wa Kimagharibi. Mwasisi huyu anauleza ufeministi wa Kiafrika kama ufeministi unaotilia mkazo swala la wanawake kuwa na uwezo pamoja na ushirikiano. Anaeleza kuwa fasihi ya ufeministi huu inajihusisha na ukombozi wa watu wote wa Afrika. Anafafanua kuwa ufeministi huu unajihusisha na tamaduni za Kiafrika pasipo kuziondolea mbali. Tamaduni hizi zinaweza kuchukuliwa tofauti tofauti na wanawake wa matabaka tofauti ya kijamii.

Swala ambalo limekuwa likitiliwa maanani na wananadharia kama vile Steady limekuwa ni kuhusishwa kwa wanaume katika ukombozi wa jinsia ya kike. Mwananadharia huyu anasisitiza kuwa ili ufeministi wa Kiafrika ufanikiwe kuna haja ya kuhusisha jinsia zote mbili. Swala hili ni tofauti katika ufeministi wa Kimagharibi, kwani wanawake hawataki kuwahusisha wanaume katika ukombozi wao.

Steady (1981:30-37) anafafanua kuwa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ina sifa zifuatayo:

- (i) Ni nadharia inayotumia fasihi kama jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo.
- (ii) Naharia hii inanuia kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu. Baadhi ya amali ni za kike na za kijadi na ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa.
- (iii) Mtazamo huu vile vile unajaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa, wanawake ambao hawawategemei wanaume ili wajitambulishie.
- (iii) Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia na umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.
- (iv) Nadharia hii hunuia kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona, na uhusiano wao na watu wengine.

(v) Lengo muhimu la nadharia hii ni kuvumbua na kuziweka wazi kazi za kifasihi zilizotungwa na wanawake na ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.

Mtandao wa *Africa Guardian Africa Network* unaeleza kwamba, ufeministi wa Kiafrika ulianza mapema katika karne ya ishirini. Ulianzishwa na wanawake kama vile Adelaide Casely-Hayord wa Sierra Leone. Kutokana na kupigania haki za wanawake mwanaharakati huyu aliishia kuitwa “African Victorian Feminist”. Alichangia pakubwa katika kuhakikisha kuwa malengo ya ufeministi yameafikiwa.

Mwanamke mwingine aliyechangia katika kuendeleza ufeministi wa Kiafrika ni Charlotta Maxeke. Mnamo mwaka wa 1918 mwanamke huyu alianzisha *Bantu Women's League* kule Afrika Kusini. Mwingine ambaye alichangia katika nadharia hii ni Huda Sharaawi ambaye mnamo mwaka wa 1923 alianzisha *The Egyptian Feminist Union*.

Mtandao huu unafafanua kwamba, ufeministi wa Kiafrika kama vuguvugu la mabadiliko pia lina chanzo chake kwa wapiganiaji uhuru hasa katika mataifa ya Algeria, Msumbiji, Guinea, Angola na Kenya; ambapo wanawake walishirikiana na wanaume kupigania ukombozi wa nchi zao pamoja na haki za wanawake. Wanaharakati wanawake wa Kiafrika waliotokea wakati huu ni kama vile waliojiunga na Mau Mau waliojumuisha Wambui Otieno, wapiganiaji wa uhuru kama vile Lilian Ngoyi, Albertina Sisulu, Margaret Ekpo na Fummilayo Anikulapo-Kuti miongoni mwa wengine waliopigana dhidi ya ukoloni na ubabedume katika jamii za Kiafrika.

Wanawake wa Afrika Magharibi kama vile wa Ghana wana historia ya kina katika maswala ya kisiasa. Kuna mwanamke wa jamii ya Ashanti aliyeitwa Yaa Asantewa ambaye aliongoza katika kupinga utawala wa kikoloni wa Waingereza wa mwaka wa 1901. Sawa na wanawake wengi wa Afrika Magharibi wanawake wa Kiashanti wamekuwa ni wakulima, wafanyabiashara na washiriki shupavu katika siasa.

Tovuti hiyo inaendelea kueleza kuwa, ufeministi wa Kiafrika ulipata nguvu zaidi kwa kipindi cha mwongo mmoja kuanzia mwaka wa 1975 hadi 1985. Katika kipindi hiki kuna mabadiliko makubwa yaliyotokea. Kulianzishwa ukereketwa wa kifeministi na udhamini wa kielimu

ulioenea kote Barani Afrika na ughaibuni. Kutoka wakati huo kumekuwa na vuguvugu la ufeministi wa Kiafrika ambalo limepanua mawanda yake kisera, kisheria, kielimu na maswala ya kiutamaduni yanayomkandamiza mwanamke. Vuguvugu hili linajihusisha na upunguzaji wa umaskini, uzuiaji wa dhuluma za kijinsia, haki za uzazi pamoja na za namna ya kuishi, uzuiaji vyombo vya habari vinavyoeneza utamaduni unaoendeleza ubabedume n.k.

Pinkie Megwe katika *An African Journal of Philosophy (Theorizing African Feminism)* kutoka kwa tovuti ya www.quest-journal.net/voixx/Quest_xx_megwe.pdf anasema kuwa, swala la waandishi wanawake wa Kiafrika lilipoanza miaka ya 1970 lilikuwa linanua kuondoa usawiri hasi wa wanawake katika kazi za fasihi uliokuwako wakati huo. Kazi zilizoandikwa za kijinsia zilifaa zisawiri hali ya mukhtadha wa Kiafrika, bali si kufuata mukhtadha wa kijinsia wa Kimagharibi ambao una tofauti kadha ukilinganishwa na wa Kiafrika. Fasihi ya ufeministi wa Kiafrika inajishughulisha na upatikanaji wa uhuru wa watu wote wa barani Afrika.

Katika utafiti wetu tutaongozwa na mhimili ifuatayo ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika: Tutaongozwa na mhimili wa utamaduni wa Kiafrika. Utamaduni huu unachangia pakubwa katika ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia. Kuna jinsi utamaduni unavyoipa jinsia ujitambuzi na utambulisho kwa misingi ya jamii husika.

Mhimili mwingine utakaokuwa na umuhimu katika utafiti wetu ni dini. Mhimili huu utatuongoza katika kufafanua ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia miongoni mwa Waafrika. Mara kwa mara dini imekuwa ikiitukuza jinsia ya kiume huku ikiidhalilisha ile ya kike.

Isitoshe, tutatumia uchumi kama mhimili wa kuchanganulia kazi yetu. Hapa tutakuwa tukitumia mhimili huu kujadili mchango wa kijinsia kuendeleza au kukwamiza uchumi katika jamii. Jinsia ya kiume mara kwa mara imekuwa ikijitambuza kama yenye uwezo wa kuzalisha mali; huku ile ya kike ikiachwa nyuma kwa kiwango kikubwa katika harakati za kuimarisha uchumi. Hata ikijiingiza katika harakati hizi za uzalishaji wa mali huwa haielekei kufanikiwa sana.

Pia, mhimili wa kisiasa utatumika katika utafiti wetu. Hapa tutajadili mchango wa kijinsia katika kuendeleza siasa. Jinsia ya kiume inaelekea kujitambuza na kutambulishwa kama

inayojishughulisha na siasa zaidi kuliko ile ya kike. Hata ya kike inapoingilia swala la siasa inaelekea kutokuwa na mchango mkubwa katika kushiriki katika mijadala mikali ya kisiasa.

Mhimili mwingine unaopatikana katika nadharia hii na tutakaoutumia katika utafiti wetu ni ule wa jamii. Jamii huwa inaipa jinsia utambulisho tofauti tofauti kwa mintarafu ya utamaduni wake. Kuna namna jamii inavyotarajia jinsia ya kiume ijitambuze, vivyo hivyo, kwa jinsia ya kike. Mwanajamii anapojitambuza tofauti na matarajio ya utambulisho wa jamii hii anakuwa kama mtu anayevunja mwiko au miiko ya jamii husika.

Ukombozi wa kijinsia ni mhimili mwingine ambao utatuongoza katika utafiti wetu. Tutautumia mhimili huu kujadili jinsi jamii inavyopigania kuwako kwa ukombozi wa kijinsia; huku ikitiliwa maanani kwamba jinsia ya kike imekuwa ikikandamizwa na ile ya kiume kwa muda mrefu barani Afrika. Hapa tutaeleza jinsi jinsia inavyopigana na maswala yanayoikandamiza kama vile utamaduni, dini, siasa na kadhalika.

Kuna wahakiki na watafiti wengi ambao wametoa mchango wao kuhusiana na nadharia ya ufeministi wa Kiafrika. Kazi ya Mfaransa, Beauvoir (1949:114) ya *The Second Sex* imekuwa na mchango katika kuleta ukomozi wa kijinsia. Kazi hii ndiyo msingi na uhakiki wa kifeministi. Mwandishi huyu alichukua mkabala wa kiharakati kwa kushambulia na kukosoa baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha au kumdunisha mwanamke ambazo ni ndoa, dini na utamaduni. Dini inatilia mkazo au nguvu itikadi ya kiume inayopatikana katika jamii nyingi. Asasi hii inaishia kuzipa nguvu mpya tamaduni dhalilishi dhidi ya mwanamke kwa kuziwekea mihimili ya tamko ya kidini.

Dini humkandamiza mwanamke kwa kumfundisha kunyenyekea (Wafula na Njogu 2007:90). Dini ni asasi inayomwangalia mwanamke kama kitu hasi na cha kando, huku ikimchukulia mwanamume kama binadamu kielelezo. Utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha mwanamke kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Baada ya kuikubali hali hiyo mwanamke anaishia kuwa kama chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni huo hasi.

Wamitila (2002:157) anasema kwamba, ndoa ni mojawapo wa asasi ya kitamaduni inayoendeleza ukandamizwaji wa wanawake. Asasi yenyewe imejengwa kwenye imani ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume na kuishia kumwona mwanamke kama chombo tu. Ndoa imejengwa kwenye misingi na imani ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume akilinganishwa na mwanamke (Wafula na Njogu 2007:91). Germane Greer (1971) anawahimiza wanawake kususia ndoa kwa kuwa hali ya kuolewa inafanya kumilikiwa na kukosa ubinafsi na uhuru wao.

Naye Millet (1977) katika *Sexual Politics* anawashambulia vikali baadhi ya waandishi maarufu wa kiume kutokana na jinsi wanavyowasawiri wahusika wao wa kike. Waandishi waliochunguzwa na mwandishi huyu ni Lawrence, Miller, Norman na Genet.

Millet anabainisha kuwa miundo ya kijamii pamoja na asasi zake vinashirikiana kumkandamiza mwanamke. Hii ni sifa inayojitokeza katika waandishi tuliowataja hapo juu. Pili, mwandishi huyu anaishambulia mikabala ya Saikolojia-Changanuzi inayohusishwa na Sigmund Freud. Freud alisema mtoto wa kike anaanza kujichukia mara tu anapotambua kuwa hana kiungo cha kiume. Hali hii inasababisha 'Wivu wa Zubu' (Wamitila 2002:158).

Millet anadai kuwa wivu uliopo ni uwezo alio nao mwanamume kutokana na muundo wa kijamii. Mwanamke anakuwa na wivu wa kinachoashiriwa na hilo zubu wala sio zubu kama kiungo cha mwili. Wahakiki wa hivi karibuni wameishia kutofautiana na Millet kuhusu mambo mengi kama anavyosema Wamitila (2002:158). Mambo haya ni kuhusiana na mawazo ya Freud. Baadhi ya wahakiki hawa wameishia kusema kuwa, mhakiki huyu alifasiri mawazo haya vibaya. Wanaufeministi walioathiriwa na mawazo ya wanaumuundoleo kama Jacques Lacan, wameishia kuyarudia mawazo haya ya Freud na kuyatumia kwa mikabala mingine tofauti na Millet.

Naye Nguta (2011:19) akimrejelea Millet anasema kuwa, ufeministi wa Kiafrika umetokana na utamaduni katika jamii inayojikita katika kilimo na ushirikiano wa kijamii. Ni ufeministi ambao umejengeka katika misingi thabiti ya kumhusisha mwanamke katika shughuli tofauti za kijamii bila kuangalia asasi zinazotawaliwa na wanaume. Ufeministi huu unasisita usawa katika shughuli za umma (jamii) na utoaji uamuzi kwa wanawake na wanaume.

Aidha, Nguta akimnukuu Steady (1981) anaeleza kuwa, ufeministi wa Kiafrika unaangalia misingi inayoangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanayotegemeana na kukamilishana. Anasema kwamba, ufeministi wa Kiafrika unaweka pamoja maswala ya ubaguzi, uana, tabaka na mielekeo tofauti ya kiutamaduni ili kuleta ufeministi unaomwangukia mwanamke kama kiumbe, lakini sio jinsia. Ufeministi huu unaangalia maswala ya kitamaduni yanayomlemaza mwanamke.

Katola (2006) akimrejelea Christopher Miller katika *Theories of Africans* anauleza ufeministi wa Kiafrika, hasa ule unaohusishwa na fasihi. Anafafanua kwamba, ufeministi huu unatofautiana na ufeministi wa Kimagharibi kwa sababu unajikita katika uhalisi wa mambo ya Kiafrika. Kimsingi unajishughulisha na uhalisi wa maisha ya mwanamke katika mikhtadha ya kijamii, kitamaduni na kiuchumi. Ufeministi huu una haja pia ya kuonyesha jinsi mikhtadha hii inavyochangia kumnyanyasa, kumdunisha na kumdhalilisha mwanamke wa Kiafrika.

Yego (2013:13-14) anasema kuwa, kila binadamu anapozaliwa ana haki za kiasili za kuwa na uhuru na usawa na hali ndiyo iliyochangia harakati za ukombozi. Mchango wa watu wa Magharibi katika ukuaji wa ufeministi huu ulitokana na Waafrika walioishi Ulaya kujifunza kupiga vita udhalimu na ubaguzi wa rangi ulioendelezwa na Wazungu dhidi yao. Wanawake Waafrika walio ng'ambo wanaendelea kupigania haki zao dhidi ya ubaguzi wa rangi, kitabaka na dhuluma za kimapenzi ambazo huendelezwa na wanaume ili kuwanyamazisha wanawake. Ufeministi wa Magharibi ulipigania haki za raia na ufeministi wa Kiafrika ulipigania haki za kibinadamu na kijinsia.

Yego anaendelea kusema kuwa, ufeministi wa Kiafrika uliendelezwa na mataifa ya Kimagharibi kupitia kwa wanawake wa rangi nyeusi na wenye asili ya Kiafrika. Mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika amesawiriwa kama kiumbe duni na ametengewa nafasi inayoonekana kuwa ni ya chini, lakini iliyo na majukumu mengi. Wanawake Waafrika wa matabaka yote wanakumbwa na changamoto za kifedha, kikazi, kifamilia na za kuzihudumia jamii zao. Kuna uhusiano mkubwa baina ya umaskini, kutosoma, hali duni ya wanawake na utamaduni wa Kiafrika wenye ukatili kama vile ndoa za mapema na za kulazimishwa na ukeketaji wa wanawake.

Mirikau (2011:15) anafafanua kwamba, ufeministi wa Kiafrika na ufeministi wa Kimagharibi unafanana ukimzungumzia mwanamke kijumla, lakini tofauti zipo ukiangalia kindani. Kwanza,

fikra za Mwafrika na uchukulio kuhusu maswala haya hutofautiana kwa vile kinachochukuliwa kama shida Uzunguni kinaweza kuonekana na Mwafrika kama furaha yake. Hali hii hutokea kwa sababu ya tofauti za kielimu, kisiasa, kidini na kiuchumi. Aidha, Mwafrika amekulia katika mazingira ya kijamii yenye desturi na tamaduni tofauti na zile za Mzungu. Pili, uthibitishaji wa mifano kuhusu shida zinazomkumba mwanamke, taswira yake iwe chanya au hasi, na ukombozi wake huenda ukawa tofauti.

Kwa ufupi, wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Vitengo vya utamaduni huu ni kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi, tohara na ukeketaji wa wanawake, kimya cha kulazimishwa, desturi na mila zinazomdhalilisha kama vile kuonewa kwa mwanamke asiyezaa n.k.

Kwa kuwa wanawake ni watu muhimu katika maendeleo ya jamii zao na maendeleo ya baadaye ya Afrika ni muhimu kuelewa ubaguzi na dhuluma mbalimbali wanazokumbana nazo katika maisha yao. Wanawake hawa wa Afrika huwa wanazungumzia hali zao, matakwa yao, haki za na wamechukua nafasi muhimu katika kupigania haki za kijinsia ili kuwe na usawa katika jamii. Hali na matakwa ya wanawake hawa yamekuwa yakishughulikiwa katika kiwango cha taasisi za kitaifa na za kimataifa kutokana na kujitolea kwao kijasiri kupigania maswala ya kijinsia. Sehemu ambazo zimekuwa zikishughulikiwa ziliongezeka zaidi kuanzia mwaka wa 1960. Sehemu hizo zinahusisha maswala ya kisiasa, kielimu na mafunzo, kupata uwezo wa kiuchumi ambapo kuna hali ya kupata ajira bora. Pia, kiuchumi hali ya kupata mikopo ya kuanzisha biashara au ya kununua vipande vya ardhi ama mali limekuwa swala muhimu. Aidha, wamekuwa katika msitari wa mbele katika kupigania kupata huduma bora za kiafya; hususan afya ya uzazi. Aidha, wanajihusisha na siasa ambapo wao wanapiga kura na kuchagua au kuchaguliwa kama viongozi serikalini.

Kimsingi hii ni nadharia ambayo imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Tovuti ya www.mavalapeter.blogspot.com/2014/12/a-define-african-feminism-b-discuss-way unaonyesha baadhi ya tofauti za ufeministi wa Kimagharibi na wa Kiafrika. Ufeministi wa Magharibi unachukulia zaidi kuwa wanawake kote duniani ni tabaka la vyombo vya kuwafurahisha wanaume kote duniani tofauti na wanawake hawa wanataka mzigo wa kuzaa na kuwalea watoto huwahusishe wanaume kikamilifu tofauti na wa Kiafrika ambao hautilii maanani swala hili. Wanawake hawa wa wanaona kuwa kupitia njia ya kugawana majukumu ya kuwalea watoto watakuwa wamepunguza udhalimu wanaoupata kutoka kwa wanaume. Hapa watakuwa wamepunguza ile hali ya kuonekana kama vyombo vya kutosheleza ashiki za wanaume. Kwa upande ule mwingine ufeministi wa Kiafrika unajishughulisha zaidi na jinsi ya kupiga umaskini vita na kukubali nafasi zao katika jamii kama wanawake na mama wa watoto. Aidha, ufeministi wa Magharibi unawaona wanawake Waafrika kama watu walionyamazishwa kwa muda mrefu na ubabedume ambapo wanaume wana uwezo wa kuwaoa wake wengi, kuwakeketa wanawake, kuwapiga wanawake na wanawake kutokuwa katika nafasi ya kurithi mali au kuwa na uwezo katika jamii zao jinsi wanaume walivyo nao. Kwa upande wao wanawake Waafrika hawataki kuutupilia mbali kabisa utamaduni huu wenye ubabedume unaomwona mwanamke kama mtu duni katika jamii, bali wanataka kuwe na usawa wa kijinsia tu.

Nadharia hii ya ufeministi wa Kiafrika ni mwafaka kwa utafiti wetu na ndiyo tutakayoitumia kama msingi wa kuchananulia na kupambanulia maswala mbalimbali tutakayoyajadili kuhusu ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* na kazi nyingine tutakazozitumia kuungia mada yetu mkono. Nadharia hii ni mwafaka zaidi kwa mada yetu, kwani riwaya tutakayoirejelea katika utafiti wetu wa kijinsia imeandikwa kwa mingi ya Kiafrika na ina mengi ya kueleza kuhusu jinsia kwa mitazamo ya Kiafrika.

Nadhari ya ufeministi wa Kiafrika ilikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu zifuatazo:

- (i) Ilitusaidia katika kujadili jinsi utamaduni unavyopelekea kuwako kwa dhuluma za kijinsia.
- (ii) Ilikuwa mwafaka pia katika kuonyesha nafasi ya jinsia katika siasa.
- (iii) Ilitufaa katika kuchunguza nafasi ya jinsia katika dini.
- (iv) Ilikuwa na dhima ya kuchunguza jinsi jamii inavyolichukulia swala la kijinsia.
- (v) Ilitupa mwelekeo kuhusu mchango wa jinsia katika kuendeleza harakati za kiuchumi.

- (vi) Ilitupa mwongozo kuhusu harakati zinazochukuliwa na wanawake ili kupambana na ubabedume katika jamii.
- (vii) Ilikuwa na manufaa katika kuonyesha jinsi jinsia ya kike inavyopigania ukombozi wake n.k.

1.7 MALENGO

Utafiti huu una malengo yafuatayo:

- (i) Kuchunguza jinsi ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia unavyoathiriwa na asasi za kijamii kama vile utamaduni, uchumi, siasa, jamii na dini.
- (ii) Kubainisha jinsi umri tofauti tofauti unavyoathiri ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii inayomkandamiza mwanamke.
- (iii) Kushughulikia ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika kupigania ukombozi katika jamii inayomkandamiza mwanamke.

1.8 NADHARIA TETE

- (i) Ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia unatofautiana baina ya jinsia ya kike na ile ya kiume kwa sababu za kitamaduni, kiuchumi, kisiasa, kidini na kijamii.
- (ii) Umri tofauti tofauti wa kijinsia huathiri ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii.
- (iii) Jinsia ya kike imefanikiwa kwa kiasi fulani katika kujitambuzi na kutambulishwa kama inavyopigania ukombozi wake katika jamii isiyomjali mwanamke.

1.9 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu ulikuwa ni wa kupata matini kutoka kwenye vitabu katika maktaba. Tulianza kwa kuisoma riwaya ya *Maisha Kitendawili*, kisha tukachambua na kuchanganua maswala ya ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya hii. Pili, tulidurusu vitabu, tasnifu na makala mbalimbali yaliyohusiana na mada yetu. Tulifanya hivi ili kujiandaa kinadharia na vile vile kuyaelewa maswala ya kijinsia kwa undani. Tatu, tulifanya upekuzi wa kuhusiana na jinsia katika tovuti mbalimbali katika mtandao wa intaneti.

1.10 HITIMISHO

Mada yetu ya utafiti imehusu “ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* (2000) ya John Habwe.” Mwandishi wa riwaya hii ni Mwafrika na ni wa jinsia ya kiume, na mengi aliyoandika ni yale yanayozikumba jamii nyingi za Kiafrika.

Swala la jinsia ya kike limetafitiwa na watafiti wengi. Hata hivyo, swala la jinsia zote mbili halikushughulikiwa na watafiti wa awali ndipo utafiti wetu ukajikita katika swala hilo lililo na pengo la kuzibwa.

Kuhusu upeo na mipaka ya utafiti wetu ni kuwa, ulijikita katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Hata hivyo, baadhi ya nyakati tulitumia kazi nyingine kuungia kauli zetu mkono.

Yaliyoandikwa kuhusu mada hii ni kuwa, watafiti wengi walioifanyia jinsia ya kike utafiti. Wengi wao tuliona kwamba wamemwangalia mwanamke kwa misingi ya dhuluma anazokumbana nazo, taswira yake, mwamko wake n.k. Tulizilinganisha na kuzitofautisha na mada yetu ya utafiti. Tulioonyesha jinsi tafiti hizi zilikavyotufaidi katika utafiti wetu.

Tulieleza kuwa utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya ufeministi kwa Kiafrika. Hii ni kwa sababu kazi tuliyoifanyia uchunguzi imeandikwa kwa misingi ya Kiafrika. Baadhi ya vipengele vya kimsingi vya nadharia hii vilivyotumika katika utafiti wetu ni utamaduni, siasa, dini miongoni mwa vingine.

Tuliona kwamba baadhi ya malengo ya utafiti huu ni kuchunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kwa kuegemea asasi tofauti tofauti. Pia kubainisha jinsi umri tofauti unavyoathiri ujitambuzi na utambulisho huu. Isitoshe, kuchunguza jinsi jinsia ya kike inavyojitambuza na kutambulishwa katika kupigania ukombozi wake.

Pia, tulizungumzia nadharia tete ya utafiti zilitokana na malengo tuliyoyataja hapo juu. Utafiti wetu ulikuwa ni wa kusoma matini tofauti kutoka katika maandishi mbalimbali maktabani yaliyotufanya tupate data ya kufanyia uchunguzi katika utafiti wetu.

SURA YA PILI

UJITAMBUZI NA UTAMBULISHO WA KIJINSIA KATIKA ASASI MBALIMBALI ZA KIJAMII

2.0 Utangulizi

Katika sura hii tutachunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kwa kuegemea asasi tofauti tofauti za kijamii kama vile utamaduni, dini, uchumi miongoni mwa nyingine. Hizi ni asasi ambazo zimezungumziwa na mwandishi katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Tutarejelea maandishi mengine pia katika kufafanua hoja zetu.

2.1 Utamaduni:

Katika sehemu hii tutajadili jinsi utamaduni unavyochangia katika ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii.

2.1.1 Tohara kama Kipengele cha Utamaduni Kinachotambulisha Jinsia

Tohara huwapa wanawake na wanaume utambulisho maalum kwa mujibu wa utamaduni wa Kiafrika. Wengi wa vijana hutahiriwa baada ya kubaleghe. Gehman (2005:64, 65) anasema kwamba, kubaleghe huwa ni mpito baina ya utoto na utu uzima. Anasema kwamba, kila jamii huwa na miviga tofauti ya tohara katika mpito wao kutoka utotoni hadi utu uzima. Ni kupitia tohara ambapo wanawake kwa wanaume hupata utambulisho katika jamii zao. Tohara huwa mara nyingi ni sherehe inayoshirikisha wanajamii wote katika jamii za Kiafrika. Wote wanashiriki katika sherehe hii kwa njia moja au nyingine.

Walibora katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* jinsi tohara inavyosherehekewa katika jamii ya Wabukusu. Anaeleza jinsi kunavyochinjwa wanyama katika sherehe hii. Kupitia kwa kumbukumbu za Almasi, Walibora anasema:

Alikumbukia Mzee Namiti aliyestahabu kumchinja fahali mkubwa ili kujishaua katika sherehe za tohara ya mwanawe na kushindwa kumlipia karo bintiye anayemalizia kidato cha nne (uk63).

Kutokana na usimulizi huu tunaona kuwa tohara inatambuliwa kuwa muhimu zaidi kuliko maswala mengine ya kijamii kama vile elimu. Miviga hii ya kijamii tunaona akipewa nafasi ya kwanza kuliko vitu vingine vingi katika jamii nyingi za asili ya Kiafrika.

Kasu katika *Maisha Kitendawili* anashuhudia kisa ambapo kuna wanaume wawili wanaotayarishwa kwa tohara. Wanajamii hapa wanashiriki katika sherehe hii kwa kuimba, kucheza ngoma miongoni mwa maswala mengine. Katika hali hii jamii inatambua kuwa tohara ni hatua muhimu sana katika maisha ya binadamu.

Wale wanajamii ambao hawatahiri watoto wao kwa kukata sehemu ya mwili, huwa wanang'olewa meno ya mbele. Wajaluo na Wamasai - ni baadhi ya jumuiya ambazo zinaendeleza utamaduni huu. Hata hivyo, Wamasai tofauti na Wajaluo huwa wanatahiriwa pia kwa kukatwa sehemu zao za mwili.

Yeyote asiyetahiriwa huchukuliwa kama mtoto katika jamii yake hata kama ni mzee kiumri. Huwa pia anatengwa na watu wa umri au rika lake. Huwa hawataki kujitambulisha naye kutokana na kutopitia hatua hiyo muhimu ya maisha. Gehman anaeleza kuwa, Waafrika wengi hali hii huwa na miviga ya tohara ambapo matambiko mengi huwa yanahusishwa na mpito huu wa maisha.

Katika jamii nyingi za Kiafrika kabla ya ndoa ni lazima mtu apitie katika tohara. Kabla ya tohara mtu huchukuliwa kuwa si kamili katika jamii husika na hawezi akaoa au akaolewa. Mtu huyu hawezi akatambulishwa na ndoa katika jamii yake.

Walibora katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* kuhusu tohara ya wavulana na wasichana anasema kuwa, wakati wa msimu wa tohara wavulana hupitishwa barabarani wakitolewa mtoni wakiwa wamepakwa matope kabla ya kuzindikizwa nyumbani kukutana na kisu cha ngariba chenye makali kuwili (uk.44). Kuwahuu wasichana mwandishi huyu anawatambulisha kama watu wanaopenda kushiriki katika itikadi hii ya kitamaduni. Baadhi yao hawapendi kuishi bila kutahiriwa. Hata wakikatazwa na jamaa zao, wanajitambuza kama watu wanaoshiriki katika miviga hii; huku wakiwa wamejificha wasijulikane na wawakatazao. Dina katika riwaya hii ya

Ndoto ya Almasi anajitambuza kama mtu anayeridhishwa na tohara ya wanawake kwa kumwambia Almasi asimwambia nyanya kuwa ameshiriki tohara. Anapoulizwa kama atatahiriwa na mvulana huyu anamjibu:

“Bila shaka. Lakini usimwambie nyanya. Hapendi nitahiriwe. Nitatoroka tu nyumbani akitahamaki nimekuwa mwanamke. Utafikiri nani atanioa nisipotahiri?” (uk.51).

Kutokana na usemi huu inabainika wazi kwamba baadhi ya wanawake wamedhibitiwa na utamaduni na mila za tohara kiasi kwamba hawaoni changamoto zinazoletwa na hali hii. Tohara inaweza kumfanya mwanamke akumbwe na matatizo ya kujifungua baadaye maishani, aambukizwe maradhi kama vile Ukimwi, avuje damu hadi kufa miongoni mwa matatizo mengine.

Wakati msichana anapopitia tambiko hili hadhi yake hubadilika kutoka ile ya chini hadi ya juu zaidi. Hii ndiyo sababu Dina anamfahamisha Almasi kuwa hatapata mwanamume wa kumuoa kama hatapitia miviga hii ya kimila na inayotambuliwa na utamaduni wa Kiafrika. Ni kupitia ukeketaji huu ambapo hadhi yake itaimarika kutoka ile ya mtoto hadi ile ya mtu mzima ambapo anaweza akaolewa.

Wakati wa tohara vijana hufunzwa jinsi ya kuwa jasiri na kuvumilia ugumu wa maisha pasipo kulia kama watoto. Huwa pia wanapewa elimu ya mapenzi baina yao na wale watakaowaoa. Tohara hapa huwa kama shule inayowafunza watahiriwa elimu inayohitajika ndipo wafae katika jamii kama watu wazima. Wanawake huwa wanapitia jandoni ili wawe wanawake kamili walio tayari kuolewa. Huku ndiko wanakopokea mafunzo kuhusu jinsi watakavyojitambuza kama wanawake na akina mama baadaye maishani.

Mbiti (1995:96) anasema kwamba, si Waafrika wote ambao hupitia katika kipindi hiki wakiwa na sherehe muhimu. Lakini baadhi ya wanajamii huwa wanakichukulia kipindi cha tohara kuwa muhimu sana. Nyakati hizi mtu binafsi huwa anapitia mabadiliko ya kimaumbile, kihisia na

kisaikolojia ambayo humtoa kutoka katika hali ya utoto kupitia hali ya kubaleghe hadi ya utu uzima. Haya huwa ni mabadiliko makubwa kwa mtu binafsi.

Wanaume wawili walio miongoni mwa kundi la kutoka nchini Uganda wanaotayarishwa kwa tohara watapitia mabadiliko kama haya. Ingawa umri wao ni mkubwa, tunawaona wanajamii wakitaka watahiriwe kwa kujipa utambulisho wa watu wanaounga mkono utamaduni wa tohara katika jamii yao. Kuwahusu mwandishi anasimulia:

Watu hawa walikuwa wanaume na wanawake pamoja. Walicheza mpaka wakakausha matope yaliyojaa kutokana na mvua siku iliyotangulia. Kati ya wachezaji ngoma wale kulikuwa na wanaume wawili wa takribani miaka thelathini ambao walipakwa matope toka juu hadi chini. Walikuwa wakicheza uchi na ulikuwa huwezi kuwatambua. Mikononi mwao mlikuwa na fimbo. Walicheza sana kufuatia milio ya ngoma tamu iliyotia kila mtu mahali pale wazimu. Mwanamke ndiye aliyeongoza katika kuimba huku wengine wakicheza utafikiria viungo vyao vilikuwa na springi. Mara wanaume hao walipigwa kwa matawi na mtu wakiitikia “woyee! Yaa! Yaa!” (uk.29-30)

Kasu anapotaka kujua ni nini kinachoendelezwa na kundi hili kutoka kwa mama shaibu, anafahamishwa kwamba ni kundi la Wagisu kutoka Uganda ambalo linawatayarisha wale wanaume wawili aliowaona kwa tohara. Pia, aliambiwa na mwanamke huyu kwamba, mtu aliyewapiga kwa matawi na kuruka kama kichaa ni ngariba. Mwandishi hapa anamtambulisha Kasu kama msichana asiyefahamu utamaduni wa tohara za aina hii. Yaelekea Kasu ameishi maisha ya mjini kwa muda mrefu, na ndio sababu utamaduni kama huu hajawahi kushuhudia au jamii yake haiendelezi tohara ya aina hii.

Kisa hiki cha tohara kinaweza kulinganishwa na kingine cha tohara kilicho katika *Ndoto ya Almasi* ambapo jamii inajitayarisha kwa tohara. Katika kisa hiki Walibora anaeleza jinsi Wabukusu wanavyojitayarisha kwa tohara Julai wakingoja Agosti ifike ndipo sherehe za tohara zianze rasmi. Mwezi huu wa Julai wavulana hukusanyika pamoja na kuanza kucheza *chinyimba*

(aina ya kengele inayofanana na zile wafungiwazo ng'ombe shingoni) wakati wa jioni. *Chinyimba* hii huambatana na nyimbo za matusi na masimbulio na mlio wa filimbi (uk.63). Wale ambao hawakupitia tohara kama vile kijana Almasi riwayani husimangwa na kutusiwa kupitia kwa nyimbo kama hizi.

Hapa inadhihirika wazi kwamba, sherehe za tohara huhusisha shughuli tofauti tofauti kama vile uimbaji, uchezeshaji wa viungo vya mwili, kupigwa kwa ngoma, kutayarishwa kwa wanaotahiriwa miongoni mwa maswala mengine. Ni kupitia tohara kama hii ambapo wanajamii humtambulisha mtu kama mmoja wao. Hali hii inabainika katika *Ndoto ya Almasi* kupitia kwa wavulana wanaooga pamoja katika Mto Kapterit bila wasiwasi wowote, kwani wao tayari wametahiriwa na wanajichukulia kuwa kitu kimoja kutokana na kutahiriwa kwao. Wanajitambuza kama kundi moja. Lakini Almasi ambaye bado hajapashwa tohara hataki kujumuika nao asije akatambuliwa nao kama mtu ambaye hajatahiriwa. Anaoga peke yake. Hata anaogopa kufumaniwa na wanawake wanaokuja kuchota maji katika mto huu wasije wakapeleka habari kwamba kijana huyu hajatahiriwa, jambo linaloweza kumfanya atengwe na jamii au atahiriwe kwa lazima (uk.44).

2.1.2 Ndoa kama Kipengele cha Utamaduni Kinachotambulisha Jinsia

Ndoa ni taasisi ambayo inapatikana katika kila jamii kote duniani. Ndoa ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Mucheke (2001:11) anaieleza ndoa kama ushirikiano baina ya mwanamume na mwanamke. Anasema kuwa ni msimamo unaohalalishwa kupitia sherehe za kiserikali, kitamaduni au kidini. Kidesturi watu huoana kutimiza matakwa yao ya kijamii ya kupata watoto.

Hata hivyo, katika *Maisha Kitendawili* ndoa imepewa utambulisho mpya unaoenda kinyume na utamaduni wa Kiafrika. Kasu na mumewe Mjomba wanapewa utambulisho wa watu wasiotilia maanani swala la utaratibu wa ndoa na ulipaji wa mahari. Wao wanakutana mara kwa mara na kisha baadaye mwanamume huyu anaishia kumwoa Kasu. Hata katika kukutana kwao hatuoni mahali popote wanapozihusisha jamaa zao katika mjadala wa ndoa kinyume na ilivyo katika utamaduni wa Kiafrika. Katika utamaduni huu ni lazima jamaa za pande mbili zikutane kujadili swala la ndoa. Hata hivyo, wanandoa hawa wameenda kinyume na utamaduni huu na kulichukulia swala hili kuwa la kibinafsi tofauti na utamaduni wa Kiafrika uliowalea.

Wahusika hawa ni viwakilishi wa vijana wengi wa barani Afrika ambao hawafuati desturi za kitamaduni za ndoa. Kwa wengi utamaduni umechukuliwa kama kikwazo kikuu katika kuhakikisha kwamba wanawake wanafurahia haki zao za kibinadamu na sababu kuu inayofanya jamii kupinga kutekelezwa kwa haki hizi. Utamaduni unabakia pia kuwa kizuizi kikubwa cha haki za wanawake barani Afrika; na pia kuendelea kuwa changamoto kwa wanawake na jamii husika pamoja na serikali na watu binafsi ambao wanapigania haki za wanawake. Wasichana na wavulana hukutania hata mijini na kuoana kama wanavyofanya Kasu na Mjomba bila kuzifahamisha au kuzihuzisha jamaa zao.

Utamaduni wa Kiafrika unamtambulisha mwanamume katika ndoa kama mtu anayetarajiwa kuulisha familia yake na pia kuhakikisha kuwa kuna usalama wa mama na watoto (Ayis, 1979:9). Mwanamume hatarajiwi kumwachia mkewe majukumu ya kinyumbani kama vile kutafutia familia yake lishe.

Ingawa huu ndio ukweli wa mambo, Mzee Omar mumewe Kibibi hatekelezi wajibu huu. Anatambulishwa na mwandishi kama mtu anayeenda kinyume na utamaduni wa Kiafrika, kwani tunaweza kumchukulia kama mtu aliyeshindwa kutimiza wajibu wake kama mzazi na baba kutokana na kuugua maradhi ya pumu tangu alipokuwa mtoto. Anayepewa utambulisho wa kutekeleza majukumu ya kinyumbani ni bibi yake. Hata wakati mumewe anapougua sana ndiye anayetafuta fedha za kumpeleka kwa Mganga Kalulu.

Ingawa mwanamume huyu ameshindwa kuihudumia familia yake jinsi utamaduni wa Kiafrika unavyopendekeza, utamaduni huu unamtambulisha kama mtu muhimu katika ndoa. Kumhusu Omar mwandishi anasema:

Japo hakuwa na kazi na aliendeshwa na mkewe ambaye alikuwa mkulima madhubuti, bado Mzee Omar alikuwa muhimu kwani alikuwa beji ya mji wake (uk.32).

Kutokana na usimulizi huu tunaona kwamba Bi Kibibi anajitambuza kama mchuma wa raslimali za familia yake, tofauti na utambulisho anaopewa na utamaduni na jamii yake. Yeye ni kielelezo cha wanawake wanaoshughulikia familia zao hasa baada ya mume kukumbwa na matatizo yasiyomwezesha kutekeleza majukumu ya nyumbani kama mwanaume na mume.

Mwanamke mwingine ambaye anatambulishwa kama mtafutia familia yake riziki ni mamake Rose. Ndiye anayeitafutia familia yao chakula kwa kuwa mumewe hana uwezo wa kufanya hivyo. Farida anapolalamikia kuhusu kufa kwa wazazi wake na Kim Rose anamwambia:

“...Wajua nilikuwa katika umaskini wa kutosha. Baba yangu ana mkono mmoja na mama hana kazi. Mama ndiye aliyejaribu kutulea. Kila siku tulikula mboga za majani mpaka jirani zetu wakatubandika majina...” (uk.105).

Mwingine aliye na utambulisho sawa na wa Kibibi na mamake Rose, ni Mama Josii. Ingawa mama huyu anakumbwa na changamoto za maisha, ndiye anayeitafutia familia yake riziki. Mumewe hayuko katika nafasi ya kutekeleza wajibu wake kama mwanamume katika ndoa kutokana na maradhi yaliyomkumba kwa muda mrefu. Ni kutokana na hali hii ambapo Kasu hataki kuishi na Mama Josii kwa muda mrefu kutokana na matatizo yanayomkumba ya kuijalia familia yake. Tunasoma:

Hangependa kukaa na yule mwanamke kwa muda mrefu kwa sababu ya mzigo wake alioshindwa kuuchukua. Maana alikuwa na watoto shule nzima. Nyumba yake yavuwa maji paani na kutani. Chakula chake na taabu na mumewe alikuwa mgonjwa sana kwa mnamo miaka saba ni baadhi ya mambo yaliyomfikirisha Kasu... Mumewe alikuwa hana pesa za kulazwa hospitalini. Pesa walizozipata walizila kama zilivyokuja. Palikuwa hapana mahali pengine pa jamaa hii ya Josii kutegemea (uk.68).

Msingi thabiti wa kudumisha ndoa ni ule wenye furaha na mapenzi. Mapenzi yanahitaji kujitolea ndipo yaimarishwe zaidi na kuendelezwa. Muccheke (2001:12) anasema kukiwa na mapenzi ya dhati, ndoa iliyo na furaha inaweza kuvumilia changamoto na matatizo ya kila aina. Kulingana

naye wanandoa wanafaa kujitambuza kama watu wenye maono sawa na kutoshelezana kimapenzi kwa kuwa hii ni muhimu kwa ndoa yenye furaha.

Ingawa Mucheke ana maoni haya, ndoa nyingi za Waafrika huwa zinakosa mapenzi kutokana na udhalimu wanaopata wanawake kutoka kwa waume zao. Mara kwa mara wake hawa hukumbana na matusi au mapigo kutoka kwa waume zao. Juma anamfahamisha Farida kuwa mara kwa mara hapati usingizi kutokana na vita vya jirani wao ambaye huzua ghasia usiku na kuanzisha vita na mkewe. Kwa hakika hii ni ndoa inayokosa mapenzi (uk.164-165).

Ingawa Habwe ameonyesha jinsi ndoa nyingi za jumuiya ya *Maisha Kitendawili* zinavyokosa mapenzi, ameonyesha kuwa si ndoa zote ambazo hukumbwa na tatizo hili. Anaitambuza ndoa baina ya Kasu na Mjomba kama ndoa inayotawaliwa na mapenzi. Wote wawili wana utambulisho wa watu wanaojua kuitunza ndoa yao. Wanapalilia mapenzi yao kwa kutembea pamoja, kula pamoja, kuwatunza watoto pamoja miongoni mwa maswala mengine.

Wanandoa pia wanafaa kujadiliana kuhusu idadi ya watoto wanaotaka kuwa nao na wanahitajika lini. Katika *Maisha Kitendawili* tunakumbana na Kasu akisema kuwa anamwambia mumewe wazae watoto wawili ndipo waweze kushughulikia matakwa yao kikamilifu kama vile kusoma hadi chuo kikuu. Wanandoa hawa wanajipa utambulisho wa wanajamii wanaofahamu changamoto tofauti tofauti kama vile kudorora kwa hali ya uchumi na gharama ya maisha kupanda n.k. zinazokumba bara la Afrika na hivyo basi kuwafanya baadhi ya wanajamii kupata watoto wachache.

Ndoa ni taasisi ambayo hukumbwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto zinazokumba familia ni pale ambapo jamaa ya mtu hupenda kudhibiti ndoa yake. Masengenyo ya kifamilia yanaweza pia kuvunja ndoa. Marafiki wa zamani pia ni changamoto kwa ndoa. Aidha, baadhi ya mahitaji na malengo ya kikazi yanaweza kumfanya mmoja kupuuza familia yake. Kim anajitambuza kama mtu anayeipuuza familia yake. Haitunzi ndoa yake kamwe. Badala ya kuyaelekeza mapenzi yake kwa bibiye ambaye anaishi nyumbani, anayaelekeza kwa Farida ambaye nia yake ni kutumia raslimali zake pasipo kujali maisha ya mwanamume huyu na mkewe.

Habwe amelizungumzia swala hili katika riwaya yake ya *Maisha Kitendawili*. Juma anapotaka kumuoa Farida bila kupitia kwa utaratibu kwa kuifahamisha jamaa yake kwa mujibu wa utamaduni wa Kiafrika, Farida anamwonya vikali kuhusu hili. Anamwambia ni lazima haifahamishe jamaa yake kabla ya kumpa jibu kama wataoana au la. Ingawa Farida amekengeuka pakubwa, kupitia kauli hii tunaona kwamba anajitambuza kama mfuasi wa utamaduni wa Kiafrika kwa kiwango fulani.

Katika jamii zote za Kiafrika huwa kuna taratibu na kanuni kuhusu wale ambao mtu hafai kuwaoa. Mara nyingi wanandoa huwa si watu wa ukoo au nasaba ya mtu au watu ambao ni wa jamaa za mtu kwa upande wa kuumeni ama kuukeni. Hii ina maana kwamba, ndoa kwa watu wa ukoo au jamaa moja hupelekea kuwako kwa mikasa au masaibu ya mauti ya wanandoa au watoto wao. Hivyo ndivyo jamii nyingi huamini barani Afrika.

Gehman (2005:65) anaeleza kwamba, ndoa na kupata watoto ni maswala muhimu sana ya maisha ya Waafrika. Wanaume wasiooa huwa hawapewi nafasi za kusimamia mambo tofauti tofauti katika jamii za Kiafrika, kwani hakuna kategoria ya wanaume wasiooa au wanawake wasioolewa. Anayekataa kuo au kuolewa ni laana kwa jamii yake. Ndoa huwa inatokea baada ya makubaliano ya jamii husika, hivyo basi, swala la ndoa si swala la mtu binafsi, bali ni swala la ushauri na maamuzi ya jamii. Kwa hivyo, mtu asiyepoa au kuolewa huwa anatakosa utambulisho katika jamii za Kiafrika.

Katika bara la Afrika ndoa inachukuliwa kama kiungo cha kuunganisha ridhimu ya maisha. Mbiti (1995:110) anasema kuwa, ndoa ni kiunganishi cha ridhimu ya maisha kwa sababu vizazi vyote huwa vinatambulishwa kama vinaunganishwa pamoja kupitia ndoa – vizazi vilivyoko, vilivyopita na vijavyo. Vizazi vilivyopita ni vingi lakini vinawakilishwa na wazazi wa mtu, kizazi kilichoko kinawasilishwa na maisha ya mtu binafsi na vizazi vijavyo huanza kuja kupitia kuzaliwa kwa watoto katika jamii.

Pia, ndoa kulingana na Waafrika inapelekea kuwako kwa ujenzi wa familia na upanuzi wa uhai wa binadamu kupitia upataji watoto. Kwa hivyo, ndoa huwa imekamilika tu wakati wanandoa

wanapopata mtoto au watoto kadhaa. Ni hali ya kusikitisha iwapo mtoto hapatikani katika ndoa. Wanajamii wataichukulia ndoa hiyo kuwa si kamilifu na mipango mingine itatokea ya kupata watoto katika ndoa. Baadhi ya nyakati wake tasa huwa wanapewa talaka na waume zao. Juliet ambaye anafanya kazi katika mtaa wa *New Rise* ambako Farida anaishi anatalikiwa na mumewe kutokana na ndoa yao kukosa mtoto. Mwandishi anatoa maelezo haya kumhusu Juliet:

Akaolewa ndoa ikakosa mtoto. Baba ya mumewe alimwambia madhali hana chake pale apaondoke asimjazie choo chake bure. Juliet alifunga virago vyake maskini akaanza kuzurura miji (uk. 163).

Katika baadhi ya jamii mwanamke aliye tasa hupewa nafasi ya kumuoa mwanamke mwingine ili bibi huyo amzalie watoto. Hata mwanaume aliyeoa huweza kumpa mkewe nafasi ya kuoia bibi mwingine ambaye anaweza kupata watoto kupitia jamaa za mumewe au wanaume wengine katika jamii. Katika hali hii watoto huwa wanatambuliwa kama watu muhimu sana katika jamii.

Aidha, ndoa inatambuliwa na jamii kama taasisi inayoleta mahusiano mapya baina ya familia na jamii zinaohusika. Hali hii inapelekea kupanuka kwa mahusiano ya kijamii kiukoo au kijamii. Katika kanuni za kindoa, jamaa za msichana na mvulana huwa zinaanzisha uhusiano wa karibu kupitia kutembeleana na kupeana zawadi. Hii ni kutokana na maono ya Kiafrika kwamba mtu haishi peke yake, bali huishi na watu wengine: anaishi kwa sababu ya kuishi kwa wengine (Mbiti 1995:108). Kwa hivyo, kupitia ndoa mahusiano mengi huwa yanaanzishwa, huku wanandoa wakichunguzwa mienendo na tabia zao na wanajamii. Kutokana na sababu hii sherehe za harusi huwa zinaandamana na sherehe nyingi ambazo huhakikisha kuwa kila mmoja amehusika katika ndoa kwa njia moja au nyingine. Tunachoona hapa ni kuwa jamii huwa inataka kujitambua na maswala mengi ya kindoa yanayoendelea katika mazingira yake.

Isitoshe, ndoa hupelekea kuwako kwa utambulisho wa wazazi waliokufa. Mbiti anasema kwamba, kupitia kwa ndoa na upataji wa watoto wazazi waliokufa huwa wanakumbukwa kupitia watoto hawa. Mtu afaye bila kumwacha nyuma mtoto au jamaa wa karibu wa kumkumbuka baada ya kufariki, huwa ni mtu asiyebahatika katika jamii.

Omar na mkewe Kibibi tayari wote ni marehemu, lakini wanaendelea kukumbukwa kupitia kwa wanao Farida na Kasu. Nao ndugu hawa wawili wakiaga dunia watatambuliwa na jamii kama watu hai kupitia kwa watoto wao. Tayari wameshaolewa na wana watoto.

Hali kadhalika, ndoa huwa inawaleta watu pamoja. Mojawapo wa sababu za kuoa ni kuwaleta watu pamoja, kuongeza idadi ya watu, kuwafanya kuwa hai na kadhalika.

Ndoa pia huwafanya watu kupata hadhi katika jamii. Hii ina maana kuwa ndoa ni kitambulisho kinachowapa wanajamii utambulisho fulani. Ndoa huwa inaweka mtu na familia yake katika ramani ya kijamii, kidini na kimaumbile ya jumua yake. Mbiti anasema kuwa, mtu huwa kamili kama ameo na ana watoto. Maisha ya binadamu yanaenda zaidi ya kifo chake kutokana na kuoa na kupata watoto kwake, kwa kuwa watoto hawa wanaendelea kuishi, hata baada ya kufa kwake jambo linalobakia kuwa ithabiti kwamba wazazi wake waliishi wakati mmoja. Wingi wa watoto humfanya mtu awe na hadhi ya juu katika jamii kushinda yule aliye na watoto wachache.

2.1.3 Utamaduni Unavyotambulisha Utumishi wa Nyumbani wa Kijinsia

Utamaduni wa Kiafrika unaipa jinsia ya kike utambulisho wa mtumishi wa nyumbani, huku wanaume wakitambulishwa na utamaduni huu kama watu wasiojijhusisha na shughuli za nyumbani kwa pakubwa. Kuna mifano kadhaa riwayani inayodhihirisha ukweli wa kauli hii.

Farida anapomtembelea Kasu nyumbani anampata akijishughulisha na upishi. Mwandishi anasimulia:

Kasu alibandika maji ya ugali. Yalichemka. Alisonga ugali mdogo wa Farida. Alimtayarishia akamtilia sima na nyama iliyokuwa imesalia na kisamu cha mpira. Kasu alitia tui zito na kijibini kidogo katika kisamvu kwa hivyo ladha yake ilipendeza. Kasu hatumii mafuta mengi na mapishi yake ya nazi yalipendeza (uk.145).

Mwanamke mwingine ambaye anajitambuza kama mtumishi wa kazi za nyumbani ni Juliet. Huyu anafanya kazi nyumbani kwa Farida. Hata hivyo, hakuanza kazi yake hapa. Baada ya

kutalikiwa na mumewe alianza kazi yake kwa Wahindi. Mwandishi anasema kuwa alikuwa akifanya kazi ya kufua na kulea mtoto kwa Wahindi hawa. Tunasoma: “Hapa alifanya kazi ya kufua vigwanda na kuangalia toto ambalo sasa ni jitu zima.” (uk.163).

Wengine wanaotambulishwa na mwandishi kama watu wanaojishughulisha na kazi za nyumbani ni mkewe Kim, Amina, Mama Josii, Rose miongoni mwa wengine. Mkewe Kim anawatunza watoto nyumbani huku Kim akizurura mjini akiwa na Farida. Amina, mkewe Ali anampikia Yasmin chai na kumletea tosti anapowasili kwa ndugu yake saa tatu asubuhi, huku Ali akiwa amepumzika kutokana na machovu ya usiku ya kazi (uk.66). Mama Josii ambaye ana watoto kumi na mmoja baada ya kuwasili nyumbani ikiwa na Kasu, anaanza kujishughulisha na kazi za nyumbani kama vile kuwatafutia wanawe watakapolala. Naye Farida anajitambuza kama mpishi bora baada ya upishi wake bora kule kwa Rose. Tunasoma:

Farida alirejesha makini yake kwenye chapati aliyokuwa akiandaa na Rose akarudi kukaa katika chumba cha wageni huku akiendelea kusoma gazeti... Farida aliingia katika chumba cha kukaa na sinia la vyakula, pande la mkate, chapati nne kwenye sahani na vikombe viwili vya kauri. Birika la chai la kauri lilipendeza macho. Alivitua kwenye kijimeza kidogo. Alipanga vikombe na kumwalika Rose chai huku ameshughulika katika usomaji wa gazeti (uk.100)... Alinyoosha (Rose) mkono wake na kuchukua chapati moja. Aliangalia na akakinai kuwa Farida ni mchawi katika mapishi. Chapati alizipika uzuri sana. Zilimfanya mwenye njaa kushiba hata kabla hajala... Farida alikuwa kama mtu wa kazi kwa Rose khudama maana yake. Mapishi ni yeye. Ufuaji wa nguo ni yeye. Udekaji wa sakafu ni yeye na ununuzi wa vitu vidogo vidogo alikuwa ni yeye (uk.100-101).

2.1.4 Haki ya Urithi kama Kipengele cha Utamaduni cha Kutambulisha Jinsia

Urithi ni kipengele muhimu cha utamaduni wa Kiafrika. Radcliffe-Brown (1881-1955:33-34) anaeleza kuwa, mali hupitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Michakato ya kurithi mali kutoka kwa mzazi mmoja au wote wawili hadi kwa mtoto au watoto wao imekuwa ikitokea katika jamii za Kiafrika kwa muda mrefu. Watu hurithi mali au uongozi kutoka kwa jamaa zao.

Vitu vya kurithishwa katika jamii nyingi za Kiafrika vilikuwa ni kama vile bidhaa za shambani, mifugo n.k. hata wanawake wanapoolewa huwa wanatambuliwa kama mali ya mumewe.

Bwana Mjomba anafikiria kwamba Farida ameolewa na kuwa mali ya mtu kutokana na kutokutana kwao kwa muda mrefu. Katika mazungumzo yao wanasema:

“Karibu tufikirie umejipatia jiko.”

“Nikijipatia kwani siwezi kuja kuwatazama?”

“Aaa mali ya mtu mwingine. Mpaka mwenyewe atoe ruhusa au siyo?”

“Sidhani shemeji. Nitakuwa msaidizi ana ruhusa. Maana si mtumwa yeye.”

(uk.145).

Mwandishi huyu inabainisha kuwa, kwa sasa kuna mivutano katika mifumo ya urithi ambayo imeathiriwa sana na mabadiliko ya kiuchumi yanayotokea katika jamii. Mahali panapoolewa wake wengi panakuwa na changamoto au matatizo ya kuwarithisha watoto mali ambayo kwa hakika inaweza kuwa chache.

Benedek, Kisaakye na Oberleitner (2002:39) wanasema kuwa, kanuni za kimila za kiuchumi na uzalishaji mali zinafanya wanawake kuwa wategemezi na wanaokosa usawa na wanaume. Hivyo basi, wanaume wanatambulishwa kuwa na uwezo wa kurithi mali. Hii ina maana kwamba, kanuni za urithi ambapo umiliki wa mali unapitishwa kwa wanaume peke yao bila kuwajali wanawake. Katika baadhi ya tamaduni nyingi za Kiafrika kama tulivyosema hapo awali wanawake huwa wanatambulishwa kama sehemu ya urithi. Waandishi hawa wanasema kuwa, wajane hawaruhusiwi kujichagulia kama wataolewa na wataolewa na nani. Wanaotoa maamuzi hapa ni wanaume wa jamaa yake pasipo kumhusisha mwanamke kamwe. Hata sio ajabu mwanaume anayeishi mbali na nyumbani kuambiwa arejee nyumbani ndipo apate urithi wake.

Kasu analalamikia swala la wanaume kutambulishwa kama warithi wa mali ya wazazi au jamaa zao, hasa baada ya wao kuaga dunia. Kwa kuwa Kasu ni mwanamke anatambulishwa kama mtu asiye na uwezo wa kurithi mali ya wazazi wake. Hali ya Kasu kutoumbwa mwanaume inamsumbua sana. Mwandishi anasema:

Lau angeumbwa mwanamume na maguvu yake basi asingehangaika kazi, kwani jamaa zake wangemrithisha shamba lake marehemu babake... Lakini mwanamke ameachwa kutamba na kusota na ulimwengu *wake* (uk.61).

Kutokana na maelezo haya tunaona kuwa utamaduni umekuwa kikwazo kikubwa kwa wanawake wa Kiafrika, hasa kutokana na ukweli kwamba hauwapi nafasi ya kurithi mali kutoka kwa jamaa zao. Haumtambui mwanamke kama mtu anayeweza kumiliki mali katika jamii za Kiafrika.

Hata hivyo, Farida katika hadithi yake aliyoandika ya *Baba Ndiye Baba* katika *Maisha Kitendawili* anatambua jinsi baadhi ya nyakati kunavyotokea ubaguzi wa kijinsia unaopelekea baadhi ya watoto wa kiume wasipate urithi katika jamii. Bwana Mokwa anataka kuwarithisha Brain na Jim mali, lakini hataki Ken apate urithi wowote. Farida akimrejelea Mokwa anasema:

Katika hali hii alimwita wakili akaandika wasia wa kuikabidhi familia yake. Nusu ya mali ilimwendea Brain. Iliyosalia ikawa ni ya Jim (uk.170).

Ken anapotaka kujua ni kwa nini babake hakumjumuisha katika wosia wa kurithishwa mali Bwana Mokwa anamwambia:

“Nilitoa urithi wangu kwa waliostahili – wanangu. Wangu kindakindaki.”

“Je, na mimi baba?”

“Hakika Ken mwanangu wewe lakini si babako mzazi.” (uk.171).

Kioja hiki kinapotokea Ken anamwendea mamake, Lucy, ili amweleze babake ni nani. Anapoulizwa swali hili anamdanganya kwamba babake kwa jina Mike Johnston alifia nchini Uganda wakati wa vita vya Idi Amini; na kwamba alimwachia mali kabla ya kufa kwake. Kwa kuwa hafurahishwi na jibu la mamake, anamwambia, “Mama lakini si mali nitakayo ni baba, baba mzazi, usuli wangu.” (uk.173). Kutokana na maelezo haya inabainika kuwa baadhi ya nyakati watoto wa kiume wanaweza kukosa urithi ikiwa mama zao waliolewa wakiwa nao au walipatikana nje ya ndoa. Hata hivyo, watoto husika wanapotambua kwamba hawamfahamu

baba mzazi huwa wanawasumbua mama zao ili wawajulishe baba zao ni nani. baada ya kusumbuka kwa muda Ken anakuja kugundua kwamba babake ni Joseph ambaye ni mtumishi wa Mungu; kasisi bila shaka.

2.2 Uchumi na Utambulisho Kijinsia

Kwa muda mrefu mwanamke wa asili ya Kiafrika amekuwa akikumbana na dhuluma za kiuchumi barani Afrika au nje ya bara hili. Kohen (1993:19-20) anaeleza kuwa, jinsi wanawake watumwa wa Kiafrika walivyokuwa wanakumbana na maisha magumu ya kiuchumi nchini Brazil. Anaeleza kuwa wanawake hawa walikuwa wanafanya kazi ngumu na za kibaguzi mashambani na nyumbani. Wanawake hawa walikuwa wanafanya kazi kama vile kupika, kuosha, uyaya katika makasri, malezi ya watoto ambapo walicheza nao, wakawalisha, wakawaosha, wakawavalisha miongoni mwa kazi nyingine za nyumbani. Mambo kama haya yanatokea katika jumuiya ya *Maisha Kitendawili*. Julieti ni mwanamke anayefanya kazi ya kumlea mtoto wa asili ya Kihindi. Anapooona akidhulumiwa kimapenzi na babake mtoto huyu anaamua kuiacha kazi hii na kuenda kufanya kazi ya nyumbani kwa Farida.

Kwa muda mrefu bara la Afrika limeshuhudia jinsia ya kiume ikijipa utambulisho wa kudhibiti harakati za uzalishaji wa mali kwa manufaa na faida zake. Juma ana wadhifa mkubwa wa kuzalisha mali katika *Tertiary Bank*. Hatuoni mwanamke aliye na wadhifa kama huu riwayani licha ya wengi wao kuwa wasomi kama vile Farida na Rose. Wanawake hawa wana shahada kutoka chuo kikuu jinsi Juma alivyo nayo, lakini wanafikia kiwango cha kuwategemea wanaume katika kuendeleza harakati zao za kiuchumi. Farida ambaye alisoma na Juma katika chuo kikuu anaishia kupewa mkopo wa kuanzisha biashara na Juma. Hiki ni kitambulisho kwamba wanawake wameachwa nyuma katika harakati za uzalishaji mali katika jamii.

Wanawake wengi katika ulimwengu wa kikazi wanapata malipo ya chini, wanakumbana na hali ngumu katika mazingira yao ya kufanyia kazi, wanafanya kazi za hadhi ya chini na mshahara wao huwa chini. Kasu na Yasmin Taabu ni wanawake wanaofanyia kazi katika mazingira magumu, kwani wanaishi katika nyumba mbovu wanayouzia makaa. Makaa haya yanawapa kipato cha chini, hivyo basi, kubakia katika hali ya ufukara. Hata hawana fedha za kulipia

nyumba yao kodi. Baadaye kunatokea matajiri wanaouza makaa kwa wingi jambo linalopelekea biashara yao kudorora na hatimaye kufikia kikomo.

Barbara (1993) anasema kwamba, wanawake wengi nchini Uingereza wameajiriwa kazi katika nafasi finyu sana. Kuna wanawake wachache ambao wanafanya kazi kama mawakili, madaktari, wachanganuzi wa kompyuta; na mwanamke mmoja kama mhandisi au mwanasayansi katika kila wafanyakazi kumi. Hii inamaanisha kuwa wanawake wanatambulishwa kama watu wasio na idadi kubwa katika sekta ya uajiri jambo ambalo ni ukiukaji wa haki za kibinadamu. Katika jumuiya ya *Maisha Kitendawili* kuna wanaume wengi wanaofanya kazi za kuajiriwa wakilinganishwa na wanawake. Ali, Mjomba, Juma, Mazuri miongoni mwa wanaume wengine wanafanya wameajiriwa kazi katika sekta tofauti tofauti; huku wanawake wachache kama vile Rose wakiajiriwa kazi na kufutwa. Wengine wanapokosa ajira hii wanaamua kujiajiri wenyewe kama vile Farida anayeanzisha kampuni yake na kuwaajiri watu kadhaa.

Einhorn (1988:22) anasema kuwa, wanawake wengi hawapati malipo sawa na yale ya wanaume. Kwa kuwa wanawake na wanaume huwa katika kazi tofauti, ni rahisi kwa waajiri kuwa na ubaguzi dhidi ya wanawake. Pia, ni rahisi kwa wanawake kupoteza kazi wakilinganishwa na wanaume. Hii ni kwa sababu wengi wanaofanya kazi ya muda wa ziada ni wanawake kuliko wanaume. Hali hii hutokea wakati kunapokuwa na kudorora kwa uchumi wa taifa.

Barbara (1993:52) kuhusu ufanyaji wa kazi anasema kwamba, unakumbwa na ubaguzi wa kijinsia wa kiitikadi. Anakubali kuwa mwanya mkubwa baina ya jinsia umekuwa kikwazo kikubwa katika jamii. Wanaume wamebakia kuwa wadhibiti wa maswala yanayohusiana na jinsia katika baadhi ya sehemu. Mathalan, wanawake wengi huwa na matatizo ya kufanya kazi hadi wakachelewa kule kazini na kutembea kwenda sehemu zilizo mbali na wanakofanya kazi, huku ikitiliwa maanani kuwa huwa kuna hatari ya kubakwa ambayo huwa inawakodolea macho.

Barbara (1993:28) akirejelea taifa la Tanzania anaeleza kuwa, miundo mingine ya kijinsia kama vile ukahaba imeibuka. Anasema kwamba ufasiki unaleta mapato au riziki ya juu kuliko aina nyingine za ajira zilizoko za wanawake na wasichana. Kando na makahaba wanaofanya kazi za

uasherati katika barabara za mijini, wanawake wengine wanatambulishwa kama wanaoendeleza ukahaba na wakubwa wao kazini, walimu na wanaume wengine kama njia ya kuongezea riziki yao. Hapa huwa wanapewa ‘zawadi’ za chakula, nguo au mlo wa kumezea mate. Jambo kama hili ni wazi katika jumuiya ya *Maisha Kitendawili*, kwani wasichana kama vile Farida na Rose wanashiriki mapenzi nje ya ndoa ili kupata vyakula, vileo, mavazi, fedha, kazi, alama za juu kutoka kwa wahadhiri n.k.

Benedek, Kisaakye na Oberleitner (2005:34,35) wanasema kuwa umaskini na kudorora kwa hali ya uchumi katika sehemu nyingi za dunia kama vile mataifa mengi ya Afrika na baadhi ya sehemu nyingi za Asia na Marekani zimechangia kuwako kwa ukahaba. Wanawake wazima na watoto wameingilia ukahaba kwa kiwango kikubwa. Kuna rekodi za kushangaza zinazoonyesha jansi kulivyo na ukahaba wa kushurutishwa unaotokana na kutekwa nyara kwa wasichana. Pia kuna usherati unaotokana na kuuzwa kwa wasichana na familia zilizo maskini. Wanawake wengine wanauzwa kimagendo au kulanguliwa katika baadhi ya sehemu duniani na kuingizwa katika ukahaba bila hiari yao. Mathalan, kule Thailand takribani wasichana 80,000 walio chini ya miaka 16 wanauzwa wakiwa na miaka 11 kupata riziki yao ya kila siku kupitia ukahaba.

2.3 Siasa, Uongozi na Jinsia

Katika *Maisha Kitendawili* tunakumbana na Chifu Mazuri ambaye ni wa jinsia ya kiume. Hii ina maana ya kwamba baadhi ya vyeo vya uongozi wa kisiasa vilivyodumu kabla ya kuja kwa mkoloni vingalipo mpaka hivi leo na mara nyingi jamii imevitengea wanaume na wanawake kuvipata ni nadra sana. Baadhi ya majukumu yaliyoendelezwa na machifu hao yangali yanaendelezwa na machifu wa kileo. Mathalan, Chifu Mazuri anahudhuria mazishi ya Omar na mkewe Kibibi na kuwahimiza wanajamii wawasaidie watoto wawili ambao ni Kasu na Farida walioachwa na wazazi hawa.

Kadhalika, kulikuwa na chifu wa kitarafa ambaye alikuwa chini ya chifu mkuu. Huyu ndiye aliyeendeleza shughuli za uongozi katika kitengo hiki cha utawala.

Utawala wa kikoloni haukutupilia mbali taasisi hizi za kimila au kiasili za uongozi, lakini ulizitambua, ukaziidhinisha na katika baadhi ya nyakati ulizitumia kikamilifu kupitisha sera zake za kikoloni kwa wananchi.

Afrika imepita hatua mbalimbali za kisiasa na ambazo zimechangia historia ya kisiasa ya bara hili kwa pakubwa. Afrika iligawanwa na wakoloni mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa ambapo kila koloni iliwapanga watu upya kulingana na kanuni za kikoloni zilizotakikana na ukoloni husika. Wakoloni hawa walianzisha mifumo tofauti tofauti ya uongozi barani Afrika kama vile nchi kuongozwa na rais. Wengi wa viongozi hawa wa juu wamekuwa ni wanaume mpaka hivi leo.

Katika riwaya hii kuna nyadhifa tofauti kama vile zile za uchifu na urais. Mwandishi anawapa wanaume utambulisho wa uongozi riwayani. Bwana Musa Oligoposema ni rais wa nchi. Anatambulishwa kama mtu anayetambua umuhimu wa elimu katika jamii. Kiongozi huyu wa taifa anahudhuria sherehe za kufuzu za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzalendo. Katika hotuba yake anawahakikishia wafuzu kwamba wangepata kazi katika idara tofauti tofauti za serikali. Hata hivyo, hawaishii kupata kazi walizoahidiwa, kwani wahusika kama vile Farida Omar na Peter Manono wangali taabani kwa ukosefu wa kazi baada ya kufuzu kwao. Rais huyu aliwataka pia watu wawe waaminifu kwa chama tawala pamoja na utamaduni wao (74-75).

Wanawake wengi barani Afrika huwa hawajishughulishi na mazungumzo yanayohusisha maswala ya kisiasa. Huwa wanawaachia wanaume ambao hujitambuza kama watu wanaofahamu yote kuhusu siasa za nchini mwao na za ng'ambo. Kazi ya wanawake huwa ni kusikiliza yale yanayosemwa na wanaume hawa au baadhi ya nyakati wakayapuuza pia. Wakati Kim na Papi wanapozungumzia maswala ya kisiasa Farida hachangii chochote. Wanazungumzia jinsi nchi ya Marekani inavyozidhulumu nchi nyingine za ulimwengu kwa kunyakua mafuta yazo, kuangusha serikali yazo n.k.

Wanaume wanatambulishwa kama jinsia iliyo na usemi serikalini kuliko jinsia ya kike. Hata kama jinsia hiyo iko serikalini mara nyingi huwa inapokea maagizo kutoka kwa wanaume. Wanaume huwa na usemi serikalini kiasi kwamba wanaweza kuitafutia jinsia ya kike kazi katika

idara tofauti za kiserikali. Si ajabu kupata kwamba watu wakubwa serikalini wakizitafutia jamaa zao za kiume au kike kazi serikalini au katika sekta za kibinafsi. Kwa kuwa babake Angela ni mtu mkubwa serikalini anamtafutia msichana huyu kazi na vitu vingine vinavyohusiana na kazi yake bila tatizo lolote. Tunasoma:

Angela alibahatika kupata kazi hata kabla ya kumaliza masomo yake chuoni.

Babake Angela alikuwa gogo serikalini na alifanya juu chini akampenyeza Angela huko. Angela alipewa gari la Toyota ambalo limeinuka juu kimo cha twiga na kwa kuwa alitamani uhuru wake, alipewa nyumba. Hayo yote yalifanywa kwa mipango ya babake (uk.80).

Viongozi wa kisiasa wanajitambuza kama watu wanaowadhulumu wanawake katika jamii. Baadhi ya nyakati wanawatusi na kuwazomea. Hata wanawake wanaofanya kazi za nyumbani kwa viongozi wanakumbana na udhalimu unaopita mipaka kutoka kwa wanasiasa waliowaajiri.

2.4 Dini na Utambulisho wa Jinsia

Katika sehemu hii tutachunguza jinsi dini inavyochangia katika ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii za Kiafrika. Ingawa dini ni taasisi muhimu katika inayorajiwa kuwapa watu mwongozo mwema, imetumiwa kuwanyanyasa wanawake.

Kim anakumbuka jinsi Terira alivyopelekea kuanguka kwa Samson. Mwandishi wa riwaya hii anasema:

Kim alikumuka mafundisho yake katika siku ya Jumapili kwamba ni pendo la Terira lililomfanya Samson, joma la misuli kufichua siri ya nguvu zake. Hicho kilikuwa chanzo cha ushindi wa Wafilisti (uk.14).

Mwandishi pia anatambua unafiki unaoendelezwa na jinsia zote katika dini. Anampa Rose utambulisho wa mtu mnaofiki aingiapo kanisani. Hapa anajitamuza kama mtu wa Mungu, ilhali yeye ni mtu anayeshiriki usherati na uavyaji mimba; mambo ambayo ni kinyume cha amri za Mungu zinazosema usizini na usiue. Aidha, Kanisani anawawaongoza waumini katika nyimbo

kufikia kiwango cha kusifiwa nao kutokana na uimbaji bora. Huwa anawahimiza waimbe. Tunasoma:

“Ndugu zangu kwa jina la Yesu tutaimba pambio moja ili kumtukuza Yesu kwa kutufia dhambi zetu. Haya tuanze: ‘Yesu, Yesu, Yesu, ameshinda, ameshindaa, ameshindaaa, aaa...uchawi, uchawi, umalaya, mauti, wizi, uchoyo uongo ... lo Yesu ayeeh!’ Umati huitikia na kuimba kwa furaha. Baada ya kukaa minong’ono hupita kanisani. Watu wakasema: “Huyo ndugu ana kipawa. Huyo amebarikiwa.” (uk.56).

Mbiti (1995:61, 67) anasema kuwa, watu wanapokutana kwa ibada ya umma huwa wanaimba, wanadansi, wanapiga makofi na kuonyesha furaha yao. Baadhi ya sherehe za ibada huwa zinahusisha kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine. Wakati wanapofanya hivi, watu huwa wanapiga ngoma, wanacheza ala au vyombo vya muziki, wanashangilia kwa pamoja kwa pamoja.

Rose pia huwa anaendeleza sala anapowasili kanisani kwa ibada. Mbiti (1995:60) kuhusu ibada anasema, kuwa ni mbinu za kuhakikisha kwamba, kuna mawasiliano baina ya watu na ulimwengu wa uunguni au usioonekana. Ibada inachukuliwa kama mbinu za kujenga umoja katika ulimwengu wa binadamu. Watu wanapokumbwa na matatizo huwa wanamwelekea Mungu. Wakati huu huwa wanataka kudumisha amani, furaha na usalama. Ibada huwa inawasaidia kupata amani na umoja katika maisha yao na ulimwengu kwa jumla. Ibada huwa inajenga uhusiano wa kirafiki baina ya binadamu na Mungu wao.

Mbiti (1995:61, 62) anaeleza kwamba, katika dini huwa kuna sala. Sala ni mbinu inayotumiwa sana kuwasiliana na Mungu. Baadhi ya sala hufanywa katika kiwango cha kijamii, katika mikutano ya umma na kwa mahitaji ya umma. Mtu yeyote yule anaweza kumwomba Mungu wakati wowote na mahali popote pale. Hata hivyo, kuna watu ambao huomba kwa niaba ya wengine kama anavyofanya Rose katika *Maisha Kitendawili*.

Watu huomba kwa sababu tofauti na nyakati tofauti. Watu huomba kwa sababu wanaamini kwamba Mungu anawasikiliza, anawakubali na kujibu maombi yao.

Katika riwaya hii tunaona kuwa, kiongozi wa Kanisa la mwombaji wa dini ya msalaba mweusi liko katika hali mbaya na badala ya kuliombea liwe katika hali nzuri, anawaombea watu. Anajitambuza kama mwanaume anayejitambulisha na dini kwa ajili ya kujinufaisha kutoka kwa watu wajao katika kanisa hili. Licha ya kuwaporwa watu na kushindwa kulikarabati linabakia kuwa na matatizo mengi. Watu wanaweza kuona ndani wakiwa nje. Mlangoni pana kinyesi cha mbwa. Pia mlango wenyewe unafunguka kwa shida kwani kanisa lenyewe limeinama na liko tayari kuanguka wakati wowote ule. Viambaza vyake vimedondoka udongo wake pia.

Licha ya kanisa hili kuwa katika hali mbaya wanawake wengi wanajitambuza kama wategemezi walo katika kusuluhisha matatizo yanayowakumba. Kuna baadhi yao wanaoamini kuwa matatizo ya ndoa yanaweza kupata suluhisho kutoka katika kanisa hili. Mwandishi anasimulia:

Mtu na mke wake walikuwa wamekuja kushtakiana kuhusu ndoa yao. Mke alimwambia mhubiri kuwa kompresa ya mume wake imesimama, haifanyi kazi hilo likapelekea watu kucheka. Mume alijitetea lakini wanawake walimcheka wakimhimiza mkewe amwache mume wake ikiwa ataendelea kuizembea dhima yake (uk.131).

Kasu, nduguye Farida anaonekana kuweka matumaini yake yote katika dini. Anaona kwamba matatizo yanayomkumba nduguye yatapata suluhisho katika dini. Yuko tayari kutumia njia zote kuhakikisha kwamba Farida amepata nafasi ya kumfikia mhubiri ambaye anatoa mahubiri yake akiwa sehemu ya mbele ya kanisa lake. Tunasoma: Kasu alifanya ufundi mpaka akamwingiza Farida kwenye mbao za mbele ili wakitoka wale aingie yeye (uk.131).

Mwandishi anawatambulisha wanaume kama viongozi katika dini. Mhubiri wa kanisa la Msalaba Mweusi ni mwanamume, si mwanamke. Mwandishi anatufahamisha kuwa ni mcheshi lakini mkali ukimdanganya. Watu ni mbumbumbu katika dini kiasi kwamba hawajali kuhusu anakotoa nguvu za utabiri wake. Tunasoma:

Kama alitabiri kwa nguvu za Maulana kweli au za mashetani hakuna katika wateja wake aliyejali. Kila mtu alitaka shida yake ishughulikiwe, basi (uk.131).

Maelezo haya yanawatambulisha baadhi ya viongozi wa kidini kama watu wanaotumia njia za ushirikina katika kuendeleza maswala yao ya kidini kwa kisingizio kwamba wanafanya miujiza.

Katika dini wahubiri wanajitambuza kama watu wanaowadanganya waumini wao. Mhubiri wa kanisa la Msalaba Mweusi ambaye ni wa jinsia ya kiume anaonekana kusema uongo wa jinsia ya kike na ambayo inajitambuza kama iliyo na matatizo mengi ya kuletwa kanisani kuliko ile ya kiume. Uongo wake unabainika kupitia mazungumzo yake na mwanamke mmoja. Yanaenda hivi:

“Wewe ni jeuri kwa mume wako,” mhubiri alianza kunena.

“Si kweli.”

“Si kweli namna gani na Mungu ndiye anayesema. Aaa Mungu anasema atakuponya ugonjwa wako.” (uk.132).

Udanganyifu wa mhubiri huyu pia unaendelea kutambulikana kupitia kwa Farida. Yaelekea afahamu chochote kuhusu binti huyu, bali anayosema ni ya kubahatisha. Farida hana kazi wala mume, lakini mhubiri huyu anampa utambulisho wa mfanyakazi na mke wa mtu. Pia, anamtambulisha kama mtu aliyekuwa juha masomoni huku tukifahamu kwamba alikuwa mwerevu ndipo akapita mtihani na kujiunga na chuo kikuu. Maswali yake kwa Farida ni ya kubahatisha ukweli wa mambo. Kama ni mtabiri kwa nini asitabiri pasipo na kubahatisha?

Aidha, mwandishi anamtambulisha mwanamke kama mjeuri wa dini. Farida anamlaumu Mungu kwa kuuchukua uhai wa Julia ambaye alikuwa ni mwanamke mwenye hekima na msomi. Tunasoma:

Farida alimwona Mungu jeuri kama ingewezekana hekima na elimu yote aliyokuwa nayo Julia mtu mwingine akapewa dunia ingeendelea (uk.154).

2.5 Jamii na Utambulisho wa Kijinsia Katika *Maisha Kitendawili*

Kwa kiwango kikubwa jamii imekuwa ikimdhaliisha mwanamke kwa kumpa majukumu na nafasi ya chini katika jamii. Hata hivyo, katika fasihi simulizi jamii inawatambulisha wanawake kwa jinsi mbili, ametukuzwa na amedhalilishwa.

Kuna pia miiko inayoimarisha uendeshaji wa utaratibu wa kimaadili na kidini. Wazazi wa Farida na Kasu waliwalea watoto wao kwa maadili ya dini ya Kiislamu. Mwandishi anasimulia:

Hawa watoto walililewa katika misingi ya kijijini na utamaduni wa kwao pamoja na mawaidha ya dini ya Kiislamu, maana Wailamu wao (uk.33).

Benedek, Kisaakye na Oberleitner (2002:37) wanasema kuwa, haki ya kupata huduma ya afya inapuuuzwa na jamii. Mwandishi wa *Maisha Kitendawili* anasimulia kuhusu mwanamke anayeletwa na mumewe katika hospitali aliyienda kupata huduma ya matibabu Mzee Omar. Mwanamke huyu anayepuuuzwa na daktari anaaga dunia muda mfupi baada ya kufikishwa hospitalini. Mwandishi anasema:

Mwanamke yule aliyeonekana mwanamke mrembo sana alianza kulia kwa uchungu wa kusimama pale na kukereketwa mwilini na michomo mikali ya maradhi. Mara daktari aliingia na kusema, “Nitaanza na watu wa kwanza kufika hapa.” Mwanamke yule aliyekuwa kazidiwa alimwangukia daktari kwa macho ya kuomba msaada lakini daktari akatembea kiaskari na kuingia ndani bila ya kumjali. Baadaye mwanamke yule alijibwaga chini baada ya muda mfupi na kurusharusha viguu. Punde si punde akanyooka na kumeza pumzi (uk.35)

Huenda kama mwanamke huyu angepata huduma ya matibabu haraka iwezekanavyo hangekumbwa na mauko kama yaliyomkumba. Huu ni utambulisho kwamba jinsia ya kike anabaguliwa katika kupata huduma za afya jamiini. Wanawake wanaonekana tu kama watoaji wa huduma za afya na watunzi wa watoto, bali si kama watu wanaohitaji huduma za afya na kuimarishwa kwa hali zao.

Ubikira ni swala lingine linalotambuliwa na wanajamii kama muhimu sana. Ayis (1979:6) anasema kuwa, baadhi ya jamii za Kiafrika zinachukulia mapenzi kuwa swala muhimu sana katika ndoa. Hivyo basi, ubikira unatiliwa maanani na jamii. Wanawake wanapoolewa wanatarajiwa kuwa mabikira, kwani wanasawadiwa wanapopatikana wakiwa wamehudumisha ubikira wao. Ayis anasema kuwa, miongoni wa Wakaani, mama na wasichana huwa wanakabidhiwa zawadi na mkwe ikiwa msichana anapatikana akiwa bikira siku ya ndoa.

Siku hizi ni vigumu sana kumpata msichana bikira, ikizingatiwa kuwa vijana wengi wa jinsia zote mbili wanajihusisha na maswala ya ngono kabla ya kuolewa kwao. Wahusika kama vile Farida na Rose tayari wameshashiriki mapenzi na wanaume kabla ya kuolewa na kuuvunja ubikira wao. Ajabu ni kwamba utamaduni wa Kiafrika unatambua ubikira wa jinsia ya kike na kusahau kwamba hata ubikira wa mwanamume ni muhimu katika jamii. Ingekuwa vyema zaidi kama utamaduni huu ungetambua ubikira wa njia zote mbili, bali si kuipuuza moja kana kwamba si sehemu ya jamii ya Kiafrika.

Jamii nyingi za Kiafrika huwa zinakataa kujamiiana kwa watu walio na uhusiano wa kijamaa. Siku hizi kumekuwa na mabadiliko makubwa katika maswala ya kimapenzi ya Waafrika. Maswala ya ngono au kujuana kimwili yanafanywa hadharani na bila siri yoyote tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Yanafanywa wazi bila kuficha chochote. Farida ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzalendo anatambulishwa kama mwanamke anayekimbilia ngono kwa pupa. Wanafunzi wengi wa kiume wameshiriki ngono naye na wakawa hawamtembelei tena, isipokuwa Juma na wenzake wachache ambao walikuwa wamebaki kumganda mwanamke huyu. Huu ni utambulisho wazi kwamba jinsia ya kiume inapojua ya kike kimwili huwa inaanza kupunguza mapenzi yake kwayo; huku ile ya kike ikiendelea kuyatamani zaidi. Kumhusu Farida mwandishi anasema:

Wengi wa wanaume walikwisha mtupa, hawaji tena kwa Farida hasa kijana mmoja – Julius Manono – ambaye alionekana imara, alikuwa kapotea kabisa. Huyu kijana alikuwa mbeja sana. Hata hivyo, alikuwa akimchezea Farida ili apate matilaba yake. Alipoupata mustakabali wake basi huyo. Akatokomea zake shimoni. Mpaka leo na kesho Farida hamwoni kutia mguu wake chumbani

mwake. Hakuona cha mno cha kumrejsha kwa Farida. Yeye Manono anajuta kwani hakuona jambo la zaidi lililomfanya kumganda Farida. Farida kwake ameshakuwa tambara mbovu (uk.11-12).

Aidha, Kimathi Masumari ameshatosheka na mapenzi ya Farida, lakini Farida angali anataka waendeleo kuwa wapenzi. Kimathi anapotoweka Farida anakumbwa na matatizo ya kisaikolojia. Kwa muda wa miezi sita tangu akamilishe masomo ya chuo kikuu hajamwona Kim. Anahuzunishwa na hili sana. Baadaye anapopata habari kwamba Kim ameuawa anahuzunika zaidi. Hamiini kwamba mpenzi wake amemwacha milele. Halichokosa kutambua Farida ni kwamba Kim hakuwa anamtaka kwa mengine ila mapenzi, na alipoona ameyapata akamtoroka msichana huyu aliyekuwa na matumaini ya kutafutiwa kazi na kuolewa naye.

Ayis (1979:23) anaeleza kwamba, punde tu baada ya mtoto kulia, jinsia yake hutambulishwa na mkunga, na huwa anamfahamisha mamake mara moja. Mama anafaa kufahamu kila kitu kumhusu mtoto kabla babake hajajulishwa kuhusu kuzaliwa kwa mtoto huyo. Jinsia inaweza kupata utambulisho kupitia idadi fulani ya kemi zinazofanywa baada ya kuzaliwa. Kwa mfano, jamii ya Wakikuyu nchini Kenya huipa utambulisho jinsia ya kiume kwa kutoa kemi tano huku wakiitambuza ile ya kike kwa kutoa kemi nne. Hii ina maana kuwa jinsia ya kiume inapendelewa zaidi kuliko ile ya kike. Katika jamii nyingi za Kiafrika wavulana huwa wanathaminiwa zaidi kuliko wasichana katika familia na jamii kwa jumla. Hata hivyo, mwandishi *Maisha Kitendawili* anaonyesha kwamba fikra na mawazo ya aina hii yanaendelea kupitwa na wakati. Mwandishi huyu anaitambulisha jinsia ya kike kuwa muhimu katika jamii kama ilivyo ile ya kiume. Haifai kuonekana kama duni kwani ina wajibu wake wa kutekelezwa katika jamii. Mzee Omar amejaliwa kuwapata wasichana wawili: Farida na Kasu. Mzee huyu aliona mtoto ni mtoto hata awe wa jinsia gani. Mwandishi anatufahamisha:

Lakini ilivyo kawaida na desturi kwa watu wakikosa mtoto wa kiume yeye hakuhangaishwa hata chembe kwani yeye Omar akiamini watoto ni zawadi toka kwa Mungu. Na ilivyo kawaida ya mtoa zawadi humwelezi cha kukutolea (uk.33)

Hali hii ni tofauti sana na wanaume wengi wa Kiafrika. Baadhi yao huwalaumu wake zao kutokana na hali ya kutowapata watoto wa kiume kufikia kiwango cha kutaka kuwataliki. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* tunafahamishwa kuhusu jinsi Zacharia alivyomzomea mkewe kutokana na kumzalia watoto wasichana kabla ya kumpata mvulana kwa jina Emmanuel baadaye maishani. Aliwathamini sana watoto wa kiume. Zacharia ni kiwakilishi cha jamii ya Kiafrika ambayo huchukulia watoto wa kiume kuwa muhimu na bora kuliko wale wa kike. Ni kutokana na hali hii ambapo jamii zangi za Kiafrika hutaka kujua jinsia ya mtoto mara tu baada ya kuzaliwa kwake.

Ayis (1979:96-100) anasema kwamba, mabadiliko ya kijamii katika Afrika Mashariki yanamaanisha maendeleo katika sehemu fulani na hali duni ya maendeleo katika sehemu nyingine.

Nayo mabadiliko ya kimuundo humaanisha mabadiliko yanayotokea katika viambajengo vya mfumo wa kijamii kama vile kuwa na upangaji uzazi ambapo familia inakuwa ndogo wala si kubwa. Jinsia ya kike inajitambuza kama isiyotaka watoto wengi kutokana na matatizo yaliyoko ya uchumi na yanayopelekea hali ya maisha kuwa ngumu zaidi. Kasu anajitambuza kama mtu anayetaka kuwapata watoto wachache ili awe katika nafasi ya kuwaona wakisoma na kujiunga na vyuo vikuu. Kwa kuwa yeye alikuwa mwerevu na hakupata nafasi ya kuendelea na masomo yake hadi chuo kikuu kutokana na changamoto za kifamilia, furaha yake ni kuwaona wanawe wakifikia upeo wa elimu ambayo yeye aliikosa. Aliyaacha masomo akiwa darasa la nne baada ya kubakwa na mjomba wake na kuishia kutoroka kwake.

Mabadiliko haya pia yanahusisha, mabadiliko ya hali ya ndoa au kuolewa kwa wanawake na wajibu wanaotekeleza katika jamii baada ya kuamua kutoolewa kamwe maishani.

Jamii inampa mtu aliyesoma utambulisho wa kutofanya kazi za mashambani. Inatarajia mtu aliyepata elimu, hasa ya chuo kikuu afanye kazi mjini; lakini si kurudi kijijini kufanya kazi za shambani. Manoti Peter anadhihirisha ukweli wa kauli hii. Anamwambia Farida:

“Mimi baba ana shamba kubwa ningerudi nyumbani nikalima hilo shamba lakini

ubaya wa nyumbani watu walioniona nikisoma, watu waliokuja katika party zangu za kufuzu katika daraja mbalimbali na kuniletea zawadi watanicheka. Siwezi kurudi. Siwezi! Kama ni kufa nitakaa hapa nifie hapa,” Manoti akasema kwa uchungu huku akitembea hatua kadhaa (uk.119).

Ingawa Manoti anaogopa jamii itasema nini akirudi mashambani, Farida hatishwi na hilo. Anajitambuza kama mtu aliye tayari kurudi mashambani na kwenda kufanya kazi huko. Hili linadhihirika kupitia usemi wake. Anamwambia Manoti, “Ningalikuwa wewe ningalirudi...” (uk.119). Kwa hakika maisha ya mjini yamemfunza mengi binti huyu, jambo linalomfanya kuwa na ukakamavu wa kutojali jamii itasema nini ikimwona akifanya kazi mashambani kama mtu asiyepata elimu ya chuo kikuu.

Kadhalika, jamii inamtambulisha mwanamke aliyesoma kama mtu asiyefaa kuishi mashambani. Wanatarajia aishi mjini. Rose anapoenda mashambani anawashangaza akina mama ambao hawatarajii aishi mashambani. Mwandishi akimrejelea Rose na kina mama hao anasema:

Anakumbuka siku moja alipokuwa kule kwao shamba, kina mama walimwuliza,
“Utarudi lini mwanangu nikutume ukanisalimie mwanangu jijini.”

“Hivi karibuni,” Rose angejibu.

“Siku ikifika nijulishe nikupe barua.”

“Haya,” Rose angesema.

Kwa nini? Rose si mmoja wao tena? Hawawezi kumwona kama mtu aliyekuja kukaa bali si mgeni wa daima (uk.184).

Jamii inachukulia pia watoto wanaposoma wanakuwa katika nafasi nzuri ya kujipatia kazi. Wanaokoza kusoma wanatambuliwa na jamii kama watu wanaokumbana mara kwa mara na ukosefu wa kazi. Kasu ambaye ni kiwakilishi cha jamii anajitambuza kama mtu aliye na mawazo kama haya. Kwingi anakoenda kutafuta kazi haipati kutokana na kutosoma kwake. Hii ndiyo sababu Kasu anawahurumia sana watoto wa Mama Josii ambao hawaendi shuleni kutokana na ukata unaoikumba familia yao. Wana umaskini kiasi kwamba baba yao anayeugua hana fedha za

kwenda hospitalini kutafuta matibabu.

Ingawa Kasu ana maoni haya, si lazima watu waliosoma wakapata kazi. Kuna waliosoma na wakaikosa ama wakapata kazi ambayo kipato chake ni cha chini ikilinganishwa na elimu yake. Katika riwaya ya *Pamba Habwe* anampa Pamba utambulisho wa mtu asiyenufaika na elimu yake baada ya kupata kazi ya uhadhiri. Profesa huyu anaendelea kukumbwa na hali ngumu ya maisha licha ya kutoka ng'ambo akiwa na matarajio makubwa kuwa angepata kazi yenye malipo mazuri nchini mwake kwa elimu ya juu tayari ameikumbatia. Maisha yanapomshinda anaishia kujitia kitanzi na kuuacha ulimwengu na matatizo yake.

Jamii inatambulishwa na mwandishi kuwa muhimu sana katika kushirikiana na watu waliokumbwa na mkasa katika jamii. Kama ni mkasa wa kifo huwa inajumuika pamoja na waliompoteza mpenzi wao.

Mzee Omar anapoaga dunia wanajamii wanafika kwa wingi kuomboleza kifo cha mzee huyu wakiwa na mkewe. Tunasoma:

Kibibi alijifunga kibwebwe. Aliomboleza na kuomboleza tena. Lau
kuomboleza kungekuwa kunamfufua mfu basi Omar angefufuka siku hiyo.
Mkojo ulimtoka hivyo Kibibi. Makamasi yalimning'inia na akajikaragaza chini
kama wazimu. Wanakijiji waliomboleza naye (uk.40).

Baadaye naye Kibibi anaaga dunia. Hakijulikani kilichomuua bibi huyu ni nini. Kumhusu mwanamke huyu mwandishi anasimulia:

Baada ya masaa tisa ya kuomboleza Kibibi alizidiwa na nguvu. Mwili
wake ulimnyong'onyea na kungwi aliyepewa kazi ya kumwangelia mpaka kifo
cha mumewe na matanga yeshe akatangazia watu kuwa hata Kibibi naye alikuwa
kafa (uk.40).

Hali hii inawahuzunisha waombolezaji zaidi. Mwandishi anawatambulisha kama watu waliojawa na mahangaiko kwa sababu ya kumpoteza mwanamke huyu pia huku ikitiliwa maanani kwamba mumewe alikuwa tayari amemtangulia kwenda jongomeo. Pia anasema kuwa watu wengine waliranda mji mzima kwa huzuni na vilio na nyasi hazingeweza kuonekana mahali popote (uk.41).

Jamii inatambulishwa kuwa na jukumu la kuwatunza watoto walioachwa nao baada ya wazazi wao kuaga dunia. Mwandishi anasema kwamba wengi katika wale walioomboleza walitetea vifaranga wawili walioachwa na marehemu Mzee Omar na mkewe Kibibi Omar. Mzee Majani ambaye ni kiwakilishi cha jamii anajitambuza kama anayefahamu wajibu wa jamii katika kuwatunza watoto mayatima ambao ni Kasu na Farida. Mzee huyu anasema:

“Waliokufa wamefumzika miomo ya dunia, lakini sisi tulio hai ndisi tulio na taabu.
Hawa watoto tumeachiwa sisi kuwaangalia.” (uk.40).

Usemi wa Mzee Majani unaungwa mkono na Chifu Mazuri ambaye anajitambuza kama mtu mwenye huruma na mapenzi. Anawaambia watu wafikirie kuhusu watoto walioachwa nyuma na marehemu. Anataka wanajamii washirikiane katika kutoa mchango wa kuwasaidia wasichana hawa wasio na baba wala mama. Anasema:

Yatupasa tufikirie zaidi juu ya tufanye nini ili kuwasaidia hawa watoto walioachwa nyuma nasi. Sasa mimi naona kitu kimoja tu. Hawa watoto tuwafanyie mchango baadaye kama kweli tuliwapenda marehemu na ama kweli tuna simanzi halisi na kama kweli sisi ni watu.” (uk.42).

Baadhi ya wanajamii huwa wanawachukua watoto walioachwa na wazazi wao na kuwapa hifadhi katika miji yao. Baadhi ya nyakati watoto hawa hukumbana na dhuluma na ubaguzi kutoka kwa watu hawa wanaowatunza. Mzee Marufuku ambaye ni kiwakilishi cha jamii, anajitambuza kama mjomba anayewajali watoto wa ndugu yake. Anawaonea huruma. Baada ya mazishi ya wazazi wao anawachukua na kwenda kuishi nao nyumbani kwake. Tunasimuliwa:

Baada ya matanga kukamilishwa, Mzee Marufuku aliwakaribisha wapwaye kwa furaha yake ya kawaida (uk.42).

Licha ya kukaribishwa huku, mkewe mzee huyu ambaye anayetambulishwa na kujitambuza kama mwenye chuki na anayekosa mapenzi anakasirishwa na kuchukizwa na kuletwa kwa watoto hawa nyumbani kwake. Siku moja mke huyu anamwambia mumewe:

“Wewe mizigo yako imekushinda na hicho kilimo chako cha mihogo umekwenda mbali huko kutafuta mengine. Au ukiwa mwanaume waona mzigoto wote waweza kuubeba? Wengine mna uume wa kuzaa wala si uume wa fikira.” (uk.42).

Mkewe Marufuku anapokuja juu kama mto wa kifuu, mumewe anamwomba awaonee watoto wale huruma, kwani ni mayatima; mkewe anamjibu kwa mkazo: “Basi ukawachukue mayatima wote ulimwenguni uwaangalie wewe kama una huruma sana.” (uk.43)

Wanajamii wanajitambuza kama watu wanapowaona watu wa njia mbili wanapokuwa pamoja huwa wanazungumzia maswala ya mapenzi. Mara nyingi wanapowaona wanaume na wanawake wakishirikiana kwa njia moja au nyingine wanachukulia kwamba wameletwa pamoja na maswala ya kimapenzi.

2.6 Asasi ya Elimu na Utambulisho wa Kijinsia

Coats (1994:29) anaeleza kuwa, jamii huwa na matarajio na mazoea tofauti katika majukumu ambayo wanaume na wanawake wanapewa na jamii jambo ambalo linaathiri ujitambuzi na utambulisho wao katika sekta ya elimu. Majukumu haya wanayopewa na jamii huanza kufunzwa jinsia zote pindi tu wakiwa watoto wadogo. Majukumu haya yanaendelezwa zaidi katika elimu ya chekechea kama anavyoeleza mwandishi huyu.

Wazee wanawatambulisha wanawake kama watu wasiofaa kupata elimu katika jamii za Kiafrika. Mugambi (1982) akirejelea tamthilia ya *Jirani Kanyolewa* ya Jay Kitsao anawatambua wazee kama watu wasiotilia maanani elimu ya mtoto msichana. Ingawa Chadi ni msichana mwenye bidii masomoni na anayepita mitihani vizuri sana, babake hataki aendelee na masomo yake.

Anasingizia kwamba hawezi kumlipia mwanamke karo ambaye atakuja kuolewa baadaye. Anasingizia pia kwamba ana watoto wengine watano shuleni wanaohitaji karo na wengine wadogo nyumbani anaowakidhia mahitaji yao. Ingawa anajidai kwamba mambo haya ndiyo yanayomfanya asimlipie Chadi karo, ukweli ni kuwa alitakalo ni kujitajirisha bila kujali maslahi ya binti yake. Kilicho muhimu kwa mzee huyu ni kuolewa kwa bintiye, bali si kuendelea na elimu. Bila shaka hii ni kasumba iliyopitwa na wakati na ambayo inafaa kuzikwa katika kaburi la sahai. Mtoto wa jinsia ya kike ana haki ya kupata elimu bila ubaguzi wowote.

Hata hivyo, utambulisho wa jinsia ya kike ni tofauti katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Mwandishi anawatambulisha wanawake kama watu wanaosoma na kuhitimu katika viwango vya elimu vya juu kama vile vyuo vikuu. Farida, Rose, Mary ni baadhi ya wanafunzi wa jinsia ya kike wanaosoma hadi chuo kikuu. Walisomea Chuo Kikuu cha Mzalendo. Aidha, watoto wa kike wanaokosa elimu wanatambulishwa kama wanaoikosa elimu hiyo kutokana na hali ya umasikini, bali si wazee kuwakataza kujiunga na shule. Watoto wa Mama Josii, Agnes na Jane hawaendi shuleni kutokana na ufukara unaoikumba familia yao.

3.0 Hitimisho

Katika sura hii tumetoa maelezo kuhusu ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kwa kuegemea kwa asasi tofauti tofauti za kijamii kama vile utamaduni, dini, uchumi miongoni mwa nyingine.

Tulianza kwa kushughulikia utamaduni ambapo tulipata kwamba vipengele vya kitamaduni kama vile ndoa, tohara, urithi miongoni mwa vingine kwa pakubwa vinaitambulisha jinsia ya kike kama isiyokuwa na uwezo wa kupata urithi ikilinganishwa na ile ya kiume. Tumeona kuwa utamaduni huu unamtukuza mwanamume na kumdhalilisha mwanamke. Kwa mfano, tumeona kwamba katika ndoa mwanamke anaonekana kama kiumbe anayefaa kuwa chini ya utawala wa mumewe. Hata hivyo, tumeona kwamba kumetokea mabadiliko kadha katika ndoa ambapo yale mambo yaliyokuwa yakizingatiwa zamani ya kindoa yamekumbwa na mabadiliko. Tukija kwa urithi tumegundua kuwa utamaduni unaipa mwanamume uwezo na mamlaka ya kurithi mali ya jamaa yake akilinganishwa na mwanamke ambaye harithi chochote kutoka kwa wazazi wake.

Tukija katika asasi ya uchumi tumeona kuwa jinsia ya kiume inajitambuza na kujitambulisha kama iliyo na mamlaka ya kudhibiti harakati zote za uzalishaji wa mali katika jamii. Pia tumeona kuwa mwanamke anayebahatika na kufanya kazi huwa anakumbana na dhuluma za kikazini kama vile kunyimwa malipo, kustaafishwa mapema, matakwa yake kutotetewa na vyama vya wafanyakazi ambapo wengi wanavyovitawala huwa ni wanaume.

Katika asasi ya kisiasa tumeona kwamba, wanaume wanajitambuza na kutambulishwa na jamii kama wanaofaa kushikilia usukani wa uongozi kuanzia kiwangu cha nyumbani hadi cha kitaifa. Jinsia ya kike hapa haitambulikani kama iliyo na uwezo wa kuongoza. Hata serikalini wanaume wanaonekana wakiwa na usemi sana kuwaliko wanawake.

Tumegundua pia dini ni asasi nyingine inayoikandamiza jinsia ya kike, huku ikiitukuza ile ya kiume. Asasi hii inamtambulisha mwanaume kama kiume aliye na mamlaka kwa jinsia ya kike. Ni kutokana na kauli ambapo mwanaume anaendelea kumdhulumu mwanamke kwa kisingizio kuwa dini imemruhusu afanye hivyo. Aidha, dini inamtambulisha mwanamke kama chanzo cha matatizo duniani. Isitoshe, John Habwe katika riwaya ya Maisha Kitendawili amezitambulisha jinsia zote mbili kama zinazoendeleza unafiki katika dini.

Tukija katika asasi ya jamii tumepata kuwa, kuna jinsi inavyomtambuza mwanamume na mwanamke katika jamii. Asasi hii inawapa wanaume viongozi usemi kuliko wanawake. Kuhusu elimu inazitambua jinsia zote mbili kama zilizo na uwezo wa kupata kiwango sawa cha elimu. Hata hivyo, wanawake wanaonekana kulemewa na changamoto za elimu wakilinganishwa na wanaume. Tumegundua pia nyakati za misiba jamii inajitambuza kama iliyo na ushirikiano katika kuungana pamoja na kumsaidia au kuwazaidia wanaokumbwa na mikasa katika jamii.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa asasi mbalimbali za kijamii zimeungana pamoja kuitukuza jinsia ya kiume huku kwa kiwango kikubwa zikiikandamiza ile ya kike ambayo utambulisho wake katika jamii ni wa chini.

SURA YA TATU

UJITAMBUZI NA UTAMBULISHO WA KIJINSIA KIUMRI

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tunajadili ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kwa kuegemea kigezo cha kiumri. Ni muhimu tukiri hapa kwamba, ni vigumu sana kufahamu umri kamili wa kimiaka wa wahusika katika kazi za kifasihi, hasa ikiwa mwandishi hajataja umri wao katika kazi husika ya kifasihi. Hata hivyo, mhakiki, mchanganuzi au mtafiti wa kazi ya fasihi anaweza kukisia umri wa wahusika kwa mujibu wa makundi matatu ya kijamii ambayo ni watoto, vijana na wazee kwa kutegemea na kuegemea maelezo na usimulizi wa mwandishi kuhusu nafasi zao na majukumu yao katika jamii. Hii ina maana kwamba, mwanafasihi anaweza kusimulia kisa au hadithi kwa namna ambayo inamfanya mtafiti kufahamu kuwa mhusika fulani ni mtoto, kijana au mzee. Ni kwa kutegemea kipengele hiki ambapo tutatoa maelezo kuhusu ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia wa makundi matatu tofauti ya kijamii tuliyotaja hapo juu. Hii ina maana kwamba, hatutakuwa tukiegemea umri wa kimiaka kama tulivyotanguliza kusema hapo awali. Hii ni kwa sababu kama zilivyo riwaya nyingi za Kiswahili, riwaya ya *Maisha Kitendawili* imeshindwa kwa kiwango kikubwa kutaja umri wa wahusika kimiaka. Hata kama John Habwe angetaja umri wa kila mhusika haingetusaidia pakubwa katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu si rahisi kuwa na umri jumuishi unaokubalika na jamii zote za Kiafrika kwamba ni wa utoto, ujana au uzee. Yaani hakuna mipaka ya kusema ni miaka mingapi anayopasa kuwa nayo mtoto, kijana ama mzee. Kinachotumiwa na jamii nyingi ni makisio tu ya kiumri pasipo na kuegemea katika kigezo cha umri kamili kinachokubalika na jamii zote. Katika utafiti wetu tutadhibitiwa na ukweli wa usemi huu katika kutoa ufafanuzi wetu kuhusu umri. Hata hivyo, tutakuwa makini tusije tukamweka mhusika katika kundi ambalo hafai kamwe kujumuishwa humo. Ni muhimu tueleze hapa kwamba, kuna baadhi ya wahusika wanaopatikana katika makundi tofauti tofauti ya kijamii kwa mintarafu ya vipindi tofauti vya kiwakati kama vile kuwa watoto, baadaye kuwa vijana na kadhalika. Kwa kiwango kikubwa Habwe ameturahisishia kazi yetu kwani katika usimulizi wake katika sehemu nyingi riwayani amewataja wahusika kama watoto, vijana na wazee.

3.1 Ujitambuzi na Utambulisho wa Watoto

Ulezi wa watoto ni swala muhimu katika jamii. Watoto hupokea malezi kutoka kwa wazazi wao, jamaa yao na jamii kwa jumla. Mtoto hutambulishwa kama mali ya jamii takribani katika

sehemu zote barani Afria. Watoto wakiwa wadogo sana huwa hawajitambulishi na jinsia yoyote. Hata huwa hawajui jinsia ya kiume au ya kike ni nini. Baadaye wanapoendelea kukua ndipo wanapokuja kutambua tofauti zao, wakajua kwamba ni wanawake na wanafaa kujitambuza na jinsia ya kike au ni wanaume na wakaanza kujitambuza na jinsia ya kiume. Wakaanza kutenda mambo kulingana na jinsia yao na utamaduni wao. Kwa kiwango kikubwa tabia na mienendo ya kijinsia huwa inatawaliwa na utamaduni wa jamii husika.

Wavulana wanatambulishwa kama watu machachari na watukutu. Suleiman ambaye ni mwanawe Mjomba anapotaka kuruka barabarani anaitwa na mamake, Kasu. Yeye hatambua kwamba kuna hatari katika kuvuka barabara ile. Tayari ameanza ile tabia ya wanaume wengi ya kutojali mambo. Ni katika hali kama hii ambapo watoto wa kiume wanapokua kiakili, kimwili na kisaikolojia wanaanza kujifunza kutoka kwa jamii na utamaduni kwamba, mwanamke ni mtu wa kudhulumiwa. Ni kutokana na ukweli huu ambapo wanaume wanakuwa hawajali haki za mwanamke katika jamii.

Watoto wanatambulishwa pia kama watu wanaosema mambo waziwazi bila kuficha. Suleiman anawaambia wazazi wake kwamba anataka biskuti huku akiwa ameubedua mdomo wake. Aidha, watoto wanajitambuza kama watu wanaofuata yale yanayosemwa au kufanywa na ndugu zao, hasa ndugu ambao wamewashinda kiumri. Suleiman anapoitisha biskuti naye nduguye, Kassim anasema kwamba hata yeye anahitaji biskuti zake (uk.123). Hii ni hali ya mtoto kutaka kujitambuza na mambo yanayofanywa na mtoto mwenzake. Watoto kama hawa ni viwakilishi vya watoto katika jamii pana ya Kiafrika ambayo inawaruhusu watoto kuwa na tabia kama hizi. Ni nadra kupata watoto kama hawa ambao ni vielelezo vya jamii wakiadhibiwa na wazazi wao kutokana na tabia kama hizi; na kama kuna kuadhibiwa aghalabu tabia ya mtoto au watoto husika huwa imevuka mipaka. Hii ndiyo sababu tunaona Mjomba na mkewe wakitimiza matakwa ya wanao bila kujishughulisha na kuwaadhibu. Wazazi kama hawa wanawalea watoto kwa niaba ya jamii.

Malezi ya watoto hutambulishwa pia na kujihusisha kwao na michezo. Watoto walioko hospitalini anakopelekwa Omar na Kibibi kupata matibabu wanajihusisha na kucheza. Tunasoma:

Kwenye ubao uliosaki watu kulikuwa na vitoto viwili vichafu na manati shingoni.

Mara kwa mara vilicheza sakafuni na kurudi katika nafasi zao ubaoni (uk.35).

Watoto wakiwa wadogo kama tulivyosema hapo awali huwa hawatambui jinsia yao, hivyo basi, katika maswala yao kama vile kucheza huwa hayatawaliwi na udhalimu wa kijinsia sana kama inavyokuwa baadaye katika maisha yao. Ni baada ya kukua ambapo wanakuja kugundua tofauti zao za kijinsia jambo linalopelekea kuwako kwa ukandamizaji wa kijinsia kwa mujibu wa utamaduni husika.

Upataji wa elimu ni jambo lingine muhimu katika jamii. Katika jamii nyingi za Kiafrika elimu ya mtoto wa kike huwa haitambuliwi na jamii ikilinganishwa na ile ya mtoto wa kiume. Ni kutokana na ukweli huu ambapo katika jamii nyingi barani Afrika wanawapeleka wavulana wao shuleni na kuwaacha wale wasichana nyumbani. Bila shaka huu ni udhalimu kwa jinsia ya kike. Katika *Maisha Kitendawili* mambo ni tofauti. Jinsia zote mbili zinaonekana kukumbwa na changamoto sawa katika usakaji wa elimu. Katika riwaya hii watoto wengi wa jinsia ya kiume na kike wanatambulishwa kama waliokosa elimu kutokana na changamoto tofauti tofauti za kimaisha. Hata hivyo, wa kike wanaelekea kuwa na idadi kubwa kushinda wale wa kiume. Baadhi yao wanakosa elimu kutokana na uyatima wao ambapo wanakohamia wanakumbana na matatizo na kuamua kuiacha elimu yao. Kasu hana wazazi ambao anaweza kuwategemea katika elimu yake. Tayari wote wameaga dunia. Anapoenda kwa mjombake ili aendelee na masomo anambaka na kumfanya ayaache masomo yake na kutorokea mjini. Wengine baba zao wana wake wengi hivyo kuwa vigumu kwao kuwashughulikia masomo yao kutokana na hali watoto wengi wanaowategemea kiuchumi. Kuna mvulana anayekuja kununua bidhaa katika kibanda cha Kasu. Anamwambia Kasu kuwa, hawezi akaendelea na elimu kutokana na hali ya babake kuwa na wake kadhaa.

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa mtoto wa jinsia yoyote anaweza kukumbwa na matatizo ya kielimu tofauti na jinsi jamii nyingi za Kiafrika zinavyochukulia. Jamii hizi zinachukulia kwamba wanawake ndio wanaokosa elimu katika jamii. Kasu na mvulana

tuliomtaja hapo juu ni vielelezo vya watoto wa jinsia mbili zinazokosa elimu kutokana na maswala tofauti ya kijamii na kitamaduni.

3.2 Ujitambuzi na Utambulisho wa Vijana:

Katika utafiti wetu tutachukulia vijana kama wale wavulana na wasichana ambao wanasoma katika shule za upili na vyuo vikuu. Wengine ambao tutawajumuisha katika tapo hili ni wale watu ambao hawajaoa au kuolewa, lakini kulingana na maelezo ya mwandishi tunaweza kuwaita vijana kwa mujibu wa nafasi zao riwayani. Hii ni kwa sababu baadhi ya nyakati kunaweza kukatokea wazee katika kazi za fasihi na wakawa hawajaoa. Kuna baadhi ya vijana ambao wanapatikana katika makundi tofauti ya kiumri kadri riwaya inavyopiga hatua mbele kuelekea kileleni kama vile Farida na Kasu wakati fulani kuwa watoto na mwingine kuwa vijana. Hata hivyo wahusika hawa ni wachache riwayani. Hawa tutakuwa tukiwaeleza kwa mujibu wa umri wao. Hali hii itatuepusha na mtafaruku au mgogoro wa kumtolea mhusika maelezo ya kijumla kana kwamba hatujui yuko katika hatua gani ya kiumri maishani mwake.

Vijana ni watu wanaotegemea jamii katika kuendeleza maisha yao. Jinsia ya kike inajitambuzi kama inayotegemea ile ya kiume kiuchumi katika kuendeleza maisha yake. Kwa muda mrefu utamaduni wa Kiafrika umemtambulisha mwanamke kama mtegemezi wa mwanaume katika kuendeleza maswala tofauti tofauti maishani. Farida ambaye ni kiwakilishi cha wanawake katika jamii anadhihirisha hali hii. Anasema: “Mimi siwezi kuolewa na mtu asiye na pesa. Haya sahu.” (uk.115). Maisha ya Farida anaishi kwa kuwategemea wanaume. Anamtegemea Kimathi kwa kupata kazi baada ya kuhitimu kutoka katika chuo kikuu. Pia anamtegemea Kim kwa ndoa. Anataka mwanamume huyu amuo baada ya kukamilisha masomo yake. Hata hivyo, mwanamume huyu hatimizi matakwa ya Farida. Badala yake anatoroka asionekane tena. Hali hii inamsikitisha sana mwanamke huyu. Ingawa mwandishi anawapa baadhi ya wahusika wa jinsia ya kiume utambulisho wa watu wanaowadanganya wanawake, ili wawatoshelezee mahitaji yao ya kimwili, anawatambulisha baadhi yao kama watu walio tayari kuwasaidia wanawake kwa hali na mali. Mathalan, Manoti Peter anapompata Farida akiwa na njaa anamsaidia.

Mwingine anayemsaidia kwa pakubwa Farida Omar ni Juma ambaye walisoma pamoja katika Chuo Kikuu cha Mzalendo. Huyu kupitia *Tertiary Bank* anampa Farida mkopo wa kuanzisha

biashara. Kwa wakati huu Juma ni mkurugenzi wa benki hii. Hivyo basi, inakuwa ni rahisi kumfanyia Farida mpango wa kupata usaidizi wa kifedha kutoka katika benki hii. Hapa mwanaume anajitambuza kama mtu mwenye huruma na ambaye yuko tayari kuwasaidia wanaokumbwa na matatizo tofauti tofauti.

Pia mwandishi anampa mwanamke utambulisho wa kutegemea jamaa zake, hasa baada ya kushindwa na maisha. Hali hii inadhihirika wazi kupitia kwa wahusika kama vile Farida, Taabu Yasmin, Kasu miongoni mwa wengine. Farida anapokumbana na changamoto za maisha kama vile ukosefu wa kazi anaenda kuishi kwa ndugu yake Kasu ambaye tayari ameolewa. Kumhusu Farida tunaelezwa:

Sasa ameguria Jamboni kwa ndugu yake mdogo, Kasu. Katika nyumba ya Kasu na mumewe Farida aliongeza hesabu ya mtu mmoja zaidi kuwafanya kuwa watano kwa jumla. Kasu na mumewe Bw. Mjomba waliwashughulikia bila kuchoka kwani walihisi uzuri Farida kuwa mikononi mwao kuliko kuwa na walimwengu (uk.121).

Rose anamtegemea Mzee wa *Volvo* kwa mengi. Aameanzisha urafiki na mzee huyu ili amlipie Mary ambaye ni ndugu yake dada huyu karo ya shule ya sekondari. Pia anataka mzee huyu amtafutie kazi. Hata hivyo, Rose hakufanikiwa kwa hili baada ya mauko ya mzee huyu. Maelezo haya yanadhihirisha wazi kwamba, jamii na utamaduni zinamtambua mwanamke kama mtu anayemtegemea mwanamume katika kuendeleza maisha yake.

Vijana ni watu wanaoshirikishwa katika harakati za kiuchumi. Hata hivyo, katika jamii nyingi za Kiafrika kwa muda mrefu utamaduni umekuwa ukimnyima mwanamke usemi katika harakati za uzalishaji mali. Mwanamume ndiye ameachiwa maswala ya kudhibiti harakati hizo. Hali hii inaleta athari hasi za kiuchumi barani Afrika. Hata hivyo, riwaya ya *Maisha Kitendawili* inapiga vita utamaduni wa aina hii na kutambua umuhimu wa jinsia zote mbili kushiriki katika maswala ya kiuchumi.

Katika riwaya hii vijana hasa wanawake wanajitambuza kama watu wanaoelewa hali ya uchumi katika nchi zao za Kiafrika. Hali ya uchumi katika mataifa mengi ya Afrika imekuwa ikidorora kutoka siku moja hadi ile nyingine. Hali hii imefanya gharama ya maisha kupanda. Farida anatambua kwamba hali ya uchumi imewafanya watu kutoishi pamoja na kujaliana kiuchumi. Farida anamwambia Mjomba:

“...Wajua shemeji kisumbuacho watu ni hali ya kiuchumi. Hata watu wenye mikono hawataweza. Kwani bei ya bidhaa zaruka juu ngani kila siku. Mishahara nayo imeganda papo hapo mwaka hata mwaka.” (uk.125)

Vijana wengi wamepewa utambulisho wa ukosefu wa kazi katika jamii nyingi za Kiafrika. Wanatafuta kazi katika sehemu tofauti tofauti mijini bila mafanikio. Wanapoitwa kwa mahojiano ya kazi wanafika kwa wingi lakini baadaye wanachukuliwa wachache sana hata kufikia wawili baadhi ya nyakati. Wasichana kwa wavulana wanafikia kiwango cha kununua suti kwa ajili ya mahojiano haya au hata kuwaomba wenzao mavazi au fedha za kujirembesha kabla ya siku ya mahojiano yenyewe. Mwandishi anatueleza jinsi vijana wanavyofika kwa wingi wakiwa wamejipamba kwa mahojiano katika kampuni ya *Price House*. Kinachobainika hapa ni kwamba, tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo wanaume waliachiwa majukumu ya kiuchumi; wanawake wameanza kujishughulisha na harakati za uzalishaji mali katika jamii. Hii ndio sababu tunawaona vijana wa jinsia mbili wakijibidiisha kutafuta kazi katika makampuni kama hili la *Price House*.

Vijana ni watu wanaojitambuza kama wapenda anasa na starehe. Wanaenda katika vilabu na kumbi za kujiburudishia na kujistareheshea. Kule huwa wanajihusisha na shughuli kama vile ulaji wa vyakula, utumiaji wa vinywaji na ulevi.

Farida anaandaliwa sherehe kubwa na Kim baada ya kufuzu kwake kutoka Chuo Kikuu cha Mzalendo. Binti huyu anawakaribisha baadhi ya marafiki zake katika sherehe hii. Marafiki hao ni kama vile Rose, Juma, Mary miongoni mwa wengine. Waliofika mwanzo walipewa vinywaji. Sherehe kubwa ilianza baada ya wao wote kuwasili. Katika hafla hii waliandaliwa minofu ya

kuku, mbuzi na ng'ombe, wali, sima miongoni mwa vyakula vingine. Farida alilewa baadaye akiwa na wenzake katika sherehe hii.

Rose naye anajitambuza pia kama mpenda anasa. Msichana huyu anashiriki ulevi kwa pakubwa. Anaenda jioni katika Florida Club kulewa na mzee wake. Baada ya ulevi wanaagana kuonana hatimaye. Hata anapopata kazi baada ya kukamilisha elimu yake ya chuo kikuu anaendelea na ulevi wake. Baadaye anaachishwa kazi kutokana na ulevi huu kama Farida anavyomweleza Juma. Pamoja na haya msichana huyu hakubali kuwa ameachishwa kazi kutokana na kushiriki vileo, bali anasema kuwa alifutwa kazi kutokana na fitina za kikabila.

Ufafanuzi huu unabainisha kwamba wanawake hasa waliosoma wanajaribu huu chini kujitafutia uhuru na usawa walionyimwa na jamii kwa muda mrefu. Ingawa wanashirikiana na wanaume katika kujistarehesha kwa njia tofauti tofauti kama njia ya kutafuta usawa, wao ndio wanaoishia kukumbwa na matatizo zaidi wakilinganishwa na wanaume.

Kadhalika, vijana wa jinsia zote mbili wanajitambuza kama watu wanaokimbilia mapenzi kwa pupa. Katika harakati za kutimiza matakwa yao ya kimwili wanajitambuza na kutambulishwa kwa jinsi tofauti tofauti.

Jinsia ya kike na ya kiume zinajitambuza kama zilizo na wivu wa kimapenzi. Mara nyingi mwanamke anapokuwa na urafiki na mwanaume fulani, huwa hataki mwanamume huyo anyemelewe na mwanamke mwingine. Farida anashuku kwamba, Mary ambaye anasoma naye katika chuo kikuu anamnyemela Kimathi Masumari.

Mary anajitambuza kama mtu asiyesahau urafiki wake na wanaume. Wakati wa sherehe anayoandaliwa na Kim kusherehekea kufuzu kwa Farida ambapo msichana huyu amewaalika marafiki zake, Mary anaonekana kuwa na wivu moyoni kumhusu Kim ambaye wakati mmoja alitaka awe rafiki yake.

Kim naye ana wivu wa kimapenzi ambapo hataki Farida kuwa na urafiki na wanaume wa chuoni. Anashuku kwamba, msichana huyu ana urafiki wa kimapenzi na vijana wanafunzi wa chuoni. Kim anasema:

“Naona wewe wanicheza mchezo mbaya Farida... Naona mnashughulika zaidi na hao vijana chipukizi wenu...” (uk.7).

Kuhusiana na mapenzi baadhi ya wahusika wa jinsia ya kike wanajitambuza kama wanaodumisha usafi na urembo ili kujipendekeza na kuwavutia wanaume. Juma anapoingia chumbani mwa Farida anapata kwamba kumepambwa kwa ajili ya kumngoja Kim. Tunasoma:

Ua lilikuwa limewekwa katika chupa pale mezani. Vitambaa vilitandazwa kwenye meza. Alijua (Juma) kuna mambo. Hayo maandalizi ni ya wenyewe mabingwa. “Lakini ubingwa wa nini?” Roho ilimtesa akili zilipomwuliza, “Ubingwa wa gari na pesa? Haya.” (uk.3)

Jinsia ya kike inamtambua mwanamke kama mtu anayejiona kama pambo. Juma hapendezwi na jinsi wanawake wanavyojiona kama mapambo ambao mara nyingi siasa yao ni ya anasa na starehe. Amefikia kiwango cha kuamua kutoa kutokana na jinsi wanawake wanavyojichukulia kama mapambo na wapenda anasa.

Kadhalika, wasichana wa chuo kikuu wanajitambuza kama wenye kuwaonea gere wasichana wenzao wanapowaona wakiwa na wapenzi wao wa kiume. Wasichana wanaomwona Farida akiwa na Kimathi wanamwonea kijicho msichana huyu. Tunasoma:

Farida alipojichoma katika gari kwa kupitia mlango wa kushoto, wasichana waliokuwa wakibarizi katika ubao wa kushoto wa maegesho hayo walipiga mbinja. Wengine walimkonyeza. Msichana mmoja Lucy, mwenye sura zisizotamanika lakini aliyekuwa hodari katika somo la sheria alimwangalia Farida na kutamani angekuwa yeye (uk.7).

Mwandishi anaipa jinsia ya kike utambulisho wa kujipendekeza kimapenzi kwa jinsia ya kiume ambayo ni ya tabaka la juu; na kuidunisha ile ya tabaka la chini. Farida anamthamini Kim ambaye ni wa tabaka la juu na kuwadunisha Juma na wenzake ambao ni wa tabaka la chini. Anatumia njia zote kuhakikisha kuwa anadumisha mapenzi yake na Kim. Mathalan, mwandishi anasimulia kuhusu tabia ya Farida akiwa garini kwa Kim. Anasema:

Shingo yake kailekeza na macho karibu ayafumbe kama mwenye usingizi. Ila Farida yeye ni mwenye kupenda. Pendo lilimjaa tele kama mtu aliyefanyiwa dawa za mchawi kilingeni (uk.7).

Jinsia ya kiume nayo inatumia utambulisho wa kifedha na mali kupata wapenzi wa kike. Farida anampenda Kim kwa kuwa ana gari na fedha. Baadhi ya nyakati wanaenda kwa gari la Kim kujistarehesha katika ukumbi wa Kibokoni kwa pombe. Anayegharamia bidhaa hii si mwingine, bali ni Kimathi Masumari.

Pia, Kim na Farida wanapokuwa garini wakienda Kibokoni wanaiona gari barabarani ambapo mle ndani mna msichana na mvulana anayeelekea kuwa wa tabaka la juu akiwa anamkumbatia msichana. Mwandishi anasimulia:

Gari hilo la aina ya Toyota lilikuwa likiendeshwa kwa mkono mmoja. Mle ndani mwake mlikuwa na binti mmoja akiwa amekumbatiana na mvulana aliyekuwa akiendesha kwa mkono mmoja (uk.8).

Mwingine ambaye anajitambuza kama mpenda tabaka la juu ni Rose. Mwandishi anasema kuwa Rose alivutiwa na wanaume wambeja na wenye mali. Msichana huyu aliwahasudu wanaume ambao baba zao wana mali.

Utambulisho huu wa Rose ndio unaotumiwa na Tom kijana ambaye ni mzembe na mlofa kumlaghai Rose kimapenzi. Kijana huyu ambaye anasoma chuoni Mzalendo na Rose na anayejitambuza kama mwenye majigambo na majisifu mengi yasiyo na maana anatumia udhaifu

wa Rose wa kuwapenda wanaume wa tabaka la juu kushiriki ngono na binti huyu na kisha baadaye kumwacha .

Mwandishi anasema kwamba kijana huyu alisema mambo mengi. Kati ya yale aliyosema ni kuwa, atakuwa mkuu wa wilaya baada ya kumaliza masomo yake ya chuo kikuu. Anapona kuwa amemteka mbakunja msichana huyu anaamua kutumia uwongo wake ili atimize ashiki yake ya kimwili. Anamdanganya Rose:

“Napanga kwenda Serengeti wiki ijayo. Nimekuja kutaka idhini ndiyo nimpe baba makadirio ili anipe pesa.” (uk.97).

Baada ya kushiriki mapenzi na Rose anamtoroka. Hakuna mahali popote walipoenda. Hali hii inamsikitisha sana binti huyu. Rose aliishia kumchukia kijana huyu kutokana na udanganyifu wake.

Ingawa vijana wa jinsia zote wanajitambuza na kutambulishwa kama wapenzi, inabainika wazi kuwa swala hili la mapenzi linapelekea kudhulumiwa kwa wanawake na jinsia ya kiume. Farida na Rose ambao ni viwakilishi vya jamii pana ya Kiafrika wanatumiwa na wanaume kama vile Kim na Mzee wa *Volvo* kama vyombo vya kutosheleza uchu wao wa kimapenzi. Baadhi ya wanaume baada ya kutosheleza ashiki zao za kimapenzi wanawatoroka wanawake kama tulivyoona hapo juu.

Aidha, mwandishi ameonyesha uhusiano wa vijana na dini. Vijana wana utambulisho wa unafiki katika dini. Baadhi yao wanatambulishwa kama watu wanaotenda vitendo vya kiuhayawani kama vile kuwa katika mstari wa mbele kanisani. Kule kanisani wanaomba na kuongoza nyimbo. Rose anajitambuza kama mtu mwenye unafiki katika dini. Yeye ameshiriki mauaji kwa uavyaji wa mimba nne. Hata hivyo, ndiye anayeongoza

Rose ambaye ni kielelezo cha vijana katika jamii inatumiwa na mwandishi kuonyesha jinsi dini inavyompa mwanamke nafasi hasi katika jamii. Dini hapa inamsawiri mwanamke kama mtu

mnafikiri na anayetafuta hifadhi katika dini. Bila shaka huu ni udhalimu wa kidini kwa mwanamke.

Isitoshe, vijana wanajitambuza na kutambulishwa kama watu wanaojishughulisha na maswala ya ndoa. Ndoa ni asasi ya kitamaduni inayopelekea kudhulumwa kwa mwanamke katika jamii kwa kisingizio kuwa mwanamke anapoolewa huwa ni mali ya mumewe. Ni kutokana na imani hii ambapo wanaume huwanyanyasa na kuwadhulumu wake zao kote barani. Ingawa jamii nyingi zinaamini hivi, vijana katika jumuiya ya *Maisha Kitendawili* wana utambulisho tofauti.

Baadhi ya vijana wa kike katika riwaya hii wanachukulia kwamba ndoa ni njia ya kujipatia raslimali maishani. Wanachukulia kwamba ndoa ni ya kuwategemea wanaume kwa mahitaji yao huku fedha zao wakizitia kibindoni. Farida anaamini kuwa ndoa inafaa kumfaidi mwanamke ambaye anapata usaidizi wa kifedha kutoka kwake.

Kuhusu mwanamke wa kumuoa Juma anajitambuza kama mtu asiyezingatia urembo wa mwanamke anayetaka kufunga ndoa naye tofauti na jinsi wanaume wengi wanavyochukulia katika jamii. Anachotilia maanani ni maadili ya mwanamke, lakini si swala la urembo wake. Anapendezwa na mwanamke mwenye kuwaheshimu watu wengine, mwenye shukrani n.k.

Kijana huyu pia anataka mwanamke anayemuoa awe na utambulisho wa mtu msamehevu, mhimili, awe mtu wa kujitolea na kutofikiria mumewe ni baba. Farida anapomchimba Juma amfahamishe mke mwema wa kuolewa ni yupi, Juma anasema:

“Aaa! Pia aweze kuwasamehe watu. Yaani ubora wa mwanamke ni katika tabia yake. Awe kitegemeo, yaani, mhimili. Ajitolee na kujituma. Na mwisho asiwe wa kufikiria mumewe ni babake. Yaani ajisimamie.” (uk.166).

Kuongezea ni kuwa, mwandishi ameonyesha jinsi vijana wanavyojitambulisha tofauti tofauti katika kwa mintarafu ya mikhtadha mbalimbali. Wao hubadilikabadilika kwa mujibu wa mikhtadha hii. Neil (1999:2) anaeleza kuwa vijana hukumbwa na utambulisho tofauti tofauti, hasa wakiwa katika mandhari tofauti tofauti kama vile nyumbani, shuleni, miongoni mwao na

kadhalika. Wakiwa katika mandhari haya tofauti wanaweza kukumbwa na utambulisho wa muda husika, wa makundi yao na pia wa kiumri. Wakiwa shuleni vijana hawa wanaweza kujitambuza kama wapenzi, wakifika nyumbani wakajitambuza kama watiifu au katili kwa wazazi wao na kadhalika.

Mwandishi anaitambulisha jinsi vijana wanakumbwa na mabadiliko katika maisha yao. Baadhi ya nyakati wakiwa vijijini wanakuwa ni washamba wasioelewa maisha ya mjini au ya vyuo vikuu. Wanaweza kuwa hawazingatii viwango vya juu vya usafi. Farida akiwa kijijini mashambani anakuwa mtu ambaye hazingatii usafi lakini anapojiunga na chuo kikuu anakumbwa na mabadiliko makubwa kuhusu kujipamba na usafi wake. Akiwa kijijini nywele zake hazishughukii, lakini anapojiunga na chuo kikuu anaanza kuzitunza.

Kule nyumbani alikuwa pia akilalia jamvi lililoliwa na mchwa. Mwandishi anafafanua kuwa, jamvi hili lilitandikwa magunia na maleso yaliyozeeka. Hili ni dhihirisho wazi kua familia ya akina Farida ilikuwa na umaskini ambao haungeiwezesha kupata mahitaji ya kimsingi kama vile malazi bora.

Anapofika chuo kikuu mambo yanakuwa tofauti kabisa. Anabadilika kabisa. Sasa anajua kutia nywele urembo, anavalia viatu vya thamani na vya aina tofauti tofauti. Pia ana nguo chungu nzima ambazo anazibadilisha anavyotaka. Kwa hakika anakumbwa na mabadiliko mengi baada ya kujiunga na elimu ya juu.

Mwingine mwenye kitambulisho cha mabadiliko ni Angela. Mwanzoni Angela aliwa na hulka nzuri. Alikuwa mcheshi na mwenye furaha, mkarimu, mwenye ukarimu n.k. Baadaye anabadilika na kukosa baadhi ya sifa hizi. Mathalan, ukarimu wake unianza kutoweka polepole. Tunaona kuwa fedha anazomruzukia Farida zikipungua kutokana na tabia hii.

Kutokana na maelezo haya tunaona kuwa, elimu haimpi mwanamke nafasi ya kuyadumisha matakwa ya kijamii na ya kitamaduni ya jamii za Kiafrika. Wahusika tuliowatolea maelezo hapa juu na ambao ni viwakilishi wa vijana wa kike jamiini wanaonyesha jinsi elimu inavyomtoa

mwanamke katika hali yake halisi na kumwingiza katika hali nyingine tofauti ya kijamii na kitamaduni. Baadhi yao hukosa maadili ya jamii yao.

Pia, tunaona kuwa ijana hujitambuza na kutambulishwa kama watu wanaoendeleza migomo na maandamano shuleni, hasa katika shule za sekondari na vyuo vikuu. Mara kwa mara huwa wanaleta maangamizi ya mali kunapotokea migomo hii. Baadhi ya nyakati huwa wanagoma au kuandamana wakilalamikia uongozi mbaya, sheria kali dhidi yao, kutoshughulikiwa kwa matakwa yao na kadhalika.

Kim anawatambulisha vijana wa vyuo vikuu kama watu wanaoshiriki katika migomo na kuleta maangamizi ya mali. Mwanaume huyu anapotaka kujua kutoka kwa Farida ni kwa nini huwa wanagoma, anamweleza kwamba kuna migomo ya vyuo vikuu siku hizi lakini si mingi kama zamani. Kim anapotaka kujua ni kwa nini wanafunzi wa vyuo vikuu hugoma, anamfahamisha kuwa, wanafunzi huwa wanauliza maswala yanayosibu jamii kisha wakaambiwa kwamba wanagoma. Kulingana na msichana huyu jamii ndiyo husababisha migomo kwani isingefanya inavyofanya wanafunzi hawangeshiriki migomo. Naye Kim anashangaa ni kwa nini wanafunzi hawa husababisha uharibifu wa mali ya watu ambao baadhi yao ni maskini na ndio hulipa kodi inayoendeleza vyuo vikuu (uk.15).

Kadhalika, vijana wanaajitambuza kama watu wanaotilia maswala ya urembo maanani. Baadhi ya vijana wa kike wanajirembesha ili kuwavutia wanaume. Jinsia ya kike anachukuliwa na jamii kama pambo la kumfurahisha mwanaume. Maina (2005:76) anaeleza kwamba wanawake wanatumiwa katika kuwapanga watu katika sherehe wanaume wakiwa ni baadhi ya watu wanaopambwa kwa maua katika sherehe hizo. Hata baadhi ya majina wanayopewa wanawake baada ya kubatizwa yanahusishwa na mapambo kama vile Rose, Veronica, Alice na kadhalika. Farida anairembesha nyumba yake ili amvutie Kim. Vidole vyake anavirembesha kwa rangi. Masikio yake anayachomeka vipuli, huku akipeta pete vidoleni. Ili kudumisha urembo wake ana viatu vya kila aina anavyovivaa na nguo anazobadilisha mara nne kwa siku. Kando na mavazi tofauti tofauti, Farida anajitambuza kama mtu anayejirembesha kwa kujikondesha. Anajifinya

kiuno kila jioni na kukimbia kuzunguka uwanja wa mpira ili kupunguza uzani wake. Kando na kutumia ndimu anaenda Sariti kubanwa na mayaya na kumfanyiza maoezi kabambe.

Mwanamke mwingine ambaye anajitambuza kama mpenda urembo ni Rose. Rose anajirembesha kwa kutengenezwa nywele na mwanamke Mhindi. Ili kudumisha urembo huu inafikia kiwango cha kumlipa mwanamke huyu zaidi ya shilingi elfu moja kwa huduma ya ususi anayompa. Kadhalika, mwanamke huyu anadumisha urembo wake kwa kuvalia nguo tofauti tofauti. Kabati lake lina nguo nyingi.

Mwandishi Habwe anaipa jinsia ya kike utambulisho wa urembo. Anawaeleza wanawake kama watu warembo kisura na kimapambo. Tunasimuliwa kuwa kando na maiti ya Julia kule ufuoni kulikuwa na mwili wa mwanamke aliyekuwa mrembo.

Ni kutokana na hali hii ya kujirembesha ambapo wanawake wanachukuliwa na wanaume kama mapambo, na kupewa majina ya kulinganishwa na vitu vya urembo kama vile maua. Majina kama vile Waridi na Rose yanatokana na maua. Baadhi yao wanapopewa majina kama haya hufurahia bila kufahamu kwamba wanadunishwa na wanaume kwa kulinganishwa na vitu kama hivyo vilivyo na thamani ya chini vikilinganishwa na binadamu.

Aidha, vijana hasa wa jinsia ya kike wanatambulishwa kama wanaojihusisha na uavyaji wa mimba kwa pakubwa katika jamii mbalimbali za Kiafrika. Utamaduni wa Kiafrika haukuruhusu kamwe uavyaji wa mimba kutokea kamwe jamiini. Lakini leo mambo ni tofauti kabisa, kwani baadhi ya wasichana wanaavya mimba ndipo waendeleo na masomo, wadumu katika baadhi ya kazi ambazo hazimkubali mwanamke kuendelea kufanya kazi huku akiwa mjamzito.

Swala la uavyaji mima si geni kwa jamii nyingi za Kiafrika. Wakazi wengi wa Soweto wanaavya mimba na kuzitupa ovyo ovyo. Kasu anaona jibwa linalobeba pande la nyama ya mtoto aliyekuwa ametupwa.

Kasu anashtuliwa sana na kioja hiki. Hakuamini aliyoyaona ndipo akamkimbilia Yasmin Taabu chumbani na kumweleza aliyoshuhudia. Yasmin huku akijitambuza kama mtu asiyeshangazwa na hali ile anamwambia Kasu kuwa, uavyaji wa mimba ni jambo la kawaida pale Soweto.

Mwandishi anampa Rose utambulisho wa muavyaji wa mimba. Msichana huyu tayari ameringwa mimba nne akiwa chuoni na tayari ameziavya mimba hizi zote. Jambo hili linamfanya kuchukiwa na baadhi ya wavulana aliosoma nao katika chuo kikuu.

Vitendo vya uavyaji wa mimba vinaenda kinyume na utamaduni wa Kiafrika. Visa kama hivi vilikuwa ni nadra sana kupatikana katika jamii za Kiafrika. Rose ni kiwakilishi cha wanawake wanaoenda kinyume na utamaduni huu kama njia ya kujitafutia uhuru kutokana na minyororo ya utamaduni huu. Hata hivyo, yaelekea kuwa hafahamu kwamba katika uavyaji wa mimba hahatarishi maisha ya mtoto, bali anahatarisha maisha yake pia. Vifo vingi vimetokea kutokana na vitendo vya aina hii. Ingekuwa bora zaid kwa kijana huyu kutumia njia za upangaji uzazi kuliko kusababisha vifo kwa watoto wasiokuwa na hatia.

Kuongezea ni kuwa, vijana ushiriki ulevi ambao bila shaka una changamoto nyingi. NACADA (2006:28) inazungumzia kuhusu baadhi ya changamoto zinazotokana na ulevi. Inaeleza kwamba wanawake ambao hutumia pombe na dawa za kulevya wanakumbana na matatizo ya kiafya ambayo nyakati nyingi huwa yanaathiri afya ya mtoto atakayezaliwa. Baadhi ya nyakati watoto hawa huzaliwa wakiwa wadogo. Wanaweza pia kuzaliwa wakiwa na matatizo ya kiakili, nyuso ndogo, pua iliyochongoka, kuwa na sura ya uzee wakiwa wangali wadogo miongoni mwa matatizo mengine.

Mwandishi anawatambulisha vijana wengi kama wanaoshiriki katika ulevi ambao unawaathiri kwa njia moja au nyingine. Farida anapozidiwa na ulevi anaanza kutapika. Wakati huu alikuwa akishiriki ulevi na Kim na Papi katika ukumbi wa Kibokoni. Farida na Papi wanaandamana pamoja baada ya Kim kulewa chakari na kuachwa kule Kibokoni. Farida anahisi ulegevu wa mwili kutokana na ulevi, hasa baada kufika nyumbani kwa Papi usiku. Msichana huyu anapoamka chumbani mwake chuoni siku inayofuatia anajipata akiwa na mnuko mbaya wa

pombe. Pia kingo za mdomo wake anazipata zikiwa na taka anazozitoa kwa vidole vyake viwili. Kadhalika, tumbo lake linakoroma kutokana na kutokula kwa muda mrefu kwa sababu ya ulevi.

Vijana wengine wanaojitambuza kama walevi ni Angela na Moses. Angela wanapofika nyumbani akiwa na rafikiye Moses huku kila mmoja akiwa anaendesha gari lake wakiwa walevi, wanadhihirisha utovu wa nidhamu. Wanapiga kelele huku Moses akiwa amemshika rafikiye. Wanapofika nyumbani kwa Angela na kupiga mlango kama polisi, Angela anaanza kumgombanisha Farida kwa kukwambia kwamba hakutaka kuwafungulia mlango.

Ulevi pia unamfanya Angela amwangukie Moses. Licha ya kwenda kulala huku wakiwa wanachekacheka, Angela na Moses Mtoro wanasikika saa kumi za usiku chumbani huku wakipiga kelele na kutukanana. Hizi ni baadhi ya athari ambazo huletwa na ulevi katika jamii.

Kutokana na tabia ya ulevi ya Angela, Farida anafikiria jinsi msichana huyu alivyojitambuza chuoni walipokuwa wanasoma pamoja. Alikuwa ni mtu mdamisi na mwenye bashasha, lakini tayari alikuwa ameanza kuubadilisha utambulisho wake wa awali. Farida anaona kuwa amejipa utambulisho huu mpya kutokana na kupata gari na kazi.

Swala la wanawake kulewa linaenda kinyume na utamaduni wa Kiafrika. Kwa kiwango kikubwa wanawake wanawake wanakatazwa na jamii kushiriki katika ulevi. Hata hivyo, wanawake kama vile Angela na Farida wanashiriki katika ulevi na wanaume kama njia ya kujitafutia njia kuwa huru kutokana na utamaduni unaomnyima mwanamke uhuru wa kutenda mambo kama wanaume. Hata hivyo, ulevi huu unaishia kuwaingiza katika matatizo kama tulivyoona hapo juu.

Vijana na majukumu ya kinyumbani yanajitokeza pia katika riwaya ya Maisha Kitendawili. Utamaduni wa Kiafrika unamtambulisha mwanamke kama mtu anayejishughulisha na kazi za kinyumbani kama vile kupika, kuwalea watoto n.k. Wanafunzwa majukumu haya na familia zao ambazo ni viwakilishi vya jamii pana.

Vijana wanajitambuza na kutambulishwa na jamii kama watu walio na majukumu tofauti ya kinyumbani. Wanaajibika kuwasaidia wazazi wao baadhi ya shughuli za kinyumbani. Farida anaajibika kupika chakula wakati wazazi wake wanapoenda kwa Mganga Kalulu. Hii ina maana

kuwa mtoto wa jinsia ya kike hufunzwa majukumu ya nyumbani na mamake hata akiwa katika umri mdogo. Kwa kuwa Farida ni mwanamke haikosi kuwa mamake na jamii ndiyo ambayo imemfunza maswala ya upishi ambayo huhusishwa na jinsia hii katika jamii.

Vijana wengine pia wanatambulishwa kama wasioishi na wazazi wao lakini wanatekeleza majukumu ya nyumbani tofauti tofauti. Kasu na Yasmini hawaishi na wazazi wao, lakini wanatekeleza wajibu wa nyumbani unaohusishwa na jinsia ya kike. Wanajipikia pale kwao wanapoishi katika mtaa wa Soweto. Katika jiko lao la nje wanatumia kuni kupikia. Wanapikia kwa kuni kwa kuwa bei ya makaa ni ghali.

Baadhi ya vijana wanapokamilisha masomo yao wanajitambuza kama watu wanaorudi mashambani kuwasaidia wazazi wao. Rose anajitambuza kama mtu wa aina hii baada ya kukamilisha masomo yake ya Chuo Kikuu cha Mzalendo. Kule nyumbani anawasaidia wazazi wake kutekeleza kazi za nyumbani.

Kwa ufupi, maelezo haya yanabainisha kuwa, utamaduni wa Kiafrika unamtambulisha mwanamke kama mtu anayejishughulisha na kazi za kinyumbani kama vile kupika, kuwalea watoto n.k. Wanafunzwa majukumu haya na familia zao ambazo ni viwakilishi vya jamii pana.

Swala la vijana na ukengeushi pia limeshughulikiwa na mwandishi. Ukengeushi ni ile hali ya kutengwa na kubaguliwa na asili na jadi yako na kuakisi sifa, tabia au matendo yanayohusishwa na jamii nyingine aghalabu za Kimagharibi. Vijana wanajitambuza na kutambulishwa kama watu waliosahau utamaduni wao na kuufuata ule wa Kimagharibi, yaani wamekengeuka. Wanauthamini utamaduni wa Wazungu kwa pakubwa kuliko ule wao. Wanataka wafanye mambo kama Wazungu. Farida na Rose wanajitambuza kama watu waliokengeuka. Tabia na mienendo yao inashabihiana kwa pakubwa na ile ya Wazungu.

Farida amekengeuka kiasi kwamba mavazi yake yanafanana kirangi na vitu anavyobeba. Mathalan, mwavuli wake wenye maandishi *Lufthansa* na pochi na mshipi wa saa zinafanana, kwani zote ni za rangi nyekundu. Pia anapoondoka anachukua kisusu chake kilichoandikwa *In* na

kukiweka kusoma *Out* (uk.6). Vitendo hivi vinamtambuza msichana huyu kama mtu aliyekengeuka. Anatumia lugha ya Kiingereza.

Rose naye si tofauti sana na Farida, kwani ana kisu cha barua cha kuacha ujumbe. Pia mlangoni pana maandishi ya kuwaonya watu wanaokuja kwa Rose wasimsumbue. Tunasoma:

Mlangoni pake kuliwekwa kibandiko DON'T DISTURB. Vile vile kulikuwa na kisu cha barua kilicho na maagizo, "Ukiwa na ujumbe tumbukiza humu ndani." (uk.58).

Vitendo kama hivi vinamtambuza Rose kama msichana aliyekengeuka maishani. Katika utamaduni wa Kiafrika mambo kama haya hayakutokea. Wazungu ndio wanaofanya vitendo kama hivi.

Vijana wanaokuja kufanya mahojiano katika kampuni ya *Price House* wanatambuliwa kama watu waliokengeuka. Vitendo wanavyofanya vinadhahirisha wazi kwamba wamekengeuka pakubwa. Namna yao ya kuvalia ina athari za utamaduni wa Kimagharibi. Hao ndio waliokuja na maswala ya uajiri wa kazi, mahojiano na namna ya kuvalia watu wanapotafuta kazi au baada ya kuajiriwa. Vijana hawa wasichana kwa wavulana waliokuja kwa mahojiano wamevalia nadhifu. Wamevalia nguo maridadi kama vile suti, tai, viatu nadhifu na kadhalika. Pia, nywele zao zimetengenezwa kwa mitindo mbalimbali, ili kuwa watu wa kuvutia katika mahojiano haya (uk.109).

3.3 Ujitambuzi na Utambulisho wa Wazee

Mwandishi ameturahisishia mambo katika riwaya hii kwa kutumia jina mzee kwa baadhi ya wahusika dhahirisho wazi kwamba wako chini ya kumbo la umri wa uzeeni. Hii ina maana kwamba, msanii wa kazi hii ya fasihi ametubainishia kiwango cha umri wa wahusika hao. utafiti wetu tutachunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kupitia maswala yafuatayo kwa kugemea umri tuliotaja hapa juu:

Swala la wazee na ndoa pamoja na familia linajitokeza wazi katika riwaya hii. Wazee wengi wanatambuliwa na mwandishi kama wanaokumbwa na changamoto nyingi katika ndoa zao. Wanakumbwa na matatizo katika kutafutia familia zao riziki. Wengi wao ni maskini na hawawezi kushughulikia mahitaji ya familia zao kikamilifu.

Mzee Omar na mkewe Bi Kibibi wanaelekea kushindwa na mahitaji ya familia zao. Watoto hawana vitanda vya kulalia, bali wanalala sakafuni katika mkeka ulioliwa na mchwa ukawa na umbo la ramani ya Afrika. Hata fedha za kumtibia Omar zinakosekana katika familia hii. Inabidi mkewe mzee huyu kufanya juu chini ili kupata fedha za kumpeleka mzee huyu kwa Mganga Kalulu akapate matibabu.

Wazee wengine wanaotambuliwa kama walio na matatizo katika familia zao ni Mama Josii na mumewe. Hawa wawili wana watoto wengi ambao Kasu anasema kwamba wanakaribia idadi ya kutoshea timu ya kandanda. Hii ina maana kuwa idadi ya watoto hawa ni kubwa. Wazazi hawa wanapata matatizo katika kuwalea watoto wao. Anayewashughulikia watoto hawa ni Mama Josii ambaye ana kibiashara kidogo katika Soko Mtumba, kwani mumewe anaugua; hivyo basi, kushindwa kuwalea wanawe. Kinyume na utamaduni wa Kiafrika ndiye ameachiwa majukumu ya kuilea familia. Mumewe hana uwezo wa kushughulikia matakwa yao yanayoelekea kuwa mengi kutokana na familia yake kubwa.

Wazee wengine ambao wanatambuliwa kama watu wanaokumbwa na matatizo katika familia zao, hasa ya kuwalea watoto wao ni wazazi wake Rose. Baba yake Rose hana mkono jambo linalomfanya kushindwa kuitafutia familia yake riziki.

Maelezo haya yanabainisha kwamba jinsia ya kiume ambayo inawakilishwa na wanaume tuliowataja hapo juu imeshindwa kutekeleza majukumu inayopewa na utamaduni na jamii yake. Badala yake wake kama vile Kibibi, Mama Josii miongoni mwa wengine ndio wanaotekeleza majukumu ya wanaume jambo ambalo ni kinyume na utamaduni wa Kiafrika.

Aidha, Wazee wengi wanatambulishwa na mwandishi kama wanaozisaliti ndoa zao kwa kushiriki mapenzi nje ya ndoa na kutumia raslimali za jamii katika njia za kutilia shaka. Kim

anajitambuza kama mtu aliyesaliti ndoa yake kwa kuwa rafiki yake Farida. Anamnunulia msichana huyu nguo za mitindo tofauti tofauti, viatu, vyakula miongoni mwa vitu vingine. Mwanamume huyu hamshughulikii mkewe kwa sasa kwani fedha za matumizi ya familia zimeelekezwa kwa binti huyu. Mkewe Kim ana watoto, lakini mumewe hashughulikii matakwa yao kama vile kuwanunulia nguo. Mzee mwingine anayetambuliwa kama aliyeisaliti ndoa yake ni rafikiye Rose. Mzee huyu wa *Volvo* ameanzisha urafiki wa kukata na shoka na msichana huyu wa Chuo Kikuu cha Mzalendo. Mahitaji ya Rose yanashughulikiwa na mwanamume huyu. Anamnunulia nguo, anampa fedha za kwenda kusukwa, anamnunulia vileo klabuni, anampa fedha za kwenda nyumbani kwa wazazi wake ambazo ni shilingi mia nane na kadhalika.

Kadhalika, Mwandishi anazitambulisha njia zote mbili kama zinazokumbana na changamoto katika malezi ya watoto, hasa ndoa ikiwa changa. Farida na Juma ambao ndoa yao ni changa hawatambui ni nini kinachomfanya mtoto wao, Faki, alie. Wanashirikiana katika kumtuliza mtoto huyu. Kinachodhihirika hapa ni kwamba, malezi huwahitaji wazazi wa jinsia zote mbili, bali si mzazi mmoja. Juma amekubali kumsaidia Farida kulea mtoto, kwani yeye anafahamu kwamba ni lazima watoto wawasumbue wazazi wao. Juma mwenyewe anasema, “Uzazi ngoma, hivi ndivyo tulivyosumbua. Basi nasikitika!” (uk.168). Hapa mwanamume huyu anajitambuza kama mtu anayefahamu changamoto wanazokumbana nazo wazazi katika kuwalea watoto wao.

Kinachobainika hapa ni kuwa, Juma anaenda kinyume na utamaduni na jamii za Kiafrika ambazo zinatarajia majukumu ya kuwalea watoto yaachiwe jinsia ya kike. Inachopiga vita hapa ni desturi na imani za Kiafrika kwamba kuna majukumu yanayotengewa jinsia maalum katika jamii.

Baadhi ya wazee wanatambuliwa na mwandishi kama watu wasiopanga uzazi. Wana watoto wengi. Mama Josii na mumewe wanatambuzwa kama wazazi walio na watoto kumi na mmoja. Watoto hawa wanaishi kwa dhiki kwani wanalala sakafuni kutokana na hali ngumu ya kimaisha inayowakumba wazazi wao. Hawana vitanda.

Wazazi hawa wanaenda kinyume na upiganiaji wa haki za wanawake ambapo wanataka swala la upangaji uzazi lipewe kipaumbele katika jamii. Wangukuwa na watoto wachache huenda hawangukumbana na matatizo kama yale wanayokumbana nayo sasa.

Isitoshe, swala la wazee na ushiriki wao katika siasa na uongozi umeshughulikiwa katika riwaya hii. Wazee wanajitambuzia kama watu wanaoelewa siasa za Afrika na ulimwengu wote kwa jumla. Baadhi ya wazee waliwahi kuwa viongozi katika bara hili ambapo walishikilia nyadhifa tofauti tofauti za kisiasa. Katika *Maisha Kitendawili* tunaelezwa kuwa, Jomo Kenyatta, Biko, Nkrumah miongoni mwa wengine waliwahi kuwa marais wa nchi za Afrika.

Mara nyingi jamii huwatambua wazee kama viongozi katika jamii. Mara nyingi wazee ndio huchaguliwa kuwaongoza wanajamii katika nyadhifa tofauti za kisiasa. Ingawa baadhi ya vijana huchaguliwa katika nyadhifa hizi, idadi yao huwa ni ya chini sana wakilinganishwa na wazee. Ingawa tunasema idadi kubwa huwa ni ya wazee katika uongozi wa kisiasa jinsia ya kiume ndiyo huwa kubwa kushinda ile ya kike katika nyadhifa hizi.

Katika baadhi ya jamii wakati wa kupiga kura kuwachagua viongozi unapowadia vijana wanaowania nyadhifa tofauti huwa wanapuuzwa huku wazee wakipendelewa kwa imani kuwa wazee wana busara kuwashinda vijana. Na panaposimama kijana wa kike achaguliwe ndipo mambo yanapokuwa mabaya zaidi, kwani baadhi ya jamii humtambua mwanamke kama mtu wa kuongozwa bali si wa kuongoza wengine.

Kuongezea ni kuwa, wazee wanajitambuzia kama watu wanaoamini dini katika jamii za Kiafrika. Dini imekuwa ikitawala maisha yao. Kunapotokea matatizo wanakimbilia suluhisho katika dini. Kunapotokea vikwazo vya kiuchumi na kijamii wanatafuta uhafadhi katika asasi hii.

Viongozi wa kidini ni watu walio na utambulisho wa unafiki katika kutekeleza majukumu yao. Viongozi hawa wanatarajiwa na jamii kuwa watu wenye maadili na ambao hawashiriki uasherati na washiriki wao kanisani au wanawake wowote wale katika jamii. Ken anaposhindwa kumfahamu baba ni nani anafuatilia na kupata kufahamu baadaye kwamba ni Baba Joseph.

Mwanzoni anashiriki katika maombi ndipo hatimaye akakuja kugundua kwamba huyu ndiye babake kupitia maelezo ya mamake anayempata akiwa amepiga magoti akiomba.

Maelezo haya yanaonyesha jinsi viongozi wa dini wanavyoitumia dini kuidhulumu jinsia ya kike. Kasisi Joseph anatumia mamlaka yake ya kidini kumdhulumu mamake Ken kimapenzi jambo linalopelekea kuzaliwa kwa mtoto huyu. Anapozaliwa hataki kujitambuza kama babake mvulana huyu bali anamweka katika hali ya taharuki kwa muda mrefu.

Jambo lingine ni kwamba, wazee wa jinsia zote wana utambulisho wa kushiriki katika ushirikina. Mzee Omar na mkewe Kibibi wana imani za kishirikina. Wanapoenda hospitalini kupata matibabu ya Omar na kuona kuwa hawajaridhika wanamua kwenda kwa Mganga Kalulu. Wanapoingia nyumbani kwa Kalulu kwa kupiga magoti na kusota nayo hadi ndani wanajionea maajabu ya kila aina. Mwandishi anamtambulisha mwanamume huyu kama mtu aliye na vitu tofauti vya shughuli za uganga. Mganga huyu ana chupa za aina tofauti, vibuyu, fuu la kichwa cha mtu n.k.

Kalulu anajitambuza kama mfuata utaratibu katika kuendeleza miviga ya uganga ambayo inafanyiwa baadhi ya watu wanaomtembelea nyumbani kwake. Anamwagiza Kibibi kushiriki katika miviga hii kwa kutia shilingi katika kibuyu. Baada ya mwanamke huyu kukichekesha kibuyu hiki kinaanza kuongea. Kutokana na miviga hii Mganga Kalulu anamfahamisha Omar kwamba ametumiwa mashetani ya aina ya talo na mogo ambayo husababisha kifo yasipotibiwa.

Kalulu ambaye ana utambulisho wa kiganga anaamini kuwa ushirikina ndio utakaomzalia mali. Anayahusisha maradhi ya Mzee Omar na miungu kisha anaitisha malipo ya kiwango cha juu ikizingatiwa kwamba familia hii ni maskini. Mganga huyu anataka kupewa korosho gunia moja, mchele madebe mawili ili amtibu mzee huyu. Kalulu anaongezea kusema kuwa, matambiko ya uganga yanahitaji damu ya mnyama au mtu ndipo Mzee Omar aweze kutibiwa maradhi yake na kupona.

Baada ya kurudi nyumbani kutoka kwa mganga Omar anarudiwa na yale mashetani. Yaelekea mashetani yanayomjia Omar huja wakati wa jioni wala si asubuhi, aduhuri au alasiri.

Mwandishi anasimulia jinsi mzee huyu anavyokuwa mwenye hali nzuri mchana kabla ya kuingiliwa na mashetani jioni. Tunasoma: Mchana, mzee alijiona ana nguvu akapata kutembea mtaani Sokomoko na kusalimiana na jamaa na kuwajulia hali. Aliogopa magharibi ilipozenea maanake alijua wakati wa kupambana nayo mashetani ndio huo (uk.38).

Mwandishi anamtambulisha Kalulu kama mtu mwenye majigambo, vitendo vya sarakasi na uwezo wa kuponya maradhi kwa njia za kiganga. Anajisifu kwamba yeye ni Fundi-Kombo Mimi mwelea majini; huku akirusharusha nafaka kila upande katika nyumba yake.

Licha ya Kalulu kufanya mazingaombwe yake mwandishi anamtambulisha kama aliyeshindwa kabisa kuponya maradhi ya Omar. Hii ni kwa sababu baada ya mzee huyu kupata matibabu haya na kupata nafuu kwa muda mfupi hatimaye anaishishia kuaga dunia. Kibibi baada ya kukumbwa na huzuni wa kuachwa na mumewe naye mwishowe anaupungia ulimwengu mkono wa buriani.

Kando na Omar, Kibibi na Kalulu kujitambuza kama watu wenye imani katika ushirikina, jamii kwa jumla inajitambuza kama iliyo na imani katika itikadi hii. Mzee Zinzi ambaye ni kiwakilishi cha jamii anaamini katika desturi hii. Mzee huyu ambaye alikuwa haogi anasema kuwa Omar na mkewe wamefanyiwa madawa. Anamaanisha kuwa wamerogwa ndipo wakaaga dunia.

Swala la wazee na uwazi katika mawasiliano pia limeshughulikiwa na riwaya hii. Tofauti na jinsi ilivyokuwa katika utamaduni wa Kiafrika ambapo jinsia ya kiume ndiyo iliyotoa maamuzi au iliyodhibiti mawasiliano katika familia, wanawake wengi sasa wana uhuru wa kuwasiliana na wanaume zao bila pingamizi zozote. Yaelekea utamaduni wa Kiafrika umelekeza kamba kiasi kutokana na elimu wanayopata wanajamii, mchanganyiko wa utamaduni wa Kiafrika na tamaduni nyingine kutoka pembe zote za dunia. Farida anajitambuza kama mtu anayewasiliana na mumewe bila wasiwasi wowote tofauti na ilivyokuwa kwa wanawake wengi ambao walidhibitiwa na utamaduni kiasi kwamba wajibu wao ulikuwa ni kusikiliza na kupokea yote wanayoambiwa na waume zao bila kutoa mchango wowote. Kasu ni mwingine anayewasiliana na mumewe bila matatizo. Haongopi kumwambia yaliyo moyoni. Anataka kumfahamisha kuwa wanafaa kuwa na watoto wawili ndipo washughulikie matakwa yao kama vile elimu bila changamoto nyingi.

Aidha, swala la wazee na anasa pamoja na starehe zinazohusisha ulevi linajitokeza katika riwaya. Barbara (1993:10) anaeleza kuwa ni jambo la kawaida kwa wanaume kubakisha sehemu ya mapato au mshahara wanaopata kwa matumizi yao ya burudani huku wanawake wakitumia sehemu yao kubwa ya mapato au mshahara wao kwa kununua vitu vya kutumiwa nyumbani na ambavyo huwafaidi watu wote pale nyumbani. Anatoa mfano wa uchunguzi uliofanywa Misri kuwahusu wafanyakazi waliopata mapato ya chini na ambao wakati familia ilipoinuka kiasi kimapato, wanawake wengi walijihusisha na ununuzi wa mashini za kuosha nguo na gesi ya kupikia; ambapo wanaume walitumia mapato yao kwa maswala ya kujiburudisha ambayo hayakushughulikia kamwe mambo ya nyumbani. Kwa mfano, kwenda katika sinema. Na kama wanaume walijihusisha na ununuzi wa vitu vya nyumbani, walinunua runinga au redio kaseti.

Swala la kununua bidhaa za nyumbani linafaa kushughulikiwa kikamilifu na jinsia zote mbili. Kwa kuwa mapato ya wanaume mara nyingi huwa yanaishia katika burudani na kushindwa kushughulikia ununuzi wa baadhi ya vifaa vya nyumbani, hili ni swala ambalo linafaa kushughulikiwa na wanaojihusisha na maswala ya wanawake na ukosefu wa usawa wa jinsia. Kushughulikia maswala ya kijinsia kutapeleke kuwako kwa uwelewano wa kina kuhusu mapato na matumizi yake kwa wale wanaohusika.

Wengi wa wanaume hutumia raslimali zao katika ulevi ambao huathiri maisha yao kwa njia moja au nyingine. Badala ya Kim kushughulikia familia yake kama jamii inavyomhitaji afanye, anamshughulikia mpenziwe Farida. Wanaenda kulewa na kustarehe katika kumbi kama vile Kibokoni. Ulevi huu unamwathiri Kim sana. Anapolewa kule ukumbini anajipata katika hali mbaya sana. Anatoka nje na kulala nyasini. Kule nyasini koti lake linaliwa na mchwa. Ulevi huu unamfanya macho yake kuwa mekundu, mashavu yake yana uyabisi na udenda n.k.

Kim anamwambia Farida kwamba ulevi ulimfanya alale nyasini ambako alipigwa na umande na upepo mkali mpaka asubuhi. Hili ni dhihirisho kwamba raha na starehe huwa na athari zake, hasa zinapohusisha dawa za kulevya na pombe.

Kadhalika, wazee wa jinsia ya kiume wana utambulisho wa ufujaji wa fedha na raslimali nyingine katika jamii. Farida katika hadithi yake ya *Baba Ndiye Baba* iliyomo katika *Maisha Kitendawili* anaonyesha jinsi jinsia hii inavyofuja mali. Babake Ken anafuja fedha zake kwa levi na uchezaji kamari akiwa nchini Tanzania. Hatimaye anarudi nyumbani akiwa fukara.

Mwanamume huyu ambaye ni kiwakilishi cha wanaume wa Kiafrika anaenda kinyume na utamaduni wa jamii yake ambao unamhitaji kutunza raslimali za familia yake. Yeye kama mhifadhi wa utamaduni huu inafaa kutumia fedha zake kwa kuifaidi jamaa yake, bali si maswala yasiyo na manufaa kwa watu wake.

3.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kiumri. Sura yenyewe tuliigawa katika sehemu tatu zenye makundi matatu ya wanajamii kwa mintarafu ya umri ambayo ni watoto, vijana na wazee.

Katika utafiti wetu tumeona kuwa, watoto hujitambuzi na kutambulishwa kwa namna tofauti na jamii. Katika kujitambuzi kwao tumeona kwamba, wanajishughulisha na maswala kama vile michezo. Pia tumepata kwamba wakiwa wadogo sana huwa hawajitambuzi na jinsia yoyote tofauti na umri wao unapoiarika na kuweza kujitambuzi na jinsia tofauti katika jamii. Pamoja na hayo watoto hukumbwa na changamoto mbalimbali kama vile kufanyizwa kazi za sulubu, kukosa malezi mwafaka miongoni mwa changamoto nyingine. Ingawa wanakumbwa na matatizo haya tumeona kuwa, baadhi ya wanajamii huwa wanawapa watoto malezi mwafaka. Kuhusu elimu tumetambua kwamba wanajamii wengi wana mwelekeo hasi kuhusu elimu ya mtoto wa kike kwani wanaithamini elimu ya mtoto wa kiume. Hata hivyo, kuna wale wanaothamini elimu ya jinsia zote mbili.

Tukija kwa ujitambuzi na utambulisho wa vijana tumeona kuwa, vijana wanapata elimu ya maisha kutoka kwa jamii. Kuhusu elimu inayopatikana shuleni tumebainisha kwamba, elimu ya msichana huwa ni chini ikilinganishwa na ile ya mvulana. Pia tumetambua kwamba, wasichana huacha shule mara kwa mara kutokana na vikwazo vya kitamaduni kama vile ndoa za mapema na za kulazimishwa. Pia tumeona vijana kama watu wanaokumbana na matatizo mengi katika

jamii kama vile ukosefu wa kazi, kutohusishwa kikamilifu katika siasa, kutorokwa na wapenzi wao miongoni mwa mengine. Ingawa wanakumbwa na matatizo haya baadhi yao ni wavumilivu maishani.

Ujitambuzi na utambulisho mwingine ambao tumeutolea maelezo katika sura hii ni ule wa wazee. Hawa wamejitambuza na kutambulishwa kwa njia tofauti tofauti. Wengi wao ni watu wanaokumbana na matatizo katika ndoa, uzazi na ulezi na kadhalika. Pia wanatambulishwa kama washirikina, watu wanaoshiriki mapenzi nje ya ndoa miongoni mwa utambulisho mwingine.

SURA YA NNE

UJITAMBUZI NA UTAMBULISHO WA KIJINSIA KATIKA KUPIGANIA UKOMBOZI

4.0 Utangulizi

Katika sura hii tutajadili ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika harakati za kupigania ukombozi wa kijinsia. Ni sura ambayo inachambua na kuchanganua mahusiano na mwingiliano wa kijinsia katika kuleta ukombozi wa kijinsia, hasa ile ya kike ambayo imedhulumiwa na kukandamizwa kwa muda mrefu kutokana na ubabedume, utamaduni, siasa miongoni mwa maswala mengine katika jamii. Kuna haja ya kupatikana kwa ukombozi wa kijinsia katika jamii. Hata baadhi ya katiba barani Afrika zinatambua umuhimu wa kuwapo na ukombozi wa kijinsia katika jamii. Katiba ya Kenya ya 2010 (uk.24) imeshughulikia swala la usawa wa kijinsia katika jamii. Inaeleza kwamba, wanawake na wanaume wana haki sawa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kidini na kijamii. Katiba hii pia inapinga dhuluma za kijinsia zinazoweza kutokana na misingi ya kirangi, kiuana, kidini, kiafya, kitamaduni, kikabila, kijamii miongoni mwa misingi mengine ya udhalimu.

Kuhusu kupatikana kwa ukombozi huu kumekuwa na makongamano tofauti tofauti yanayoshughulikia ukombozi wa jinsia, hasa ile ya kike ambayo imegandamizwa na ile ya kiume kwa muda mrefu. Kuhusu hali hii Mirikau (2011:19) akimrejelea Nzomo (1997) katika kazi yake ya *Empowering Kenyan Women* (Kongamano lililoandaliwa tarehe 20 Februari 1993 katika Hotel ya Milimani) anaeleza jinsi wanawake walivyojitokeza kwa uthabiti ili sauti zao zisikike. Wanawake hawa walipigania kuhusishwa kidemokrasia ili ajenda yao iwe sawa na ya wanaume. Walijadili kushirikishwa kwao katika urithi wa mali na kazi zao kuacha kuchukuliwa kama za nyumbani na ukulima mdogo, utoaji wa bidhaa za kuuzwa, uwekaji wa akaunti za wanaume wao.

Mirikau anasema pia kuwa katika kongamano lingine la Amani na Maendeleo Jijini Nairobi tarehe 15 – 16 Julai 1985 kupitia kipengele 40/08 cha Desemba 13 ilipitishwa kuwa: kuwe na usawa kuhusu kuamua mambo kuhusu ngono, kutupiliwa mbali kwa aina zote za ubaguzi, usawa na haki kuhusu talaka uzingatiwe, uanzishaji wa kitengo cha kuchunguza na kutekeleza maswala yanayohusu usawa. Pia kongamano hili lilishughulikia uhuru wa wanawake na uwezo wa kununua na kuuza mali, mashamba na kadhalika uzingatiwe, kutambua kazi za mwanamke

zisizolipiwa kama zile za nyumbani kuwa ni muhimu na huchangia maendeleo kisha wanawake wastawishe nafasi zao kielimu na kuzingatia afya na uzazi. Katika utafiti huu tutajadili jinsi jamii inavyopigania ukombozi wa kijinsia kupitia maswala tofauti tofauti.

4.1 Ukombozi wa Kijinsia Katika Siasa

Swala la ukombozi wa kijinsia katika siasa halikuanza hivi karibuni, bali lilianza zamani. Limechukua muda kufikia sasa. Mirikau (2011) katika utafiti wake anaeleza kwamba, jitihada za kutaka usawa kati ya wanaume zilikuwapo nchini Ufaransa wakati wa mageuzi maarufu mwaka wa 1789 – 1795 yaliyopatiwa *Msimbo wa Napoleon (Code Napoleon)*. Wanawake waliandamana kote nchini kupinga Napoleon dhidi ya madai yake kuwa wanawake walikuwa na akili dhaifu wakilinganishwa na wanaume, hivyo walistahili kupewa elimu ya chini na kufanya kazi za chini kama vile ushonaji. Pia, kule Marekani mambo yalikuwa vivyo, kwani wanawake wa huko walijitambuza kama wapiganiaji ukombozi. Wanawake Abigail na Mercy Otis Warren kule Marekani ya Kaskazini waliitisha Marais George Washington na Thomas Jefferson kuongoza ukombozi wa wanawake kupitia kipengele katika katiba ya nchi yao ingawa hawakufaulu. Bila shaka tunaona kwamba huu ulikuwa ni mwanzo mwema wa upiganiaji wa ukombozi wa kijinsia katika jamii.

Tukija katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* mambo si tofauti sana na yale ya kule nchini Ufaransa na Marekani. Farida ambaye ni kiwakilishi cha wanawake katika jamii baada ya kukamilisha elimu ya chuo kikuu tunamwona akizungumza wazi wazi kuhusu maswala ya kisiasa kuliko alivyokuwa hapo awali. Inaikosoa serikali bila woga. Msichana huyu anaomweleza Manoti jinsi serikali inavyoshindwa kuwaajiri vijana waliokamilisha masomo yao ya chuo kikuu. Kutokana na maelezo yake ni wazi kwamba mwanamke huyu anaishambulia serikali kwa kushindwa kutimiza ahadi zake kwa vijana wanaohitimu kutoka vyuoni. Licha ya rais wa nchi kutotoa hakikisho katika sherehe za mahafala za akina Farida kwamba, vijana hao wangeajiriwa; msichana huyu na wenzake wengi bado hawajapata ajira mpaka sasa. Hali hii ndiyo inayomfanya Farida kuikemea serikali kwa kushindwa kuendeleza nchi kwa kushindwa kuwaajiri vijana kama wao.

4.2 Ukombozi wa Kijinsia Katika Dini

Jinsia ya kike inajitambua kama inayotaka ukombozi wa kidini, kwani dini inaendeleza dhuluma dhidi ya jinsia hii. Ni kutokana na hali hii ambapo wanawake wanapigania kuwako wa ukombozi wa kidini ambapo mwanamke hatakuwa hakidhulumiwa nayo. Mwandishi anamtambua Farida kama mtu asiyetilia maanani maswala ya kidini baada ya kuona unafiki ulioko katika taasisi hii inayopatikana katika jamii mbalimbali kote duniani. Mwandishi anasema kuwa, banati huyu inaiona dini kama asasi iliyo na udhalimu katika jamii. Mwandishi anaeleza jinsi Farida alivyosikia kikundi fulani kikiimba nyimbo ndipo akaenda kukitazama.

Farida akiwa yungali pale, Mhubiri Papi anasimama kuhubiria watu waliokuwa pale. Mwanzoni hamfahamu mhubiri huyu, lakini baada ya kumwuliza dada mmoja anamwambia kuwa, huyo ni Pastor Papi. Mhubiri huyu anamshangaza Farida kwa kuwa na mikono ya chuma. Anaitumia mikono hii kuifungua Biblia. Farida haamini yule jambazi Papi amebadilika na kuwa mhubiri. Farida anashindwa ni vipi mwanamume huyu katili amegeukia dini, hasa kutokana na ukweli kwamba alimuua msichana mmoja na kumshurutisha Farida kuiosha maiti hiyo kwa pamba. Ni kutokana na ukatili huu ambapo Farida yuko tayari kumpokonya Papi mikono hiyo yake ya bandia ya chuma. Ukakamavu huu Farida unaonyesha jinsi mwanamke anavyokabiliana na madhalimu wa kiume katika dini ili kusaka ukombozi wa kidini.

4.3 Ukombozi wa Kijinsia Katika Utamaduni

Utamaduni umechukuliwa kama kikwazo kikuu katika kuhakikisha kwamba wanawake wanafurahia haki zao za kibinadamu na sababu kuu inayofanya jamii kupinga kutekelezwa kwa haki hizi. Utamaduni unabakia pia kuwa kizuizi kikubwa cha haki za wanawake barani Afrika; na pia kuendelea kuwa changamoto kwa wanawake na jamii husika pamoja na serikali na watu binafsi ambao wanapigania haki za wanawake. Kwa hivyo, kuna haja ya kupiga vita utamaduni unaoendeleza udhalimu wa kijinsia katika jamii. Hali hii inaleta ukombozi wa kitamaduni katika jamii.

Mwandishi wa riwaya ya *Maisha Kitendawili* anatambua kuwa ili kuwe na ukombozi katika jinsia zote mbili hazina budi kupigania ndoa ambayo haidhibitiwi na maswala ya kitamaduni yanayomwona mwanamke kama mtu anayefaa kutengewa baadhi ya majukumu ya kutekeleza

katika jamii. Kuna haja ya wanandoa kujitambua wote kama watu muhimu wa kuendeleza ndoa yao bila kumdunisha mmoja wao kwa misingi ya kijinsia. Ndoa ya Farida na Juma inatambuliwa kama ndoa iliyo na mapenzi ya dhati ambapo kila mmoja anachukulia jambo la mwenzake kama lake. Tunasoma: “Jambo la Farida lilimshughulisha Juma zaidi yake na Farida kadhalika. Walijiona marafiki wa kijumla tu. Ni kama mmoja alikuwa nusu ya mwingine.” (uk.175-176).

4.4 Ukombozi wa Kijinsia wa Kiuchumi

Jinsia ya kike inajitambua na pia kupewa utambulisho wa jinsia inayopigania kupata ukombozi wa kiuchumi katika jamii. Hali hii inapunguza utegemezi wao kwa jinsia ya kiume. Wanawake wengi hudhulumiwa sana na wanaume kutokana na ukosefu wa ukombozi wa kiuchumi miongoni mwao. Baadhi ya wanawake katika jamii za Kiafrika wameanza kufanya kazi zinazonuiwa kuwainua kiuchumi. Mama Josii anajitambua kama mfanyabiashara. Ana kibanda cha biashara katika Soko Mtumba. Mwanamke huyu ana bidii sana katika kazi yake.

Pia jinsia ya kike inajitambua kama inayotaka kujikomboa kutoka katika minyororo ya kukandamizwa na wanaume kiuchumi. Hii ndiyo sababu Farida anamwambia Juma kuwa, mwanamke ni yule aliye huru kiuchumi, kwani hatakuwa mtegemezi kwa mumewe.

Mama Josii na Farida si tofauti sana na Lanina katika tamthilia ya *Kilio cha Haki*. Lanina anajitambua kama mpiganiaji wa ukombozi wa kiuchumi. Mhusika huyu akiungwa mkono na baadhi ya wahusika wa jinsia ya kiume walio na utambulisho wa kupigania ukombozi wa kiuchumi anaungana nao katika kuleta mabadiliko katika shamba la Delamon. Ili kupinga udhalimu wa Delamon kazini Lanina anawaunganisha wafanyakazi wote, kwani ni dhahiri kwamba watu hawa wakiwa na umoja wataushinda ukandamizaji na kuleta mapinduzi ya kiuchumi ambayo yatapelekea kuundwa kwa jamii mpya inayozingatia haki kwa wote. Katika kupigania haki hizi Lanina ameungana na Dewe na Musa ambao ni wafanyakazi wenzake. Wahusika hawa wanajitambua kama wenye ujasiri wa hali ya juu katika mapambano, ari ya ukakamavu na kujitolea kufa kupona katika kupigania haki za wenzao wanaozidi kudhulumiwa kila kuchao.

Barbara (1993:50) anatoa maoni kuhusu kuwaimarisha wanawake kimaendeleo. Anasema kama kunatakikana kuwe na maendeleo ya wanawake, inafaa nafasi zaidi za kazi zibuniwe na wanawake kupata nafasi za kwenda mijini kutafuta kazi; bali si kukaa mashambani wakitekeleza kazi za nyumbani. Jinsia ya kike inajitambuza kama mshiriki kamili katika kuimarisha uchumi wa nchi. Kupitia njia hii ni wazi kwamba mwanamke ameanza kujikomboa kiuchumi. mwanamke Farida ana kampuni lake la uchapishaji ambalo lina mitambo ya aina ya *Xerox* kutoka Ujerumani. Katika kampuni hii ana wafanyakazi kumi na wawili: wanaume watano na wanawake saba. Wanaume hawa wanajishughulisha na urekebishaji wa mitambo huku wanawake wakishughulika na michapo ya nakala.

Kwa sasa Farida ana ofisi yake iliyoandikwa “Mkurugenzi.” Watu wengi huja kutafuta kazi hapa. Baadhi yao huipata huku wengine wakiambiwa kuwa hakuna kazi. Mwanamke hapa anatambulishwa kama mchumi.

Benedek, Kisaakye na Oberleitner (2002:36) wanasema kuwa, Mkutano wa Kimataifa kuhusu Haki za Kibinadamu ulipendekeza kwamba wote wanaohusika wanafaa kuhakikisha kuna usawa katika kupata ajira bila kusingatia misingi ya kijinsia (wanaume na wanawake), uhuru wa uchaguzi wa utaalumu pamoja na kuajiriwa, usawa katika kupata ruzuku, kulipwa mshahara na hali za utendakazi. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo imefikia hatua hii. Waandishi hawa wanasema kuwa data iliyoko inaonyesha kwamba, wanawake wengi wanajiunga na ajira kuliko ilivyokuwa hapo awali. Hata hivyo, idadi yao ni ya chini ikilinganishwa na ile ya wanaume. Ajira hii pia haiambatani na uimarishaji wa uboreshaji wa kikazi ambapo wanawake wanakumbana na udhalimu na ubaguzi.

4.5 Ukombozi Kupitia Ushirikiano wa Kijinsia

Ushirikiano wa kijinsia unaweza kuhusisha kuungana kwa wanawake peke yao au pamoja na wanaume kupigania ukombozi wa kijinsia. Hata hivyo, mara nyingi huwa ni wa wanawake. Barbara (1993:49) katika *Women and Economic Policy* anasema kuwa, mara kwa mara wanawake wamekuwa wakikutana kujadiliana kuhusu maisha yao pamoja na matatizo yao.

Katika *Maisha Kitendawili* jinsia ya kike inajitambuza kama inayothamini ushirikiano katika kutatua mizozo au changamoto zinazoikumba maishani. Farida anapokutana na Rose na kutaka kujua anapoishi, Rose anamwambia kwamba anaishi na shangazi yake akitafuta vyakula. Msichana huyu anaishi kwa jamaa huyu wake baada ya kufutwa kazi katika kampuni aliyokuwa ameajiriwa. Anaishi hapa akiwa anatafuta vibarua. Baadhi ya nyakati anavipata na nyakati nyingine akavikosa.

Jinsia ya kike inajitambuza kama inayoshirikiana na ya kiume katika kupigania uhuru wa kijinsia au umenke katika jamii. Farida anakutana na Rose katika mkutano wa utamaduni na ulioshughulikia kitengo cha umenke. Wanawake na wanaume kutoka mawanda haya na yale walifika kusikiliza hotuba himizi na chochezi. Hali hii inadhihirisha kuwa ili kuwe na ukombozi kamili wa kijinsia jinsia zote mbili hazina budi kushirikishwa katika kupigania ukombozi wa kijinsia.

Jinsia ya kike pia anajitambuza kama yenye ushirikiano kupitia kwa kuwapa makazi wanawake wasiokuwa na kwao. Mama Josii anapompata Kasu akiwa amesimama bila kujua aende wapi mjini Singida, anamuua kumchukua ili aende akaishi kwake nyumbani.

4.6 Ukombozi wa Kutoa Maamuzi na Ushauri Katika Jamii

Benedek, Kisaakye na Oberleitner (2002:39) waeleza kuwa shirikisho la kimataifa la kutetea haki za kibinadamu linapendekeza kuwe na usawa baina ya wanawake na wanaume katika kuchagua uraia wao pasipo kuzingatia hali ya kuolewa kwao, kuwapo kwa haki sawa kwa wanawake na wanaume katika kutoa maamuzi kuhusu kuwachagua wachumba, kutamatisha ndoa na kuitisha talaka katika ndoa, uzazi, taaluma, utaifa na umilikaji wa mali.

Farida anajitambuza kama mtu anayefahamu changamoto za ndoa, hivyo basi, kutaka ukombozi katika taasisi hii inayochangia pakubwa unyanyaswaji wa mwanamke. Msichana huyu haoni maana ya ndoa. Anasema kuwa zamani ndoa ilikuwa ya lazima, lakini kwa sasa si ya lazima. Kulingana naye mwanamke anaweza kuishi bila kuolewa.

Utamaduni wa Kiafrika haupendekezi kamwe kuwa na ndoa za kandarasi katika jamii. Hata hivyo, ili kuwe na ukombozi katika ndoa Farida anajitambuza kama mtu anayetaka kuwe na ndoa za mkataba kama ilivyo miongoni mwa baadhi ya wanandoa wa mataifa ya Magharibi. Anamwambia Juma:

“Mimi nitapenda kama ndoa itakuwa kandarasi. Masharti ya kandarasi yawe wazi. Yakiwa wazi masharti kupigana kutafungiwa nje ya mlango. Matusi hakuna. Ile kandarasi iwe ya watu wanaoiona wana mchango sawa.” (uk.166).

Kwingineko riwayani tunaona Farida akimtolea Juma uamuzi kwamba hangetaka kuolewa kwa kuwa hayuko tayari kukabiliana na changamoto za ndoa. Hii ilikuwa ni baada ya Juma kumweleza jinsi anavoshuhudia kisa ambapo wanandoa wawili hawapatani ila wanazua vurugu na mapigano usiku kiasi kwamba wanawakosesha usingizi. Ni kutokana na maelezo haya ambapo, anamtolea uamuzi kwamba hataki kuolewa naye kwa sababu hataki kukumbwa na matatizo kama hayo yanayowakumba wanandoa hao.

Pia mwanamke anajitambuza kama mtu anayesaka ukombozi katika taasisi ya ndoa kupitia talaka. Farida anapomwuliza Rose kama ameolewa, Rose anasema kuwa, tayari ametalikiana na mumewe. Rose anamwambia Farida: “Nilifunga pingu za maisha nikakata tena.” Farida anapotaka kujua sababu iliyopelekea kuvunjika kwa ndoa hii, Rose anasema: “... Mchezo wa wanaume siutaki mimi.” (uk.149).

Mkewe Mzee Marufuku anajitambuza kama aliye na uhuru wa kutoa maoni na maamuzi katika familia yake. Anazungumza na mumewe bila woga wowote tofauti na jinsi utamaduni wa Kiafrika umekuwa ukimchukulia mwanamke katika jamii; kwamba ni mtu anayefaa kuamuliwa mambo na mume katika ndoa. Anamwambia wazi kwama hapendezwi na kuletwa kwa Kasu na Farida kwake nyumbani na Mzee Marufuku.

Wanawake pia wanapata ukombozi kupitia kutoa maamuzi katika jamii bila kuwaogopa wanaume. Rose anajitambuza kama mtu mwenye ujasiri wa kutoa maamuzi bila kuogopa shurutisho za Mzee wake wa *Volvo* anayemlazimisha asiende nyumbani kabla hajapata kazi.

Hata hivyo, Rose anatoa maamuzi kwamba hana budi kwenda nyumba kuwatembelea wazazi wake.

4.7 Ukombozi Kupitia Upangaji Uzazi

Einhorn (1988:24) anasema kuwa, swala moja kati ya yale muhimu yaliyotolewa na Vuguvugu la Ukombozi wa Wanawake katika miaka ya sabini lilikuwa ni wanawake kuwa na haki ya kupata njia za bure za upangaji uzazi pasipo na kuzingatia umri wao au hali yao ya kindoa; na kuwa wangeweza kuavya mimba kisheria bila pingamizi. Mucheke (2000:15) anaeleza kuwa, upangaji uzazi ni mbinu au njia wanandoa huchagua idadi watakayokuwa nayo ya watoto, lini wataanza kuwazaa watoto hawa, kipindi cha wakati baina ya kuzaliwa kwa mtoto na mwingine na wakati wa kuacha kuwazaa watoto. Upangaji uzazi unahusisha matumizi ya mbinu za kisasa na za kikale au za kimila za upangaji uzazi ambapo wanandoa wanapata idadi ya watoto watakaowatosheleza katika mahitaji yao ya kiuchumi, kielimu, kiafya na kadhalika. Pasipo kupanga uzazi itakuwa vigumu kuwajalia watoto mahitaji yao kama vile kuwanunulia nguo, kuwatafutia chakula, kuwatafutia makazi mema ya kuishi miongoni mwa mahitaji mengine. Kwa ufupi, kampeni hii ilihusu haki za wanawake kuamua kama watakuwa na watoto na lini watakuwa nao.

Ni kutokana na ugumu huu wa maisha ambapo Kasu anajitambuza kama mtu anayetaka watoto wawili ndipo wapate nafasi ya kusoma hadi chuo kikuu bila matatizo. Anaamini kuwa mtu akisoma hadi chuo kikuu huwa anafanikiwa maishani. Atakuwa katika nafasi ya kupata kazi nzuri itakayompelekea kuwa na mshahara mkubwa, marupurupu, gari n.k. Ni kutokana na hali hii ambapo mwanamke huyu yuko tayari kumshauri mumewe Mjomba kuhusu umuhimu wa kupata watoto wachache.

Hali ya kujifungua ni mchakato ambao wanaufeministi wengi walihisi kwamba ulikuwa umeondolewa kutoka kwa uthibiti wa wanawake wenyewe. Madaktari hasa wanaume walikuwa wanatoa maamuzi kama mwanamke alifaa kupewa dawa wakati wa kujifungua au kufanyiwa upasuaji wakati wa kuzaa. Mwanamke alikuwa na nafasi finyu sana katika maamuzi yake katika hali kama hii. Wanaufeministi na wanawake wanaoshirikiana kufanya kazi pamoja wamekuwa

katika nafasi ya kufanya mabadiliko mengi katika utendakazi wa hospitalini. Wanatetea haki za mwanamke katika kupata afya ya uzazi.

Mucheke (2000:16) anaeleza kwamba, upangaji uzazi huwa muhimu katika familia. Anafafanua kuwa familia kubwa huwa na mahitaji mengi, hivyo basi, huwa na changamoto katika kuafikia matakwa yao ya kimsingi. Kando na matatizo ya kiuchumi na kijamii, ukosefu wa upangaji wa uzazi huathiri kwa pakubwa afya ya mama na mtoto aliyezaliwa.

Kadhalika, ujauzito na ujifunguaji wa watoto vimebakia kuwa vyanzo vya vifo mengi vya wanawake. Uzuiaji wa ujauzito kwa wanawake ambao wana uwezekano kukumbwa na matatizo ya kiafya wakati wa kujifungua kama wale mama ambao tayari wamejifungua watoto wengi, wanawake wachanga na wale wazee walio na matatizo ya kiafya; upangaji wa uzazi unaokoa maisha yao.

Idara ya Elimu ya Watu Wazima Kenya (1989) inasisitiza umuhimu wa upangaji uzazi katika jamii. Inaeleza kuwa upangaji uzazi unapelekea familia kuwa na chakula cha kutosha, mavazi ya kutosha, mahali pazuri pa kuishi, elimu bora, matibabu mazuri na kadhalika. Idara hii inaeleza kuwa, kuwa na watoto wengi huwa ni changamoto kwa mzazi, kwani wote huwa wanahitaji chakula cha kutosha, mavazi, nyumba, elimu na matibabu (uk.2).

Idara hii inasisitiza kuwa watu wengi wanafikiria kuwa upangaji uzazi ni shughuli ya akina mama tu. Hii si kweli. Kupanga uzazi ni muhimu kwa kila mwanamume na kila mwanamke. Hii ni kwa sababu mtoto anazaliwa baada ya mwanaume na mwanamke kukutana kingono (uk.5).

Idara hii inapendekeza ili kufanikisha hatua ya upangaji uzazi, mafunzo kuhusu upangaji uzazi hayana budi kuanza mapema nyumbani, shuleni na jamii nzima kwa jumla (uk.11). Hali hii itawasaidia vijana kujua hatari mbalimbali za kujua hatari mbalimbali za kuwa wajawazito wakiwa bado wadogo. Kwa mfano, kabla msichana hajafikisha umri wa miaka kumi na sita, kizazi chake na sehemu nyingine za uzazi huwa bado hazijakua na kupanuka vizuri. Mifupa yake ya nyonga inakuwa bado ni midogo na hii husababisha matatizo wakati wa kujifungua.

Benedek, Kisaakye na Oberleiner (2002:41) wanaeleza kwamba, Shirikisho la Haki za Kibinadamu limechukua msimamo kuhusu haki za uzazi na upangaji uzazi, likitoa masharti ya kuingizwa kwa haki hizi katika mifumo ya elimu, pamoja na kuweka sheria zinazowaruhusu wanawake kuwa na haki ya kuchagua idadi ya watoto watakayokuwa nayo na vipindi vya wakati atakavyokuwa navyo baina ya kumzaa mtoto mmoja na mwingine. Upangaji wa uzazi unakumbwa na matatizo yanayowapa wanawake nafasi za chini za kijamii, uzalishaji wa mali, kiwango cha chini cha elimu miongoni mwa mambo mengine. Pia, kuna wanawake wanaonyimwa upangaji uzazi na elimu ya uzazi kutokana na vikwazo vya kidini, kitamaduni na kijamii.

Isitoshe, maafa mengi yanayotokana na uavyaji wa mimba yanaweza kuzuiwa kupitia upangaji uzazi. Upangaji uzazi utapelekea kuwako kwa uzuiaji kwa mimba zisizohitajika.

Aidha, kiuchumi kuwa na watoto wachache huwa kunapunguza muda anaotumia mwanamke kujifungua na kuwalea watoto. Wakati wanawake wachanga wanapokuwa na watoto wachache wanaweza kuchangia kiuchumi kuendeleza familia zao.

Kadhalika, nafasi ya kutosha baina ya kuzaliwa kwa mtoto na mwingine huhakikisha kwamba, mtoto amenyonyeshwa kwa kipindi kinachofaa na kukua, huku akiwa na nguvu ya kuwazuia watoto kutokana na magonjwa yanayowapata watoto wakiwa wachanga.

4.8 Ukombozi wa Kijinsia Kupitia Sekta ya Elimu

Elimu ni chombo muhimu ambacho kikitumiwa vizuri kinaweza kuleta ukombozi wa kijinsia. Maina (1995:51) akimrejelea Wollstonecraft (1972) anasema kuwa, elimu ndiyo msingi wa kila kitu maishani na kukosa elimu ni kukosa kitu cha thamani kubwa sana katika maisha. Anafafanua kuwa elimu ndiyo inayoweza kumfanya mtu ajielewe na aielewe jamii. Kama ilivyosikitizwa na waasisi wa ufeministi, elimu ni kitu cha msingi kabisa katika harakati za kupigania ukombozi wa mwanamke.

Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* jinsia zote mbili zinajitambuza na kutambulishwa kama wasomi hata kufikia elimu ya kiwango cha chuo kikuu. Farida, Lucy, Juma na Mary wamesoma

hadi chuo kikuu. Wote wanadhihirisha uhodari wao katika elimu. Rose anafanya vizuri masomoni kiasi cha kupewa tuzo za juu na chuo kikuu. Pia wahadhiri wanampongeza na kumpenda sana kutokana na matokeo yake bora. Hii ni ishara bora ya kuleta ukombozi wa kielimu katika jamii. Jinsia zote zinafaa kutambulishwa kama zilizo na uwezo wa kusoma hata kufikia kiwango cha uzamili na uzamifu au zaidi bila ubaguzi wa kijinsia wowote ule.

Kinachobainika hapa ni kwamba, jinsia ya kiume na ya kike zinajitambuza na kutambulishwa kama zinazopata elimu sawa tofauti na ilivyokuwa hapo zamani; ambapo jinsia ya kiume ndiyo ilivyokuwa ikitambuliwa katika kupata elimu, huku ile ya kike ikipuuzwa. Hata hivyo, kumekuwa na mabadiliko makubwa katika jamii, kwani watoto wengi wa kike wanapata elimu kuliko ilivyokuwa hapo zamani.

Mwandishi wa riwaya hii pia anaonyesha kuwa ushirikiano wa jinsia zote ni muhimu katika kuimarisha kiwango cha elimu katika jamii. Juma, Amos na Farida wanajitambuza kama watu wanaothamini umuhimu wa mijadala kabla ya kufanya mitihani. Wanajumuika pamoja katika mijadala hii.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa, unyonge wa mwanamke husababishwa na mfumo wa kijamii na hali hii inaweza kurekebisha kwa kusambaza kiwango cha elimu kwa watoto wote wasichana kwa wavulana. Wasichana wakipokea elimu bora watakuwa katika nafasi nzuri ya kupigania haki zao na pia kugombea nafasi mbalimbali katika jamii ambazo kwa sasa zinatawaliwa na wanaume.

4.9 Ukombozi Kupitia Kutoshiriki Ngono na Jinsia Inayoidhulumu ile Nyingine

Jinsia ya kike inajitambuza kama yenye ujasiri katika kujijitetea kijasiri, hususan wakati jinsia ya kiume inapotaka kushiriki mapenzi nayo. Inasimama kidete na kukataa kutumiwa na wanaume kwa minajili ya kujifurahisha. Ingawa mwanzoni Farida alikuwa kama tambara mbovu kwa kushiriki ngono na takriban kila mwanaume, tayari amebadilika na hataki mchezo wa wanaume tena. Farida anapoketi na wanaume wengine wanne katika kiti kimoja katika *Tertiary Bank* kuna mwanamume mmoja anayeelekea kumtaka Farida kimapenzi. Mwanamume huyu anapomfahamisha msichana huyu kwamba angetaka kumwulizia kitu baadaye, Farida anamjibu

kijasiri kwamba kama hamwulizi wakati huo na mahali hapo, asimwulize tena. Mazungumzo yao yanakuwa hivi:

“*Afterwards* ningetaka kukuuliza kitu.”

“Usiniulize chochote baadaye. Kama ni kuniuliza jambo niulie hapa na sasa. Ama kama huna lolote la maana usinipigishe mdomo bure.” Kwa kauli hii Farida alinyamaza (uk.139).

Mwandishi anafafanua kauli hii kwa kusema kuwa, Farida alikuwa amewashiba wanaume mpaka kooni, hasa wanaume wanaoonekana wataka kumchezea mtu na kumfanya mjinga (uk.139). Mwandishi hapa anampa Farida utambulisho wa mtu anayetambua makosa aliyofanya hapo awali ya kujamiiana na wanaume ovyo ovyo na kuamua kuyaacha kabisa baada ya kugundua kuwa jinsia ya kiume inamchukulia mwanamke kama chombo cha mapenzi.

Mwanamke mwingine anayejitambuza kama mtu asiyetaka kushiriki mapenzi na wanaume ni Juliet. Juliet anapooni kwamba ananyemelewa na Mhindi anayefanya kazi kwake, na ambaye tayari ana mke; anaamua kuondoka kwake na kwenda kufanya kazi ya nyumbani kwa Farida. Hataki kujihusisha na jinsia inayotaka kumdhulumu mwanamke kimapenzi.

4.10 Hitimisho

Katika sura hii tumelifanyia uchunguzi swala la ujitambozi na utambulisho wa kijinsia katika kupigania ukombozi wa kijinsia katika jamii. Ni swala ambalo linahitaji kuhusishwa kwa jinsia mbili ndipo lifanikiwe. Hata hivyo, jinsia ya kike ndiyo inayoonekana kuwa katika mstari wa mbele kupigania ukombozi huu, kwani imedhulumwa na ile ya kiume kwa muda mrefu. Kuna mambo kadhaa ambayo tumeyatolea maelezo kuhusu ukombozi wa kijinsia katika jamii.

Tumezungumzia kuhusu ukombozi wa kijinsia katika maswala ya kisiasa. Ukombozi huu ulianza zamani kule nchini Ufaransa na Marekani. Harakati za mwanzo za kupigania ukombozi huu zilihusisha wanawake kupigania haki ya kupiga kura katika jamii, jambo walilokuwa wamenyimwa kwa muda mrefu katika jamii. Usawa wa kijinsia umeanza kushuhudiwa katika baadhi ya mataifa barani Afrika ambapo wakati mmoja Afrika Kusini ilikuwa na nusu ya

wanawake katika Baraza la Mawaziri. Katika kazi nyingi za fasihi wanawake wanasawiriwa kama watu wanaopigania bila kurudi nyuma ukombozi wa jinsia ya kike katika kisiasa.

Ukombozi mwingine wa kijinsia tuliojadili hapa ni ule wa kidini. Jinsia ya kike ambayo imedhulumiwa na asasi hii ya jamii kwa muda mrefu, inajitambuza kama iliyopevuka kimawazo na kugundua kwamba dini inapalilia na kuendeleza udhalimu wa kijinsia. Wanaume nao hawajaachwa nyuma, kwani wanapigana na zile kauli za kidini zinazomkandamiza mwanamke katika jamii.

Pia jinsia ya kike imejitambuza kama iliyo na uwezo wa kupigania ukombozi wa kiuchumi. Jinsia hii imekuwa ikipigania nyenzo za uzalishaji mali ambazo zimekuwa zikidhitiwa na mwanamume kwa kipindi kirefu katika jamii. Kupitia hali hii jinsia imeweza kuanzisha shughuli kama vile za kibiashara ili kusukuma gurudumu la maisha. Wanawake wengi pia wanajiunga na ajira kuliko hapo awali.

Mbinu nyingine inayotumiwa na wanawake katika kuleta ukombozi wa kijinsia ni kuwa huru kutoa ushauri na maamuzi katika jamii. Tumeona kwamba kuna haja ya kuwa na usawa wa kijinsia katika ushauri na maamuzi katika viwango tofauti vya kijamii. Kwa sasa wanawake wengi hasa wale waliosoma wana uhuru wa kutoa mchango wa kiusemi kuhusu matatizo yanayozikumba ndoa zao.

Isitoshe, jinsia hii inatafuta ukombozi kupitia njia ya upangaji uzazi ambayo inashirikisha jinsia zote mbili. Jinsia hizi (hasa ile ya kike) zinapigania kuwako kwa huduma bora za uzazi, ili kutatua matatizo ya uzazi ambayo yamekuwa yakiwakumba wanawake. Pia, wanawake wanawashauri wanaume wapate idadi ndogo ya watoto ndipo waweza kushughulikia matakwa na mahitaji yao bila matatizo.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Katika utafiti wetu tulijikita katika mada ya “Ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*.” Utafiti wenyewe ulikuwa na sura tano. Tutatoa mukhtasari wa kila sura, huku tukionesha mambo tuliyogundua kutokana na utafiti wetu. Pia, tutaangalia manufaa ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika pamoja na malengo na matokeo ya nadharia tete za utafiti huu. Baadaye tutatoa mapendekezo ya utafiti wa siku za usoni.

5.1 Mukhtasari wa Sura Zote

Katika sura ya kwanza tulichunguza maswala tofauti tofauti yaliyohusiana na utafiti wetu. Tulizungumzia kuhusu tatizo la utafiti. Katika tatizo hilo tuliona kwamba, kulikuwa na pengo ambapo tafiti za hapo awali zilikuwa zimeshughulikia jinsia ya kike na kuipuuza ile ya kiume. Ni kutokana na pengo hili ambapo tuliamua kushughulikia jinsia zote mbili kwa pamoja kwa kurejelea riwaya ya *Maisha Kitendawili* ya John Habwe.

Aidha, tulitoa ufafanuzi kuhusu nadharia ambayo ingetuongoza katika utafiti wetu ambayo ilikuwa ni ile ya ufeministi wa Kiafrika. Tuliteua nadharia hii kwa sababu kazi tuliyoifanyia uchunguzi iliandikwa kwa misingi ya Kiafrika na ilikuwa na uhalisia mwingi unaopatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Nadharia ilikuwa na manufaa katika utafiti wetu. Tuliitumia katika kueleza asasi tofauti zinazopelekea kuwako kwa dhuluma za kijinsia. Tuliitumia pia katika kugundua mbinu zinazotumiwa na wanajamii ili kuleta ukombozi wa kijinsia.

Isitoshe, tuliyataja malengo ya utafiti wetu. Kulikuwa na lengo la kuchunguza jinsi ujitamuzi na utambulisho wa kijinsia unavyoathiriwa na asasi tofauti tofauti za jamii. Lengo lingine lilikuwa ni kubainisha jinsi umri tofauti tofauti ulivyoathiri ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika jamii inayomkandamiza mwanamke. Aidha, kulikuwa na lengo la kushughulikia ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika kupigania ukombozi katika jamii ukombozi katika jamii inayomkandamiza mwanamke.

Katika sura hii pia tulitaja nadharia tete ambapo tulikuwa tunanua kuzifanyia uchunguzi katika utafiti wetu. Baada ya uchunguzi wetu tuligundua mambo kadhaa kuhusiana na nadharia tete hizo. Tuligundua kwamba ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia unatofautiana kwa kiwango kikuwa kutokana na sababu za kitamaduni, kiuchumi, kisiasa na kadhalika. Pia tulipata kuwa umri tofauti tofauti huathiri ujitambuzi na utambulisho wa vijana na wazee katika maswala mengi yanayopatikana katika jamii. Watoto wadogo ndio kwa kiwango kikubwa wanaonyesha ujitambuzi tofauti wakilinganishwa na vijana na wazee. Jambo lingine tulilogundua ni kwamba, jinsia ya kike imefanikiwa kwa kiasi fulani katika kujitambuza na kutambuliwa kama inayopigania ukombozi wa kijinsia kuliko ile ya kiume.

Katika sura ya pili tumefanya uchunguzi kuhusu ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kwa mujibu wa vipengele au asasi tofauti za kijamii. Tulikifanyia uchunguzi kipengele cha utamaduni tukijikita katika baadhi ya maswala yake kama vile ndoa, tohara, urithi miongoni mwa mengine. Tuliona kuwa jamii za Kiafrika hutilia maanani swala la tohara kwa jinsia zote mbili. Kuhusu ndoa tumeona kwamba utamaduni unapelekea kukandamizwa kwa mwanamke katika jamii na jinsia ya kiume. Tulitoa maelezo pia kuhusu jinsia na utumishi wa nyumbani ambapo tumepata kwamba, jinsia ya kike huwa na majukumu mengi ya kinyumbani kuliko ile ya kiume. Tulikuwa pia katika nafasi ya kushughulikia ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika kipengele cha uchumi. Hapa tulipata kuwa, wanaume ndio wanaomiliki nyenzo za uzalishaji wa mali kushinda wanawake. Kuhusu kipengele cha dini tuliona kuwa jinsia ya kiume imetambuliwa na dini zaidi kuliko ile ya kike. Dini imemweka mwanamke chini ya mwanaume siku zote. Tulijadili pia kuhusu jinsi jamii inavyoitambua jinsia. Jinsia ya kiume inatukuzwa na jamii huku ile ya kike ikiwa inakandamizwa kwa njia moja au nyingine na jamii hii kadhalika.

Katika sura ya tatu tulichunguza ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia kwa misingi ya umri. Tuligawanya umri katika matapo matatu: umri wa utotoni, ujanani na uzeeni. Katika kutoa maelezo tulionyesha jinsi watoto wanavyojitambuza na kutambulishwa katika jamii. Kuhusu malezi yao tumeona kwamba wazazi wana wajibu wa kuwalea na kuwaelekeza watoto wao vyema. Tuligundua pia kuwa watoto wa jinsia zote wanatambulishwa kama wanaokosa elimu katika jamii. Pia tulitambua kwamba, watoto huwa wanajihusisha na vitendo kama vile uchezaji.

Katika sura hii pia tulijadili kuhusu ujitambuzi na utambulisho wa vijana katika jamii. Tulizungumzia kuhusu kupatikana na kukosekana kwa elimu baina ya jinsia zote mbili. Baadhi ya jamii hazithamini elimu ya mtoto msichana, kwani wanamwona kama mtu wa kuolewa tu na asiyeleta manufaa kwa familia au jamaa yake. Kadhalika, tulitambua jinsi swala la mapenzi linavyoathiri elimu ya vijana. Katika sura hii pia tumechunguza pia ujitambuzi na utambulisho wa wazee katika jamii. Tumetoa maelezo kuhusu jinsi tofauti wazee wanavyojitambua na kutambulishwa katika malezi ya watoto wao. Wazee wengi pia wanaonekana kutilia swala la ushirikina maanani bila kuangalia athari yake kwao wenyewe na jamii. Aidha, baadhi ya wazee wanatambulishwa kama wabadhirifu wa fedha au mali, huku wengine wakitambulishwa kama wanaopenda starehe na anasa.

Sura nyingine ambayo tuliitolea ufafanuzi ni sura ya nne ambayo ilijihusisha na ujitambozi na utambulisho wa jinsia inayotaka kujikomboa. Hapa tulitoa ufafanuzi kuhusu namna jinsia inavyopigania ukombozi wake katika jamii. Tuligundua kwamba jinsia, hasa ile ya kike inaweza kujikomboa kisiasa ikiwa itaingiliana na maswala ya kisiasa.

Inaweza pia kujikomboa kupitia kwenda kinyume na maswala ya kidini ambayo yanapelekea kudhulumiwa kwayo. Tuliona pia kuwa, kuna pia haja ya jinsia kushirikiana na kuungana, ili kusaka ukombozi wa kijinsia katika jamii. Kwa kwenda kinyume na vipengele vya kitamaduni vinavyomkandamiza mwanamke, kunakuwa na ukombozi wa kijinsia. Aidha, tulitambua kuwa, kando na kuwako kwa utoaji wa maamuzi katika jamii, jinsia anasaka ukombozi wake kupitia kwa upangaji wa uzazi. Ukombozi mwingine ambao jinsia umekuwa ukiutumia ule wa kujipatia viwango sawa vya kielimu katika jamii.

5.2 Mapendekezo

Katika utafiti wowote ule mtafiti huwa anatoa mapendekezo kuhusu utafiti utakaofanywa na watafiti baadaye. Hii ina maana kwamba, mtafiti huwa anaona kwamba kuna pengo liliko katika utafiti wake ambalo linafaa kuzibwa na watafiti wa siku za halafu. Tunatoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wa hapo baadaye:

- (i) Ujitambuzi na utambulisho wa jinsia ya kiume ni ule wa kidhalimu.
- (ii) Vijana wameshindwa kupigania ukombozi wao katika jamii.

MAREJELEO

Africa Guardian Africa Network: Defining African Feminism kutoka kwa www.theguardian.com>*World>Africa*, retrieved on 30/4/2015.

African Economics Research Consortium, (1995), *Addressing Gender Bias: Graduate Training in Economics*, AERC on Women.

Asikia, R.I. Celebrating African Feminism: Its Essence kutoka kwa www.academia.edu/8281460/celebrating_African-Feminism_Its_Essence, retrieved on 30/4/2015.

Ayisi, O.E., (1979), *An Introduction to the African Culture*, (2nd ed.), Nairobi: East African Educational Publishers.

Barbara, E., (1998), *Lets Discuss Women's Rights*, England: Wayland Publishers.

Bressler, C.E., (1999), *Literary Theory and Criticism: An Introduction to Theory and Practice*, New Jersey: Prentice Hall.

Barnett, R.L., (1985), *People Making People: Child Development Context*, London, Melbourne, Sydney, Auckland and Johannesburg: Hutchinson Publishers.

Barry, P., (2002), *Beginning Theory: An Introduction to Literary Theory*, (2nd ed.), Manchester and New York: Manchester University Press.

Benedek W., Kisaakye M. and Esther O., (2002), *The Human Rights of Women: International Instruments and African Experiences*, London and New York: Zed Books.

Bertoncini, E.Z. et al, (2009), *Outline of Swahili Literature*, (2nd ed.), Leiden and Boston: Brill.

Buliba, A., Gwachi M. na Matinde R., (2014), *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*, Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Burhani, Z., (1987), *Mwisho wa Kosa*, Longman, Nairobi.

Carol, F.R., (1997), *Business and Feminine Principle: The Untapped Resource*, Boston, Oxford, Johannesburg, Melbourne, New Delhi and Singapore: Butterworth-Heinemann.

Chisholm, L. and September J., (eds.), (2005), *Gender Equity in South African Education 1994-2004: Perspectives from Research*, Human Science Research Council.

Chacha, W.C., (2013), *Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Nguzo Mama na Mama Ee, Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.

Coats, M., (1994), *Women's Education*, Society of Research in Higher Education and Open University Press.

- De Beauvoir, S., (1953), *The Second Sex*, Jonathan Cape, London.
- Emma Day and Umra Omar, The Open Society Initiative for Eastern Africa, Kukuza Demokrasia, OSIEA, Nairobi, kutoka kwa www.OPENSOCIETYFOUNDATION.ORG, retrieved on 28/6/2015.
- Gill, G., (1999), *Choices: A Choice for Young People*, Oxford: Macmillan Publishers.
- Habwe J. (2000), *Maisha Kitendawili*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Habwe, J., Matei, A.K. na Nyonje J., (2010), *Darubini ya Isimujamii kwa Shule na Vyuvo*, Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hanke, R., (1998), "Theorizing Masculinity with/in the Media", *Communication Theory* 8, (2) 183-203.
- Idara ya Watu Wazima Kenya, (1989), *Panga Uwe na Familia Ndogo Yenye Afya na Furaha*, Nairobi: Oxford.
- Iribemwangi, P.I. na Mukhwana A., (2011), *Isimujamii*, Nairobi: Focus Publishers.
- Karinge, J.W., (2013), *Usawiri wa Ndoa katika Riwaya ya Unaitwa Nani?*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Katola, E., (2006), "Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili," *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Kezilahabi, E., (1971), *Rosa Mistika*, Nairobi: Kenye Literature Bureau.
- Kinyua, A.M., (2011), "Riwaya ya Unaitwa Nani? Inavyoshughulikia Swala la Ukombozi wa Mwanamke," *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Kipyegon, P.E., (2013), "Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke katika Natala na Kifo Kisimani," *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Kohen, W.J., (1993), *Women in Society*, New York, London and Routledge: Marshall Cavendish.
- Kweyu Dorothy, (2007), "A Critical Analysis of Patriarchy and Masculinity in Kezilahabi's *Rosa Mistika* nd Kichwa Maji," Unpublished MA Thesis, University of Nairobi.
- Madumulla, J.S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Dar es Salaam na Nairobi: Mture Educational Publishers na Phoenix Publishers.
- Magoma, N.H., (1997), "Mwamko wa Mwanamke katika, katika Tamthilia Nne za Penina Muhando," *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.

- Maina, V., (2005), “Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi Mbili za Shaaban Robert: Utenzi wa Haki na Utenzi wa Adili,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Maingi, H.G, (2011), “Upembezaji wa Mwanamke kama Udokezi wa Nafasi ya Mwanamke katika Utenzi wa Fatuma,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Maobe, O.J., (2011), “Ukombozi wa Mwanamke katika Riwaya za Habwe,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Mbilinyi, J.M., (1969), *The Education of Girls in Tanzania*, Dar es Salaam: Institute of Education University College.
- Mbiti, J.S. (1995), *Introduction to African Religion (2nd ed.)*, Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mdee, J.M. na wenzake, (2009), *Kamusi Kamili ya Kiswahili*, Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mdee, J.S., Njogu K. na Shafi A., (2011), *Kamusi ya Karne ya 21*, Nairobi: Longhorn Publishers.
- Millet, K., (1977), *Sexual Politics*, London: Virago Press.
- Mirikau, S.A., (2011), “Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Wamitila K.W.,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Mlacha, S.A.K. na Madumulla, (1995), *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mogere, O.J., (2003), “Uhakiki wa Riwaya za Ahmed Mohamed katika Misingi ya Ufeministi,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Mohamed, S.A., (1995), *Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*, Nairobi: East African Educational Publishers.
- Moi, T., (1985), *Sexual/Textual Politics*, London and New York: Meltuen.
- Momanyi, C., (2006), *Tumaini*, Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Mucheke, S., (2001), *What Every Man Should Know, (Revised ed.)*, Nairobi: Family Planning Association of Kenya.
- Muhanda, B.H., (2011), “Nafasi ya Dini katika Ndoa: Tathmini ya Utengano na Paradiso,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.

- Mugambi, P.M., (1982), “Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya Zilizochapishwa,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Mulacha, S.A.K. na Madumulla, J.S., (1995), *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.
- Mutua, J.M., (2007), “Mitazamo ya Vijana na Wazee Kuhusu Ukombozi wa Wanawake,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- NACADA, (2006), *Frequently Asked Questions on Substance Abuse*, kutoka kwa www.nacada.go.ke, retrieved on 2/2/2015.
- (2011), *For A Drug Free Nation: A Report on the National Alcohol and Drug Abuse Research Workshop*, Nairobi: Kenya Institute of Administration.
- Ndambuki, R., (2009), *African Girl: A Girls’ Guide to Teenage Body Care*, Nairobi: Aura Books.
- Ndung’o, C.M., (1985), “Mwanamke na Maendeleo ya Kihistoria,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Neil Duncan, (1999), *Sexual Bullying: Gender Conflict and Pupil Culture in Secondary Schools*, London and Newyork: Routledge.
- Nguta, K. H., (2011), “Fani na Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia ya Pango na Mama Ee,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Njogu J. na Chimerah R., (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Obure, E.M, (2012), “Dhuluma Dhidi ya Vijana wa Kike katika Riwaya za Rosa Mistika na Tumaini,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Ohly, R. (1981), *Aggressive Prose of the Seventies*, Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.
- (1990), *The Zanzibarian Challenge: Swahili Prose in the Years 1975-1981, Vol. 3*, Windhock: African Studies Academy.
- Onyoni, J.K., (2012), “Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Natala na Mama Ee,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.
- Ronaldi, M., (2002), *Unstable Categories: Comparing the Politics of Gender in Early 1990s in Canada and South Africa*, Vol. 14, EBSCO.
- Republic of Kenya, (2010), *The Constitution of Kenya*, Nairobi: The Government Printer.

- Richmond, A.M., (1992), *Masculine and Feminine: Gender Roles over the Life Cycle*, New Delhi: Sage Publishers.
- Robbins, R., (2000), *Literary Feminisms*, Hampshire: Palgrave.
- Salisbury, J. and Riddell, (2000), *Gender, Policy Challenge and Educational: Shifting Agendas in the UK and Europe*, London and New York: Routledge.
- Steady, F.C., (1979), "African Feminism. A world Wide Perspective" in Terbog-penn, *et al* (eds.), *Women in Africa the Diaspora*, Washington: Howard University Press.
- The National Conference on HIV/AIDS and the Family in Kenya, (2004), AAWORD Kenya Chapter (Association of African Women for Research and Development), held at Silver Springs Hotel, Nairobi, Kenya, on 29-30 November 2001, kutoka kwa www.twaweza.org, retrieved on 5/7/2015.
- Timammy, R. and Swaleh, A., (2013), "Characterization and Construction of Gender in John Habwe's *Maumbile si Huja*" in *International Journal of Education and Research*, vol. 1, No. 9.
- TUKI, (1990), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, (Toleo la Pili)*, Nairobi: Oxford University Press.
- United Nations, *10 Years of Educating Through Pictures UNFPA Graphic Narrative Series Book 10: Cultural Sensitization*, Blue Eyes Ltd.
- Utambulisho Swahili, Kuwakinga Watetezi wa Haki za Kibinadamu kutoka kwa www.opensocietyfoundation.org, retrieved on 10/7/2015.
- Wafula, R.M., (1999), *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maeneleo Yake*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Walibora, K, (1996), *Siku Njema*, Longhorn Publishers, Nairobi.
- Wamitila, K.W., (1999), *Nguvu ya Sala*, Longhorn Publishers, Nairobi.
- (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Phoenix, Nairobi.
- (2003), *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Focus Publishers, Nairobi.
- (2008), *Kanzi ya Fasihi: Misingi na Uchambuzi wa Fasihi*, Vide-Muwa Publishers, Nairobi.
- Woolf, V., (1929), *A Room of One's Own*, Horgath, London.
- waywww.edu/8281460/celebrating_African_Feminism, retrieved on 20/5/2015.
- www.mavalapeter.blogspot.com/2014/12/a-define-african-feminism-b-discuss-way, retrieved on 20/5/2015.

Young, J., (2008), *Teach Yourself Christianity, (New ed.)*, London: MacGraw-Hill Companies.